

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

#### MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 2 AGOSTI, 2012**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

#### DUA

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

#### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

#### **NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mzime vipasa sauti vyenu maana naona vinaingiliana.

Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaingia hatua inayofuata.

## **MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Leo ni siku ya Alhamisi lakini tulishatoa taarifa kwamba Waziri Mkuu yuko safarini kwa hiyo kama kawaida hatutakuwa na kipindi cha maswali hayo. Maswali ya kawaida yapo machache na atakayeuliza swali la kwanza ni Mheshimiwa Vita R. M. Kawawa.

Na. 310

### **Fedha za Uendeshaji Shule za Msingi**

**MHE. VITA R. M. KAWAWA** aliuliza:-

Kumekuwa na makato ya fedha za uendeshaji wa Shule za Msingi - *Capitation* bila taarifa hali inayofanya Walimu kuwa na hali ngumu ya uendeshaji wa shule hizo.

Je, Serikali ina mipango gani ya kuhakikisha kuwa, fedha za *Capitation* zinatoloewa kama ilivyotarajiwa ili kupunguza matatizo wanayopata wazazi wa wanafunzi kwa kuchangia gharama za uendeshaji shule?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (*MMEM*) imepanga kila mwanafunzi wa Shule ya Msingi kupata shilingi 10,000 kama fedha za uendeshaji wa shule (*Capitation Grant*) kwa mwaka. Upatikanaji wa fedha unatokana na mapato ya Serikali Kuu na fedha za nje kutoka kwa Wadau wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu. Serikali wakati wote imekuwa na dhamira ya kuona kila Halmashauri inapata ruzuku hii kila baada ya miezi mitatu kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Aidha, Elimu ya Msingi nchini inatolewa bure kwa Serikali kugharamia huduma hiii isipokuwa katika mazingira ambayo kwa ridhaa ya wazazi na Kamati za Shule, Wazazi wameamua kuchangia uboreshaji wa huduma, mbalimbali ikiwemo kutoa uji au chakula cha mchana shulenii.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya *capitation* kwa shule za msingi jumla ya shilingi bilioni 50,029,990,000 ambapo Halmsahauri ya Wilaya ya Namtumbo ilitengewa shilingi 290,453,000. Hadi mwezi Juni, 2012 jumla ya shilingi 19,410,768,698 zilikuwa zimepelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ilipokea jumla ya shilingi 102,230,877. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 52,545,074,000 kwa ajili ya uendeshaji wa shule za msingi yaani *Capitation Grant*.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele cha kupeleka fedha za uendeshaji wa

shule katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kadri ya upatikanaji wa bajeti ili kuboresha utowaji wa elimu nchini. Kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kusisitiza maelekezo ya Serikali kwa Halmashauri kuhakikisha kuwa fedha zote za uendeshaji wa shule na za maendeleo zikishapokelewa katika Halmashauri zipelekwe shuleni ndani ya siku 14. Wazazi wasichangishwe mchango wowote shuleni pasipo ridhaa ya wazazi wenyewe na Kamati za Shule.

**MHE. VITA R.M. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa, Serikali ililetä fedha za *capitation* chini ya 50% na kwa kuwa, Nambumto ilipangiwa shilingi milioni 290,453 kama Waziri alivyosema na zikapatikana shilingi milioni 102,230,871/= hii ilisababisha Walimu Wakuu kuita Kamati za Shule kuwaomba wazazi wachangie gharama za uendeshaji wa shule hizo. Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa fedha tunazotenga Bungeni ziwe zinapelekwa fedha kamili kama zilivyokusudiwa?

Pili, kwa kuwa, pia kulikuwa na maelekezo kutoka TAMISEMI kwamba 10% ya fedha hizi zitengwe kwa ajili ya michezo, nayo pia ilipunguza zaidi fedha za kugharamia uendeshaji wa shule. Je, Serikali haioni sasa hivi wakati umefika wa kutenganisha fedha za shughuli za uendeshaji wa shule na fedha za michezo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, napenda nikiri kwamba kweli fedha ambazo tulikuwa tumetenga mwaka wa fedha 2011/2012, hatukuzipeleka zote na hii inatokana na kauli ya msingi kwamba fedha hizo tulizopeleka za *capitation* zinatokana na mapato yaliyokusanywa na Serikali na kwa hiyo mapato kwa kipindi kilichopita hayakukamilika. Mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba fedha hizi zinazopangwa ziweze kupelekwa zote kama ambavyo zimeamuriwa. Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu, tuna uhakika tutafikisha fedha hizi kwenye shule kama ilivyokubalika na kama ambavyo tumepanga na kadri ambavyo Bunge limeidhinisha.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ni kweli kwamba fedha za *capitation* tunapozipeleka mashulenii nazo zimewekwa katika madaraja yake. Kwa shule za msingi, zimetengwa katika asilimia, tuna asilimia 40 ambayo inanunua vitabu na ununuzi wa vifaa mbalimbali lakini kuna asilimia 20 ya utawala, asilimia 20 ya vifaa, mitihani 10, ukarabati asilimia 20, utawala 10 na hii sasa ndiyo inafanya asilimia 100 ya fedha ile.

Mheshimiwa Spika, eneo la vifaa ambalo ni asilimia 20, mionganii mwa vifaa ambavyo vinatakiwa vinunuliwe ni pamoja na vitabu au vifaa vyaa michezo. Kwa maagizo ambayo yalijitokeza mwaka huu kwamba fedha ya michezo ilichukuliwa kutoka kwenye vifaa ni ile fedha ambayo kila shule ilitenga kwa ajili ya kununua vifaa na kwa kuwa tumerudisha michezo katika shule za msingi nchini na kwa hiyo basi

uendeshaji wa michezo ngazi ya Kata na Wilaya unatokana na mikakati inayotolewa, kuna fedha ile ya *capitation* ambayo imekwenda kwenye shule zile baada ya makubaliano hayo. Kwa kwa hiyo basi, tutaendelea kuboresha uendeshaji wa michezo nchini kwa kutenga bajeti pekee mbali ya *capitation* ili sasa kuwawezesha Wakuu wa Shule kutokupata tatizo la matumizi ya fedha kidogo ambayo tumewatengea kwenye maeneo yao.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa kueleza Halmashauri na Shule kwamba michango inayotolewa na wazazi ni lazima ikubaliwe na wazazi pamoja na Kamati za Shule lakini Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kwamba hizi pesa nyingine ambazo amesema 20% zinazonunua vifaa vingine hazitumiki sawasawa na badala yake wazazi nchi nzima hasa Mkoa wa Singida wanachangishwa pia fedha za kununulia chaki na vitasa vya madarasa? Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie, hizi fedha ni za nini? Nashukuru sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumeagiza na tumeelekeza pia kwa Wakuu wa Shule, Maafisa Elimu na Halmashauri kwa ujumla mpaka shulenii, suala la shule kuwachangisha wazazi tumeelekeza na kama ambavyo leo nimesisitiza kwenye jibu la msingi

kwamba hakuna michango yoyote ile ambayo Mwalimu Mkuu au Walimu wanaweza kukaa wao wenyewe wakaamua kwamba hapa kuwe na michango ya aina fulani. Michango yote ni lazima itaamuriwa na wazazi wenyewe kupitia mikutano ya wazazi shulenii na kwa kufanya hilo fedha kidogo tuliyoituma ya *capitation* ambayo sasa inatakiwa kununua vifaa ikiwemo na upatikanaji wa chaki na vitu ambavyo ni vidogovidogo shulenii, ndiyo vinatumika kwa fedha hiyo na kama Mwalimu Mkuu ana upungufu mkubwa anatakiwa kuijulisha Halmashauri kwamba tunahitaji huduma hii kwenye eneo hilo. Hakuna umuhimu wa kumchangisha mzazi kununua kitasa badala ya kutumia njia halisi ya kwenda kumjulisha mwajiri ambaye tumempa dhamana ya kuzihudumia hizi shule ili huduma hii iendelee na kuwaondolea usumbufu wazazi bila sababu na hii ni kwa shule za msingi na sekondari vilevile.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na kwamba pesa hizi za *capitation* zinakuja chini ya kiwango, je, ni kwa nini viwango hivi hutofautiana kati ya Halmashauri na Halmashauri? Kwa mfano, kuna Halmashauri mwanafunzi anaweza kupata shilingi 6,000/= na Halmashauri nyingine mwanafunzi anapata shilingi 5,000/=?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba fedha hizi zinapogawiwa katika Halmashauri zinatofautiana, utofauti unatokana na kigezo kimojawapo kikubwa kwamba fedha ya

*capitation* inatumwa kwenye Halmashauri kwa idadi ya wanafunzi waliopo kwenye Halmashauri husika na hiyo ndiyo inapelekea kutofautiana kutoka Halmashauri moja mpaka nyingine.

**SPIKA:** Tumekuwa na maswali zaidi ya manne katika swali hili kwa hiyo tunaendelea na swali linalofuata nalo litaulizwa na Mhonga Said Ruhwanya.

Na. 311

### **Serikali Kushindwa Kuwalipa Walimu Wapya**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Hivi karibuni Serikali iliwapangia vituo vyatya kazi Walimu katika maeneo mengi nchini, lakini imeshindwa kuwalipa malipo yao hali iliyosababisha maandamano na malalamikio mengi:-

(a) Je, kwa nini Serikali iliwapangia kazi Walimu hao bila kuandaa malipo yao hali iliyosababisha wakate tamaa na kukimbia kwenye vituo vyatya kazi?

(b) Je, Serikali inatatuaje tatizo hili la uhaba wa Walimu ikiwa hata wale wachache wanaopatikana imeshindwa kuwalipa stahili zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya,

Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Januari, 2012, Serikali iliwapanga jumla ya Walimu 24,431 (wakiwemo Walimu wa Msingi 11,243 na Sekondari 13,188) kwenda kufundisha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wakati huohuo Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 7,325,976,850/= kwa ajili ya kulipia stahili za posho ya siku saba na nauli kwa Walimu hao. Kutokana na changamoto ya baadhi ya Walimu kuripoti na kuondoka katika vituo baada ya kupokea fedha, Serikali ilituma fedha hizi kwa awamu mbili. Mwezi Januari 2012, jumla ya shilingi bilioni 3,339,152,500 ili Walimu wakifika vituoni waweze kulipwa bila usumbufu na awamu ya pili shilingi bilioni 3,986,824,3500/= zilitumwa mwezi wa pili 2012. Baadhi ya changamoto zilizokuwepo na kusababisha malipo kuchelewa kwa baadhi ya Walimu ni baadhi ya Walimu kuripoti bila ya kuwa na vyeti halisi na kuwasilisha madai ya nauli yenye viwango vikubwa kuliko uhalisia.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inalitatua tatizo la uhaba wa Walimu kwa kuendelea kushirikiana na sekta binafsi kuongeza udahili katika Vyuo vya Ualimu na kuajiri Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wanaofuzu katika Vyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu vya Serikali na vya Binafsi. Mwaka 2010/2011, jumla ya Walimu 9,226 (Shahada 4,920 na Stashahada 4,306) walipangwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na mwaka 2011/2012, jumla ya Walimu 24,431 (Msingi 11,243 na Sekondari 13,188) wamepangwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na jitihada za kuwafundisha Walimu katika Vyuo mbalimbali vyataga Ualimu na Vyuo Vikuu na kuwaajiri kila wanapohitimu. Aidha, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia hususani katika shule za pembezoni kwa kuhimiza ujenzi wa nyumba za Walimu ili wanaopangwa waweze kupata mahali pa kuishi. Kwa jitihada zillizopo, Serikali imedhamiria kupunguza tatizo la Walimu kwa 90% ifikapo mwaka 2014.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, aliyoyasema Mheshimiwa Waziri ni kweli kwamba ni Walimu wapya ambao walijiriwa katika kipindi cha Januari 2012 ndiyo niliowalenga lakini tulishuhudia katika vyombo vyahabari Walimu wengi wapya baada ya kucheleweshewa malipo yao walikuwa wakiandamana mpaka kwenye ofisi za Halmashauri na wengine kwenda mpaka ofisi za Mkoa kwa sababu walicheleweshewa malipo yao na walilipwa siku saba badala ya siku 14 kwa sababu walikuwa wameshakaa zaidi ya siku 14 lakini vilevile walilipwa nauli tu hawakulipwa pesa za mizigo yao. Mpaka sasa kuna baadhi ya Walimu wa Shule za Msingi na wengine wa Shule za Sekondari hawajalipwa mshahara wa mwezi wa pili. Naomba kufahamu kwa nini Serikali inaendelea ku-create madeni kila wakati?

Swali la pili, naiuliza Serikali hivi kwa mtindo huu haioni kwamba inazidi kutengeneza au kusababisha matatizo ya Walimu na elimu nchini kwa sababu Walimu wengi badala ya kufundisha wanakuwa wanafikiria kudai madai yao na matokeo yake watoto wetu wanakosa elimu bora? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nieleze kwamba kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa mwaka 2011, mtumishi yeoyote wa Serikali anapokwenda kuripoti kwenye kituo atalipwa siku saba na siyo siku 14 na hili ndiyo lilipelekea kuwa na mkanganyiko wa Walimu wapya waliokwenda kuripoti walikuwa wakidhani malipo ni ya siku 14 badala ya siku saba na kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi kwamba kwa kuwa tulipata uzoefu wa kipindi kilichopita kwa Walimu wapya wanapokwenda kwenye Halmashauri wanapolipwa fedha zao zote wanaondoka, hawaripoti kazini maana yake wanaondoka na zile fedha. Awamu hii tuliiimarisha zaidi tabia hiyo ili isiweze kujrudia kwamba Mwalimu akija ni lazima kwanza awasilishe vyeti halisi na wakati anafanya zoezi hilo tutampa fedha yake nusu ili aendelee na taratibu za ofisini na kwenda kuripoti, akisharipoti anamaliziwa fedha iliyobaki. Eneo hilo ndilo ambalo liliteta mkanganyiko kwa sababu wao wanajua kwamba ukifika kwenye kituo unalipwa fedha zote. Kwa uzoefu tuliuopata tulilazimika kwenda kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo pia lilichelewesha jambo hili ni pale ambapo mtumishi

mpya anapotakiwa kwenda kuripoti kwenye kituo chake ni lazima awe na vyeti halisi vya masomo ili kuthibitisha kwamba huyu aliyejeka ndiye mwenye vyeti hivi ili pia aweze kuendelea na taratibu nyingine za utumishi.

Mheshimiwa Spika, wale ambao hawajalipwa mshahara wa mwezi Februari, utaratibu wa ulipaji wa mishahara ni kwamba mtumishi anaporipoti kituo cha kazi kabla ya tarehe 15 tuna uhakika kwamba atalipwa mshahara wa mwezi ule lakini anapokuja kuripoti baada ya tarehe ile, taratibu za kiutumishi haziwezi kumwezesha kupata mshahara ndani ya mwezi huo kwa sababu kunakuwa na *process* ya kuhakiki na kuona kwamba yeye ni mtumishi halali. Walimu wengi tuliowapangia mwaka huu 2012 kwenye vituo vya kazi tulitoa matangazo tarehe 01/2/ na kwa hiyo wengi walikuja kuripoti baada ya tarehe 15 na ndiyo sababu hawakuweza kupata mishahara ya mwezi Februari. Kwa sasa tatizo hilo la kukosa mishahara linatokana na taratibu za utumiaji wa mtandao mpya. Halmashauri na Utumishi tumejiweka vizuri kuhakikisha kwamba hakuna tatizo tena la mtumishi kutokupata mshahara wake wakati wa utumishi.

Mheshimiwa Spika, suala la malipo ya Walimu, madeni mbalimbali ambayo yamepelekea Serikali kuhakiki upya kwenye maeneo haya. Taarifa za ulipaji wa madeni kwenye maeneo yote, madeni yote ya Walimu yaliyohakikiwa yameshalipwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na madeni haya yalikuwa pia na Wizara ya Elimu lakini taarifa tulizonazo, Wizara ya Elimu imekamilisha.

Mheshimiwa Spika, pia nataka nieleze jambo moja kwamba, katika ulipaji huu, zipo Halmashauri tano zilipata fedha pungufu nazo ni Kongwa, Dodoma (M), Chamwino, Kilosa na Same. Wilaya hizi hadi kufikia tarehe 30, waliahidi kuwa watakuwa wameshazipelekea jumla ya shilingi milioni 405 ambazo tunatarajia zitakuwa zimeshafikishwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na kwa Walimu wachache amba walikuwa wamebakia watakuwa wameshalipwa. Kwa hiyo, ulipaji wa madeni ya Walimu umeendelea vizuri na taarifa zimeendelea kutolewa na nimezitoa hati kwenye taarifa zangu nilipokuwa najibu maswali ya msingi wakati uliopita, ahsante.

**MHE. MODESTUS D. KILIFI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba madai mbalimbali ya Walimu kwa sehemu kubwa yameshalipwa lakini hivi tunavyozungumza kuna mgomo unaendelea, je, Mheshimiwa Waziri anaweza akaeleza nini hasa ambacho hawa Walimu wanagomea?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba mgomo huu wa Walimu sasa hivi hauhusishi tatizo lile ambalo lilikuwa limewasilishwa na Chama cha Walimu (CWT) mwaka jana mwezi Juni, ambalo ni madeni mbalimbali ya Walimu, yale ya mishahara na yale yasiyokuwa malimbikizo ya mishahara. Ndiyo hili ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri amelijibu kwa ufasaha kwamba, deni lile ambalo jumla yake lilikuwa shilingi bilioni 52 mpaka kufikia tarehe 30

mwezi Juni mwaka huu tumelikamilisha, ukiacha kasoro ndogondogo kwa baadhi, hatuna tena deni la Walimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili la mgomo limekuja baada ya Serikali na CWT kutoweza kuelewana au kupatana au kumaliza tatizo la madai mapya ya Walimu ya kutaka kuongezewa mshahara kwa zaidi ya asilimia 100, pia wapewe posho ya kufundishia ya asilimia 55 kwa Walimu wa Sayansi na asilimia 50 kwa Walimu wa Masomo ya Sanaa, pia wapewe posho ya asilimia 30 ya mazingira magumu. Kwa hivyo, jumla ni nyongeza ya mshahara ya asilimia 180 ambayo Serikali hii haimudu mzigo huo. Tumeshindwa kupatana katika hilo na Walimu wameamua kwenda kwenye mgomo.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami ili niulize swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kuna Halmashauri ambazo ziko pembezoni kama Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ambapo Walimu hawa vijana wakipangwa wanapelekwa shule za vijiji ambako hakuna vivutio vyta maisha kama umeme na lami, je, Serikali haioni kwamba umefika wakati kwa Walimu wanaokwenda sehemu hizo kupewa malipo zaidi kama *hardship allowance*?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZOYA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, suala hili tumelitafakari sana Serikalini na tunaendelea kulitafutia namna ambayo itaweza kuwapunguzia uzito watumishi wa umma katika sekta mbalimbali ambao wanaenda katika

maeneo yote yenye changamoto. Mwanzoni tulifikiria tulifanye kwa Walimu peke yake, lakini katika maeneo yale tunayoyazungumza kwamba ni ya changamoto hapohapo yuko Daktari, Muuguzi, Mkunga, Mgani na watumishi kadhaa wa umma ambao bila shaka na wao wangestahili kupata posho hii ya ziada ya mazingira magumu. Kwa hiyo, tunaifanyia kazi kwa upana wake badala ya kuchukua sekta moja tu halafu ukawaacha watumishi wengine wa umma wakiwa hawana chochote. (*Makofi*)

Na. 312

### **Ujenzi wa Barabara ya Korogwe – Soni**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI** aliuliza:-

Barabara ya Korogwe – Kwashemshi – Bumbuli – Soni imo kwenye llani ya Uchaguzi kwa lengo la kujengwa kwa kiwango cha lami kutokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2010.

Je, Serikali itaanza lini ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijiji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Korogwe - Kwashemshi - Bumbuli - Soni, ni barabara ya Mkoa yenye urefu wa kilomita 77.51 na inahudumiwa na Wizara kupitia *TANROADS*. Ni kweli kwamba katika llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, barabara hiyo imeainishwa kufanyiwa upembuzi na usanifu ikiwa ni maandalizi ya kujenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimwa Mbunge kuwa, Wizara imejipanga kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais na llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Serikal kupitia Wizara ya Ujenzi, imepanga kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mwaka wa fedha 2013/2014. Ujenzi utaanza baada ya kukamilika kwa usanifu na upatikanaji wa fedha.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa nini utekelezaji wa ahadi hii ya Mheshimiwa Rais unasuasua? Je, Wizara inamdhara Mheshimiwa Rais? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara haiidharau ahadi ya Rais. Ni kwamba Rais aliahidi na sisi tumeshaipangia bajeti tutaanza katika mwaka wa fedha 2013/2014. Kwa hiyo, hatujadharau ila kila kitu ni lazima tupange kwani hatuwezi kujenga barabara zote kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane na mimi kwamba ahadi hii ya Rais tutaitekeleza na

tumeshapangia bajeti kwenye mwaka wa fedha utakaofuata.

**SPIKA:** Mheshimiwa nani sasa hapa! Aah, ndiyo Kafulila, watu wa Kigoma ni wadogowadogo na tena wanafanana. (*Kicheko*)

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na kumshukuru Waziri na Naibu Waziri kwa kuhakikisha miradi ya barabara kule Kigoma Kusini inakwenda vizuri, napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Mwaka jana mwezi wa Tano wakati Rais akiwa na Balozi wa Abu Dhabi kwenye ziara katika Jimbo la Kigoma Kusini, yeye pamoja na Balozi walikubaliana ijengwe barabara ya kilomita 48 ambayo itaunganisha mradi wa Daraja la Malagarasi kuja mpaka Uvinza. Napenda kujua *status* ya Serikali katika kutekeleza jambo hili imefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba swali hilo liletwe upya kwa sababu ni jipya sina jibu la kutoa kwa sasa hivi.

**SPIKA:** Tena kubwa kabisa! Mheshimiwa Shekifu!

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nina swali moja la nyongeza. Tatizo la kuchelewesha mradi mpaka wananchi wanafika mahali pa kukata tamaa ni la kisera na inaonekana kwa kweli linagusa maeneo mengi. Iko barabara ya kutoka Lushoto kilomita 10 tu ilianza kujengwa kwa kiwango cha lami mwaka 2004 mpaka sasa ninavyozungumza zimejengwa kilomita

mbili tu. Serikali inatoa tamko gani maana sasa hivi zinatolewa mita 100, 200, 500, kumpata Mkandarasi ni kazi ngumu na ujenzi wa barabara hauendi na wananchi wanakata tamaa?

**SPIKA:** Yaani sera ya kuchelewesha barabara, kama ipo! Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama barabara ina mkandarasi halafu akachelewesha kazi hiyo kwa kweli inakera wananchi na hata mimi pia nisingependa kama tuna mkataba na mkandarasi halafu anachelewesha. Lakini kama tumepanga kujenga kilomita mbili (2) maana yake ndiyo uwezo uliopo kwa mwaka huo na mwaka mwingine tunaendelea na kilomita mbili (2) zingine. Kama tulivyosema kwamba, sisi tumeona ni vizuri tuanze na barabara kuu na kwa Mkoa wa Tanga kwa taarifa ya Bunge hili karibu barabara zote kuu ni za lami, isipokuwa imebakia kama kilomita moja tu kukamilisha ile barabara ya Tanga - Horohoro. Kwa kweli Serikali inajali sana Mkoa wa Tanga, barabara zote kuu ni za lami na hiyo barabara anayoizungumza Mheshimiwa Mbunge ni barabara ya Mkoa. Tukimaliza barabara kuu tutaingia kwenye kujenga barabara za Mkoa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane na *speed* hiyo ya kwenda kilomita moja kwa barabara za Mkoa ili tumalize kwanza barabara kuu.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kumekuwa na mtindo Wizara mbalimbali zinapokuwa zinatoa majibu kuhusiana na

ahadi za Mheshimiwa Rais kila mmoja amekuwa akisema ahadi za Rais tumejipanga vizuri. Sasa kwa kuwa kujipanga vizuri kunaendana na kuwa na mpango mahsus ambao umeandikwa, ni kwa nini sasa Wizara zisiletie mpango hapa Bungeni kuhusiana na zilivyojipanga kwa kila sekta ili Wabunge tuweze kuona kweli walivyojipanga kuhusiana na utekelezaji wa ahadi za Rais nchi nzima kuliko kuwa wanatumia maneno tu kwamba kila siku tumejipanga vizuri. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa Wizara ya Ujenzi tutaleta ratiba kamili ya ahadi za Rais pamoja na llani ya Uchaguzi kuhusiana na barabara tukieleza kwamba tutazitekeleza vipi. Kwa hiyo, tutaleta ratiba hiyo.

**SPIKA:** Tunaendelea, hili swali Na. 313 tumelileta kwa makosa kwani lilishajibiwa. Kwa hiyo, tunaenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa!

Na. 314

### **Wataalamu wa Ushauri Nasaha**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA** aliuliza:-

Moja ya changamoto mbalimbali za maisha ni pamoja na kupanda kwa gharama za maisha jambo ambalo limesababisha kutokea kwa migandamizo (*stress*) mingi kwa watu na hivyo kuwepo na haja ya

kuwa na watoa ushauri nasaha (waliosomea *counseling*):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwa na wataalam wengi wa fani hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mch. Peter S. Msigwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo changamoto mbalimbali za maisha zinazowakabili watu na kuwasababishia mkandamizo (*stress*). Aidha, Serikali inatambua umuhimu wa huduma ya ushauri nasaha katika kusaidia kuondokana na mgandamizo (*stress*). Kwa kuzingatia umuhimu wa huduma hiyo, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, itaendelea kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii kadri bajeti itakavyoruhusu ili kuwa na wataalamu wa kutosha katika eneo hili la huduma ya ushauri nasaha. Vilevile Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imefanya ugatuaji wa huduma za Ustawi wa Jamii kwenda katika Halmashauri ili kuwezesha huduma za Ustawi wa Jamii, ikiwemo ushauri nasaha kwa ajili ya kuwafikia wananchi walio wengi. Kupitia ugatuaji huo, jumla ya Maafisa Ustawi wa Jamii 218 wakiwemo wanawake 137 na wanaume 81 wameshaajiriwa katika Halmashauri 133.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Taasisi ya Ustawi wa Jamii inaendelea kutoa mafunzo ya fani ya Ustawi wa Jamii katika ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada kwa lengo la kupata Maafisa Ustawi wa Jamii wenye utaalam wa kutoa ushauri nasaha ili kuwa na wataalam wengi wa fani hiyo. Aidha, Wizara imeandaa mpango wa mafunzo ya Wasaidizi wa Ustawi wa Jamii (*Social Welfare Assistants*) ambao watatoa huduma za Ustawi wa Jamii ikiwemo huduma ya ushauri nasaha katika ngazi za Kata na Vijiji. Aidha, mafunzo haya yanatarajiwa kuanza mwezi Juni, mwaka huu wa 2012 katika Chuo cha Ustawi wa Jamii kilichoko Kisangara, Mkoani Kilimanjaro.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini elimu inapaswa iwe *dynamic* siyo *static* na lengo la elimu ni kutatua changamoto tulizo nazo *current*. Tafiti zinaonesha zaidi ya asilimia 50 ya elimu inayotolewa katika Vyuo Vikuu vyetu ni *irrelevant* kwenye jamii. Sasa maswali:-

(a) Pamoja na wataalam ambao amesema ambao inaonesha ujuzi wao ni mdogo, hauendani na changamoto ambazo Watanzania wanazo, ni mkakati gani wa makusudi ambao Serikali inao kwa kushirikiana hata na Wizara ya Elimu kuleta mabadiliko makubwa ambayo yataendana na changamoto ambazo wananchi wanazipata?

(b) Kwa kuwa Chuo Kikuu cha Tumaini, Iringa Mjini ni chuo cha kwanza ambacho kinatoa Shahada ya *Counseling* na kwa kuwa mafunzo wanayoyatoa

pale yako *current* na yanaendana na wakati wa sasa, je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuwatumia wale wanafunzi waliomaliza ile Shahada ya *Counseling* ili waweze kutoa msaada katika Taifa letu la Tanzania?

### **NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Mheshimiwa Spika, sina hakika kama kweli vyuo vikuu vyetu vinatoa mafunzo na taaluma ambazo ni *irrelevant*. Naamini tunatoa wataalam kwa malengo ya kutekeleza kazi maalum kutegemeana na fani husika na ukweli tunaona tumekuwa na Walimu, Madaktari, Wahandisi na kadhalika. Kwa hiyo, ni mafunzo ambayo yanaenda kwa kutekeleza malengo fulani ya kukabiliana na changamoto za maisha yetu kwa ujumla wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nafahamu Chuo Kikuu cha Tumaini kinatoa mafunzo ya *counseling* na ni muhimu pia katika kuwatumia hao *counselors* kwa kusudio la kutoa ushauri nasaha. Ushauri nasaha unaweza kwenda kiuchumi, kifamilia, maeneo ya kazi, magonjwa na kwa ujumla ushauri nasaha huo unaweza kuwa mpana kwa kiasi chake. Kwa sasa hivi tunawatumia Maafisa Ustawi wa Jamii katika kutoa ushauri nasaha pale inapohusu mgandamizo (*stress*).

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Napenda kujua Serikali ina mpango gani wa kupeleka watoa ushauri nasaha katika shule zetu za Msingi na Sekondari ili kusaidia wanafunzi wa kike na kiume wajitambue na kuweza kuepukana na mimba za utotoni na kujua ni jinsi gani watajikinga na mafataki?

**WAZIRI WA ELIMU:** Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba tuna tatizo hilo kubwa katika shule zetu za Msingi na Sekondari na juhudini ambazo tumeziandaa ni kuandaa Walimu ambao wanakuwa kama Washauri Nasaha lakini hili ambalo amelieleza Mheshimiwa Mbunge tutalisisitizia ili tuangalie namna ya kuandaa wataalam hao maalum kwa ajili ya kazi hiyo.

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya amekiri kwamba, wataalamu hawa wa utoaji ushauri nasaha ni wachache na sasa hivi kumekuwepo na ongezeko kubwa sana la magonjwa ya kisukari, *pressure* na kadhalika. Je, haoni sasa ni wakati mwafaka wa kuangalia angalau bajeti ya dharura kwa ajili ya ku-*train* watu hawa wasaidie kutoa ushauri nasaha katika maradhi haya? (*Makof!*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, tunafahamu changamoto zilizopo na hasa ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo kisukari, shinikizo la damu na mengineyo na umuhimu wa ushauri nasaha katika kukabiliana na kumudu changamoto hizo za magonjwa ambayo mtu anakuwa nayo. Ushauri nasaha unahitajika katika maeneo mengi tu ikiwemo hayo ya magonjwa na hata yale magonjwa ambayo yanaambukiza pia na mambo mengine hayo. Lakini uwepo wa watalaam wetu na kusema kwamba tunaweza kujitahidi kwa kiasi gani sasa kuongeza idadi yao ni kama nilivyojibu katika

swali la msingi nikielezea kwamba pamoja na uwepo wa mafunzo haya ya Stashahada na Shahada kwa taaluma hii Ustawi wa Jamii, sasa Serikali imeanza kuandaa na mafunzo haya yameanza mwaka huu ya wale *Social Welfare Assistants* yaani Wasaidizi Maafisa Ustawi wa Jamii katika Chuo hicho ambacho nimekisema kipo Kilimanjaro. Kwa hiyo, naamini mafundisho haya yanaweza yakatusaidia tukapata wengi ambao wanaweza wakafanya kazi hata katika ngazi zile za chini.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kupata nafasi. Kwa kuwa Serikali imekiri katika swalii la msingi kwamba changamoto ya kupanda kwa maisha ni sababu tosha ya kuwafanya wananchi wake kuwa na msongo wa mawazo; na kwa kuwa, njia sahihi ya kuweza kutatua tatizo hili ni kupunguza gharama za maisha kuliko kuzalisha wataalam ambao watakwenda kutatua tatizo hilo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba gharama ya maisha ya wananchi wake zinapungua au zinakuwa chini ili wananchi wake waepukane na tatizo hili la msongo wa mawazo? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli moja katika sababu za kupata mgandamizo yaani *stress* ni kupanda kwa gharama za maisha lakini kupanda kwa gharama za maisha ni moja tu katika zile sababu ambazo zinatokea na siyo lazima kwa kila mtu ambaye anakabiliana na gharama au changamoto za kupanda kwa gharama za maisha anaweza akapata *stress*. Kuna wengine ambao wanamuudu na wanaweza kukabiliana na kuishi

na mabadiliko ya kimaisha bila kupata *stress*. Lakini kuna sababu nyinginezo nyingi tu, lakini mojawapo ni vile vinasaba ambavyo vinatoka kwenye familia. Kwa hiyo, familia fulani inakuwa na uwezekano wa kupata *stress* kuliko familia nyingine. Kuna mengine ambayo mtu anaweza akapata *stress* kwa mfano, changamoto za kurudia kwa ule mkangandamizo au zile *stress*, zinaporudi mara kwa mara na mtu anashindwa kuhimili marudio ya *stress* hizo basi anaweza kushindwa na akaanza kuhitaji huo ushauri nasaha na mambo mengineyo.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali inafanya nini sasa katika angalau kupunguza hizo gharama za maisha? Nafikiri mojawapo ni katika kutuwezesha kuwa na mazingira mazuri kiuchumi ili kila mmoja wetu aweze kukabiliana na kufanya shughuli zile kimaendeleo za kwake mwenyewe kama familia, lakini vilevile Kitaifa. Pamoja na mambo mengineyo ambayo Serikali imewezesha kitu kikubwa kuliko chochote ni kuiwezesha jamii kukabiliana na matatizo yetu na changamoto za kimaisha ambazo lazima tukubaliana nazo, mojawapo ni elimu na juhudzi za Serikali ni kubwa katika kuwezesha watu wetu na wananchi wetu kupata elimu ya kutosha. (*Makof*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kila kitu kina mwanzo na mwisho. Sasa maswali yamekwisha na muda pia wa maswali matano umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, tuwatambue wageni tulionao hapa. Wapo wageni wa Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Naibu Waziri wa Uchukuzi ambao ni

wadogo zake wakiongozwa na mke wake Mrs. Furaha J. Tizeba. Mrs. Furaha Tizeba asimame kwanza, ahsante. Halafu na wadogo zake wengine wasimame. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tuna wageni waliofika kwa ajili ya Mafunzo hawa ni Waheshimiwa Madiwani 47 ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mheshimiwa William Ngeleja wanatoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Mwanza wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Mheshimiwa Mathew Lubongeja. Mheshimiwa Meya kwanza asimame Lubongeja tumwone na Waheshimiwa Madiwani wengine wote wasimame. Ahsante sana Waheshimiwa. Naamini mnafanya kazi yenu kadri inavyopaswa, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi wengine 50 pamoja na Walimu wao kutoka shule ya msingi El-Shaddai Dodoma, wasimame hao wanafunzi 50, ahsante sana, karibuni sana tumefurahia kuwaona. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi 60 pamoja na Walimu wao kutoka shule ya msingi Msalato. Tunaomba wasimame wanafunzi wa Msalato na walimu. Ahsanteni sana, tumefurahi kuwaona. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi 50 pamoja na Walimu wao kutoka shule ya Sekondari ya Jamhuri Dodoma. Wako wapi wanafunzi wa shule ya Sekondari ya Jamhuri, ahsante sana. Msome kwa bidii. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi 31 na Walimu wao kutoka shule ya Al-qaem Seminary Dodoma, wasimame hawa wanafunzi wa Seminary. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Tuna Waheshimiwa Madiwani watatu ambao ni wageni wa Mheshimiwa John Paul Lwanji wa Manyoni Magharibi wakiongozwa na Mheshimiwa Saidi Mtandu. Waheshimiwa Madiwani hao wasimame popote walipo. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Tuna wajasiriamali watatu kutoka Kata ya Endasack, Wilaya ya Hanang ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu wakiongozwa na ndugu Leonard Lono. Wajasiriamali wasimame popote walipo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mussa Zungu, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi namba 231, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala.

Halafu kuna tangazo lingine kutoka kwa Mwenyekiti wa Tanzania *Women Parliamentary Group (TWPG)*, Mheshimiwa Anna Abdallah, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa TWPG kuwa leo kutakuwa na kikao saa 7.15 katika chumba namba 208 ghorofa ya pili.

Halafu nina tangazo lingine kutoka Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, ye ye ndiye Katibu wa Waheshimiwa

Wabunge wa Kanda ya Ziwa anasema kutakuwa na kikao kifupi cha Waheshimiwa Wabunge wote wa Kanda ya Ziwa, Mkoa wa Kagera, Geita, Mwanza, Mara, Simiyu, Shinyanga na Tabora saa 7.15 katika ukumbi wa Msekwa C na wenyewe wanajifahamu, mnakaribishwa kwenye kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, jana nilitangaza kwamba fomu za kugombea nafasi ya UWT zilianza kuchukuliwa jana mpaka tarehe 6 Agosti, 2012. Hili tangazo amelileta Mheshimiwa Mary Chatanda kwa hiyo, atawafahamisha mahali pa kwenda kuchukua fomu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba masikio yenu kuna suala ambalo nataka kulizungumzia sasa.

Waheshimiwa Wabunge, mnamo tarehe 28 Julai, 2012, wakati wa Mjadala wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa alitoa hoja kwa mujibu wa Kanuni 53(2), 55(3)(f) na Kanuni ya 5(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007 kwamba michango mingi iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia hotuba hiyo imetuhumu baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kuwa wanajihuisha na vitendo vya rushwa kwa namna moja au nydingine wakiwemo Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Spika alitoa Mwongozo kwamba kwa mujibu wa Kanuni 53 atazipeleka tuhuma hizo kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili zifanyiwe uchunguzi na imshauri Spika ipasavyo.

Waheshimiwa Wabunge, tumeandaa Hadidu za Rejea kwa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu suala hili kama ifuatazo:-

Kuchunguza na kumshauri Spika iwapo tuhuma kwa baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kujihusisha na vitendo vyatia rushwa ni za kweli au hapana. Wajumbe wa Kamati baada ya mashauriano kati ya Spika na Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kuzingatia *nature* ya suala lenyewe imeonekana kwamba suala hili linaweza kushughulikiwa vizuri zaidi kwa mujibu wa Kanuni 114(18) kwa kuunda Kamati Ndogo ya Wabunge watano itakayoongozwa na Mheshimiwa *Brig. Gen.* Hassan Ngwiliza, (Mb) ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, kwa lengo la kuwezesha suala lenyewe kufanyiwa kazi kwa haraka na kutolewa uamuzi. Aidha, Kamati hiyo Ndogo italifanyia kazi suala hilo kwa muda wa wiki mbili na baada ya kukamilisha kazi yake itawasilisha taarifa yake kwa Spika kama Bunge liliivoamua.

Wajumbe hao wa Kamati hiyo Ndogo ni Mheshimiwa *Brig. Gen.* Hassan Ngwiliza, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, namna Kamati Ndogo itakavyofanya kazi. Ili suala hili liweze kushughulikiwa kwa haraka na kwa ufanisi, Kamati Ndogo inatakiwa ifanye yafuatayo:-

(a) Kwanza, kukutana na kukubaliana namna bora za kulishughulikia suala hili pamoja na mapendekezo yaliyotolewa. Aidha, kwa kuzingatia misingi ya haki asili (*natural justices*) katika orodha hii hakuna wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini.

(b) Kupitia Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard* za tarehe 27 na 28 Julai, 2012 ambapo Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2012/2013 iliwasilishwa ili kupata picha ya namna ambavyo mjadala mzima ulivyoendeshwa.

(c) Kuwaita na kuwahoji mashahidi ambao watasaidia Kamati kujua ukweli kuhusu tuhuma hizo na wafuatao wanaweza kuitwa ili kuhojiwa. Moja, Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambaye katika Mkutano wake na Waandishi wa Habari ambapo alifanya *press conference* alitaja majina ya Wabunge kadhaa wenyе mgongano wa maslahi. Pili, Waziri wa Nishati na Madini aliainisha tuhuma za kuwepo kwa vitendo vya rushwa kwa baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini wakati wa majumuisho ya hotuba yake. Tatu, Wabunge wote waliochangia hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini na kutoa tuhuma dhidi ya Wabunge wengine kujihusisha na vitendo vya rushwa katika Wizara ya Nishati na Madini. Nne, Mbunge mwengine yeoyote ambaye anaweza kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa suala hili, namna ya kufanya.

(d) Kuwasilisha taarifa kwa Spika kwa ajili ya ushauri na mapendekezo ya hatua zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati Ndogo hii itashughulikia suala hili katika muda wa siku 14.

Mwisho ni kwamba, kwa kuwa suala hili ni nyeti na linahusu mustakabali wa Taifa katika suala nzima la kupambana na vitendo vyote vya rushwa, ni muhimu sana Kamati kwa kadri inavyowezekana ijitahidi kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni za Bunge na weledi wa hali halisi juu ya suala hili.

Waheshimiwa Wabunge, ninaamini kabisa wale wote waliokuwa wanasema wana ushahidi ama walimtaka Spika ataje majina, sasa wakataje kule yale majina. Wakataje huko na watakaokuwa wanaitwa nao watoe ushirikiano na Kamati inaruhusiwa kutumia watu wengine inaowafahamu ili waweze kuwasaidia.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, nafikiri kuna tangazo lingine walichelewa kulileta. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Philipa Mturano, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 mchana watakuwa na kikao chao chumba namba 227, wajumbe wote wanatakiwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tatizo, nina kazi za kufanya pale ofisini. Kwa hiyo, nitamwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama aje anisaidie kwenye Kiti hiki. (*Makofi*)

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia  
Kiti*

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MBUNGE**      **FULANI:**      Mheshimiwa      Mwenyekiti,  
Mwongozo!

**MWENYEKITI:**      Waheshimiwa      Wabunge,  
tunaendelea, Katibu!

**MBUNGE**      **FULANI:**      Mheshimiwa      Mwenyekiti,  
Mwongozo!

## **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka  
2012/2013  
Wizara ya Uchukuzi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaona nitawapa nafasi, hebu ngoja tuanze kazi kwanza. Majadiliano yanaendelea na mchangiaji wangu wa kwanza aliyepo hapa mezani ni Mheshimiwa Augustino Masele.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukupongeza wewe kwa kunipatia nafasi hii ili niweze na mimi kutoa

mchango wangu katika bajeti hii ya Waziri wa Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya uchukuzi na usafirishaji katika Taifa letu, ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na katika mustakabali wa kisiasa katika nchi yetu na vilevile katika suala zima la usalama. Kuyumba kwa sekta ya usafirishaji na uchukuzi katika nchi yetu kumepelekea kwa namna moja ama nyingine kuyumba kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari yetu ya Dar es Salaam imekuwa ikipanuliwa kwa kasi kubwa lakini kwa bahati mbaya sana upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam umekuwa hauendi sambamba na kuimariswa kwa miundombinu ya reli inayokwenda katika Mikoa ya Kigoma pamoja na Mikoa mengine ya Kanda ya Ziwa. Matokeo yake tumeyaona ya kwamba sasa usafirishaji na uchukuzi unafanywa zaidi kwa kutumia barabara zetu ambazo zinajengwa kwa gharama kubwa, barabara za lami. Barabara hizi licha ya kuchukua fedha nyingi za Taifa hili, zimekuwa hazidumu kwa sababu mizigo mingi inayozalishwa katika bandari ya Dar es Salaam imekuwa ikipitishwa katika barabara zetu hizi ambazo zimejengwa kwa gharama kubwa na matokeo yake barabara hizi zinaharibika na matokeo yake bajeti nyingine ya kila mwaka inaundwa tena ya kuzitengeneza hizi upya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii isiporekebishwa kwa kuimarisha reli zetu nchini, utakuwa ni mchezo wa kuigiza bandua bandika. Unabandika lami kwa bei

kubwa unabandua tena na kuifanya upya, lakini wakati huohuo sekta zingine nazo zinahitaji fedha. Sasa kama tutakuwa hatuna msimamo mzuri wa kuzitengeneza hizi reli zetu na kuzifanya kuwa za kisasa, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu na matokeo yake itakuwa ni kila siku tunalalamika kwamba hali ya uchumi ni mbaya, hali ya maisha nchini Tanzania inazidi kushuka na wananchi wetu hawataisamehe Serikali yetu kwa sababu hiyo, kwa sababu vitu vya msingi ambavyo ni vya muhimu katika maisha ya kila siku vinawafikia vikiwa viko katika bei ya juu kwa sababu vinasafirishwa kwa magari ambayo yanatumia mafuta ambayo mafuta yenyewe katika soko la dunia yako bei juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri sana Wizara yetu ya Uchukuzi ambayo inaongozwa na Dkt. Harrison Mwakyembe akisaidiwa na Dkt. Charles Tizeba waliangalie suala hili kwa umakini mkubwa na waige mtindo uleule aliokuwa anafanya kazi katika Wizara ya Ujenzi ambako kuna mkakati wa kuziunganisha barabara za lami kwa Mikoa yote ya Tanzania. Sasa mkakati huohuo uwepo wa kuhakikisha kwamba reli zinafika katika kila Mkoa katika Taifa hili la Tanzania. Hapo peke yake ndipo tutakapokuwa tumefikia hatua ambayo itakuwa ni ukombozi kwa Taifa hili la Tanzania vinginevyo tutakuwa tunajidanganya kusema kwamba tunaunganisha Tanzania hii kwa barabara zote za lami lakini wakati huohuo tunaua Shirika letu la Reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa reli ni mwanzo wa meli, pale reli inapoishia inatakiwa iunganishiwe meli. Mtindo ni huohuo kwa maana ya

kwamba meli zinasafiri katika bahari kuu zinafika bandarini, zikifika bandarini kwa sababu zina mzigo mkubwa zinahitaji *counterpart* mwingine ambaye naye ana ubavu uleule wa kusafirisha mzigo mkubwa ambao si mwingine isipokuwa ni treni ambazo zinasafiri katika reli. Tuko katika wakati mgumu kama Taifa na makosa tulyafanya yapata miaka 15 iliyopita kama alivyosema Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwamba ndani ya kipindi cha miaka 15 Shirika la Reli limepita katika msukosuko mkubwa na matokeo yake sasa tunaona kwamba nchi yetu imefika hapa tulipofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 12 kuna kibwagizo hapa amezungumza kinachosema ya kwamba "TRL na Kampuni Miliki ya Rasilimali za Reli Nchini (*RAHCO*) zimefanya kazi kubwa katika kipindi kifupi cha miezi 12 tu kurejesha uhai katika usafiri na uchukuzi wa reli. Nguvu kubwa tulionayo ni rasilimali watu. Tuna wafanyakazi wazalendo TRL na *RAHCO* wenye ari ya kufanya kazi na ujuzi mkubwa unaorutubishwa na uzoefu wa muda mrefu wa kufufua chochote kile kinachotambaa kwenye reli".

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya ni maneno mazito lakini kwa kipindi chote hiki cha miaka 15 wamekuwepo watu hawa na waliifanya Serikali ifikie mahali ifikirie namna ya kubinafsisha Shirika hili kwa sababu ya utendaji waliokuwa nao pamoja na uzalendo waliokuwa nao lakini Shirika hili likaonekana halina tija likafikia hatua ya kubinafishwa. Kwa maana hiyo sasa Mheshimiwa Waziri maadam unao hawa wafanyakazi basi ni muhimu wakapewa mwongozo wa kujifunza hata kutoka katika Mashirika mengine

ambayo yameonesha wazi kwamba yanaweza yakafanya kazi vizuri. NSSF ni mfano mzuri tu, ni Watanzania hawahawa ambao wanafanya kazi wakiwa katika mazingira hayahaya ya Tanzania hiihii, wanafanya maajabu, wanawekeza katika kila sekta. Watu wa Shirika la Reli basi wajifunze kutoka kwa wenzao wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii wanafanya kazi kubwa na nawapongeza hawa na niombe kwamba kujifunza kutoka kwa wenzetu wanaofanya vizuri uwe ndio utamaduni ambao ndio unaoweza ukalifanya Taifa letu liwe ni Taifa la watu wanaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli zetu ni za muda mrefu tunatakiwa tubadilike sasa kwa sababu hata teknolojia ya utengenezaji wa magari, gari liliokuwa linatengenezwa miaka ya 1960 leo hii ukipanda watu wanakushangaa kwa sababu wataona kwamba unafanya kituko ambacho pengine unataka kuburudisha watu na kwa maana hiyo reli zetu na lenyewe zinatakiwa zibadilishwe tuingie kwenye *standard gauge* kama mataifa mengine yanavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye Shirika la Ndege. Shirika la Ndege kama liliyo Shirika la Reli na lenyewe liko katika hali ngumu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba kasi aliyanza nayo ya kuyafufua mashirika haya asirudi nyuma.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya pili imelia, basi naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Masele. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mheshimiwa Sabreena Sungura atafuatiwa na Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami bila ya kupoteza muda, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waislam wote wanaofunga katika Mwezi huu Mtukufu na kumwomba Mwenyezi Mungu *Subhana Wataallah* aweze kuwatakabaria swaumu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuzipa pole familia zote za marehemu katika ajali ya M.V. Skagit na Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, napenda kuipa pole familia ya aliyejikuwa mfanyakazi wa Bunge, Mwenyezi Mungu awape subira na ampunzishe marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda moja kwa moja kwenye bajeti, tukiangalia bajeti ya mwaka huu ni bajeti ambayo ni kiini macho na ni bajeti ambayo inaendelea kuwalaghai Watanzania, kwa nini nasema hivi? Ukiangalia kiwango cha fedha ambacho kiliwekwa mwaka jana na fedha iliyotolewa ni chache sana. Mwaka jana bajeti ilikuwa ni shilingi bilioni 332 lakini fedha iliyotolewa ni shilingi bilioni 122 sawa na

asilimia 37 tu. Bajeti hii imeendelea kuwa tegemezi kwa wafadhili. Mwaka jana tunaona ni asilimia tano (5%) tu iliyotoka kwa wafadhili, lakini mwaka huu tena tumetenga takribani bilioni 60 na kidogo kutoka nje. Sasa Mheshimiwa Waziri atuambie ana uhakika gani kwamba watu hawa wataendelea kutupa fedha hizi na tukiangalia bajeti ya mwaka jana na mwaka huu imezidi kuwa pungufu, bajeti ya mwaka huu imekaa kulipa madeni zaidi kuliko kutekeleza matakwa ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nihamie suala la ndege. Katika suala la ndege kumekuwa na matatizo. Zimetokea ajali mbalimbali Mkoani Kigoma, Mkoa ambao mimi natoka na nawawakilisha wananchi. Tatizo kubwa ambalo linasababisha ajali hizi za ndege Mkoani Kigoma ni upanuzi wa uwanja. Tumeiambia Serikali iwalipe fidia wakazi wa Kigoma maeneo ya karibu na *Airport* ili waweze kuvunja nyumba zao na kutoa ile miti mirefu (migazi) ili angalau pale wanapotaka ku-*approach landing* basi waweze kushindana na vile vikwazo ambavyo ni nyumba za watu na mimea, lakini sasa hivi sioni dalili ya Serikali kuweza kulipa fidia, hali hii ndio inapelekea matatizo ya ndege kudondoka pale Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ni ile ndege inapodondoka pale, kule ilipodondokea, Ofisi ya Uchukuzi ilitoa fedha kwa ajili ya uangalizi wa eneo lile. Lakini ilipokokotwa kule sasa hivi imeshakuwa *scraper haifanyi* kazi kwa sababu mabawa yalikatika mkono wa kulia, miguu yote imekwisha, matairi yamevunjika, imevutwa mpaka pale *Airport*. Lakini

pale nani anaangalia ulinzi wa ile ndege au ndiyo basi Shamba la Bibi tukaanza kuchukua kifaa kimoja baada ya kingine maana vimeanza kuibiwa. Kwa hiyo ni vizuri sasa Mheshimiwa Waziri akaweza kuwasiliana na kule na kuhakikisha kwamba kunakuwa na ulinzi wa uhakika na wapeleke malipo kwa ajili ya walinzi hao ili iweze kuangaliwa kwa sababu ndege hii ilinunuliwa kwa fedha za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo lingine lipo kwenye *running way*. Ndege ile ilikuwa inatumia takribani mita 1,800, lakini sasa hivi kwa ajili ya ukarabati zimebakia mita 1,300 tu. Kwa hiyo, Rubani anajikuta wakati anaendelea na ndege kwenye eneo la lami akitahamaki lami imeisha anaanza kupita kwenye vumbi na haoni chochote. Ukiangalia juzijuzi hapa wenzenetu wa *Precision Air* matairi yao yalipasuka kwa ajili hiyo. Sasa ni wazi Mheshimiwa Waziri inampasa kuhakikisha zoezi hili la ulipwaji wa fidia kwa wananchi linafanyika ili eneo lile liweze kupanuliwa na kwa hali ya sasa hivi jinsi ilivyo ni kuomba tu Wizara ndege zinazoenda kutua Kigoma basi wapelekwe marubani ambao ni wazoefu wasithhubutu kupeleka ma-*interns* wataua watu wa Kigoma na Watanzania wengine kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nielekee kwenye sekta ya bandari. Sekta ya bandari nayo ina urasimu. Huyo *Private Operator* wa Kigoma mpaka sasa hivi anadaiwa dola takriban 700,000 hajalipa. Ukienda bandari ya Kasanga ana deni toka mwaka 2008 mpaka leo hii hajalipa na bado anazidi kuongezewa mikataba kila mwaka. Mheshimiwa Waziri

hana kuna rushwa ya ujisadi na ningeomba tu Wizara iweze kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha kwamba kwa nini hawa watu wanaiibia Serikali mpaka dakika hii. Kwa nini hawalipi madeni yao na wakati sekta hii ni sekta muhimu ambayo inachangia kwenye pato la Taifa? Wao ni akina nani mpaka wasilipe madeni haya kwa muda wote huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna tatizo bandarini, tatizo la wizi, tukiangalia mwaka jana pekee zimeibiwa takriban *container* nne za shaba, hii nchi mnatupeleka wapi? Hivi *container* ya shaba bandarini inaibiwaje? Tukiangalia wenzetu wa Hongkong ndani ya miaka 20 wamewahi kuibiwa *Mercedes Benz* na ndani ya masaa machache ikapatikana, lakini bandari yetu ya Dar es Salaam zinaibiwa *container* nne ndani ya mwaka mmoja, hapa kuna *poor security system*. Kwa hiyo, napenda kumwomba Waziri afanye afanyalo ahakikishe kwamba anadhibiti wizi wa bandarini. Wizi wa bandarini imekuwa ni kero na wanaoiba sio kwamba ni vibaka kutoka mtaani ni wataalamu, wafanyakazi wa bandari, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hakikisha kwamba masuala haya unayashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kugusia suala zima la ajali. Wenzetu wa *SUMATRA* walikuwa wakishirikiana na wenzetu wa *Zanzibar Maritime Authority*, lakini baadaye inasemekana wenzetu wa Zanzibar wakajitenga lakini ajali hizi zinapotokea jamani watu wanaokufa ni wote, Watanzania Bara na wa Tanzania Zanzibar. Mimi nimefika eneo la tukio, nimewakuta wapiga kura Mheshimiwa Chenge kule

wengine wame-save, nimewakuta watu kutoka Arusha, Kigoma hali ni mbaya meli ile inabeba watu wa *design* zote, lakini kwa nini vitu chakavu vinaendelea kufanya kazi katika nchi hii? Mwaka jana hapa imepitishwa Sheria, Upinzani wote tulipinga, Sheria ya Ununuzi wa Vitu Chakavu ni mbaya, watu watachakachua, lakini wenzetu wa Chama Tawala mkapinga, kutahamaki meli zimekuwa zinadondosha watu, ndege nazo vioo vinapasuka hii ni kwa sababu ya Sheria mbaya ya Vitu Chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mnaweza mkamuona mbaya ni *Pression Air* kwamba anaihujumu *Air Tanzania* lakini sheria zenu je zikoje? Sasa ni lazima Serikali muiangalie, Sheria ya Vitu Chakavu ni sheria mbaya, hii nchi ni tajiri ina uwezo mkubwa sana wa kununua vitu vipyta. Tuna uwezo wa kununua ndege mpya, tuna uwezo wa kununua meli mpya lakini Watanzania kila siku wanaendelea kufa. Hivi wenzetu wa Ethiopia wana uchumi gani mpaka kila siku wanunuua ndege, wenzetu wa *Kenya Airway* wana uchumi gani kila siku wanunuua ndege, tunashindwa mpaka na nchi ndogo Rwanda ambayo imepigana vita miaka na miaka. Hii ni aibu kwa Taifa la miaka 50 na kama Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa ni bora mjaribu kuwapa vyama vingine viingie tuone na wenyewe watafanyaje lakini hatuwezi kuendelea kufa na kupata ajali kila siku. Sisi ndio wahanga wa kwanza wa ajali ya ndege, Mheshimiwa Buyogera alikuwepo ni Mheshimiwa lakini hata Mawaziri wangeweza kuwepo. Sasa hii hali ni mbaya jamani hivi ndugu zetu wa huko Serikalini hamuoni aibu kutokana na hali hii? Ni lazima tubadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende moja kwa moja kwenye sekta ya reli. Sekta ya reli imekuwa ni sekta muhimu sana katika uchumi wa Tanzania lakini reli hizi toka enzi ya mkoloni aliiacha mpaka leo hii hali inazidi kuwa mbaya zaidi, yaani tulikotoka kuna afadhali kuliko tunakokwenda. Ukiangalia reli kuanzia Kigoma kuja Dar es Salaam hapa katikati kuna Stesheni kubwa nyingi, kuna Salanda, Itigi, Manyoni, Kazuamimba, Kalenge, Kandaga, Kaliua, Urambo Stesheni zote hizo walikuwa wanajaa vijana wa Kitanzania. Vijana hawa walikuwa wanafanya kazi nyingi, wanapata uchumi na pato la Taifa likawa linapatikana lakini sasa hivi tangu treni imeanza kusuasua vijana wote wale wanahamia mjini kufanya biashara haramu. Nchi inakwenda wapi, ni lazima tuwekeze kwenye miundombinu ya reli tuhakikishe vijana wetu wanabaki huko na wanafanya kazi kwa ajili ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009/2010 mwanzoni kulikuwa kuna ukarabati wa reli ya Kilosa - Gulwe. Ukarabati ule *RAHCO* ilichukua Kampuni zenye *bulldozer* kwa ajili ya kukarabati eneo lile. Lakini cha kushangaza walichukua Kampuni hizi kwa bei za dharura lakini kuna dharura ya miaka mitatu na kodi inayotumika hapo ni kodi ya Watanzania. Hivi kweli mnatumia kodi ya Watanzania ambao hawana dawa, ambao Walimu wanagoma, ambao wanafunzi hawakai kwenye madawati mazuri, kulipa watu kwa dharura ndani ya miaka mitatu, hii hali ni tete na tunaomba Waziri achunguze na zoezi hili lisitishwe, zilipwe *rate* za kawaida kwa sababu hamna dharura

ya miaka mitatu. Sasa hivi njia imekaa vizuri, treni inapita na ukarabati unaendelea. Mheshimiwa Waziri suala hili lifanyie kazi kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna suala la *Dry Port*. Tumeona hapa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba kuna *equipment machine* tano zimetolewa na Serikali ya Ubelgiji kwa ajili ya Mkoa wa Dar es Salaam, Mwanza na Shinyanga. Lakini mpaka leo hii *Dry Port* ya Shinyanga iko tayari kwa nini hizi *equipment machine* hazijapelekwa Shinyanga au ndio zipo katika dhana ya kusubiri uchakachuaji? Hii ni changamoto Mheshimiwa Waziri naomba watu wa Shinyanga wapelekewe *equipment machine* kwa ajili ya kupanga na kushusha makontena kabla muda wa kuchakachuliwa haujafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwe tunajali muda ukifikia kengele ya pili basi iwe ni utii bila shuruti. (*Makof*)

Naomba nimwite mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed atafuatiwa na Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuchangia, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote, aliyenijalia kuwa mzima na nikaweza kufika katika mjengo huu bila ya kushikwa mkono na nikaweza kuchangia katika hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda nimpe pongezi aliyekuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar Mheshimiwa Hamad Masoud kwa maamuzi yake aliyoyafanya ya kujiuzulu baada ya kuzama kwa M.V. Skagit. Maamuzi aliyoyafanya huyu ni ya kijasiri ambayo si wengi wa viongozi wetu katika Bara letu la Afrika wanaweza kutoa maamuzi ya kijasiri kama hayo. Kwa hiyo, nawaambia watu wa Ole, huyu amejenga heshima ya kisiasa na pia ni chuma cha pua, kwa hiyo waendelee kumchagua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nichangie kwanza kuhusu *SUMATRA*. *SUMATRA* ina majukumu ya kusimamia na kudhibiti usafiri wa majini na nchi kavu. Juu ya kuwa mamlaka hii ina jukumu hili, lakini bado usafiri wa baharini unatisha, hauaminiki na kwa kweli ukiukumbuka unaliza. Nasema haya kwa mfano kwanza hapa Tanzania palitokea meli ya M.V. Bukoba kuzama, meli hii illua mamia ya Watanzania na ikaahidiwa kuwa itapatikana meli nyingine kule Bukoba lakini mpaka leo haipo. Kilizama chombo kutoka Tanga kwenda Pemba kikiitwa Limoyoni. Chombo hiki kiliua Watanzania wote waliokuwemo katika chombo kile. Kilizama chombo kutoka Unguja kwenda Pemba, kiliitwa MV Kabuli. Hii ilikuwa kaburi kweli kwa sababu hakuna kilichopatikana. Kuna chombo kilizama kutoka Tanga

kwenda Pemba kililipuka na kikaua watu wote. Meli ya MV Spice Islanders ilizama tarehe 11 Septemba 2011, ikaua mamia ya Watanzania. Mwezi wa saba 2012 imezama MV Skagit imeua mamia ya Watanzania. Jamani hali hii inatisha, inaliza na Serikali ilikuwa ikae iangalie nini tufanye ili kuokoa maisha ya Watanzania. Inapotokea majanga haya Serikali huunda Tume lengo ni kujua chanzo cha yaliyotokea ili kujikinga yasitokee mengine. Lakini matokeo yake Tume hii inakula pesa, hakuna kinachopatikana na watu wanaendelea kuzama na kufa. Jamani tuone hili ni janga la kitaifa. Yote haya yanasaababishwa na vyombo vibovu. Vyombo vya Serikali vilivyopo ni vibovu, vimechoka na kuchakaa, vyombo vya wafanyabiashara vingi vyao ni vibovu lakini Serikali haioni hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki cha MV Skagit kiliponunuliwa kutoka huko kilikuwa kimechoka na kuchakaa. Chombo hiki inasemekana muundo wake si ule uliokuja hapa. Chombo kile sijui kilipelekwa kwa fundi vibatari au kwa nani kikaongezewa ghorofa nyingine juu. Nahodha wa chombo hiki alisema kwamba chombo kilipigwa na dhoruba moja na kikazama kama kilichopigwa mtama. Hii ni dhahiri kama chombo hiki hakikuwa na *balance* kwa sababu ya ongezeko ya ghorofa ilioongezeka juu. Chombo kimeza, kimeua watu, Serikali inajiandaa na mchakato wa kuunda Tume nyingine eti ya kuangalia ajali hii ilitokeaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani tunamalizika hili ni janga la kitaifa Serikali iamue kuunda na chombo kimoja tu ambacho kitasajili vyombo hivi kwa pande

zote mbili za Muungano. Isiwe watu wanakwenda huko madubwana yaliyochakaa wakatuletea hapa halafu yakaaza kuua watu na tukaambiwa eti kuna mamlaka inayodhibiti na kusimamia. Mamlaka gani hii, mbona inatumaliza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo hivi nya baharini vyote ni vibovu. Hata hivi nya *Azam Marine* tunavyovitegemea, kuna vingine ni vibovu. Kwa ushahidi mimi nimeshaingia *Sea Bus III*, mara tatu ilizima ikiwa baharini. Meli ilipofika Dar es Salaam hawakusema wafanyakazi kama chombo kina matatizo na wakapakia abiria wengine wakawapeleka Unguja na kikaenda kikazima muda wa masaa mawili. Tunaiomba Mamlaka hii ifanye kazi yake iliyokusudiwa sio wakae tu huko ofisini wakituambia vyombo wanavikagua si kweli, haiwezekani hata siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata vyombo nya nchi kavu vinasababisha ajali kwa wingi. Tuangalie jinsi mabasi yanavyoanguka na kuua abiria kila siku. Mamia ya Watanzania wanateketea. Barabara ziongezwe upana wake. Barabara ni nyembamba wakati wa kupishana na maroli gari nyingine zinaanguka. Hebu jamani tuangalie ni kitu gani hasa sisi kilichotupata hata ikawa usafiri wote una matatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hizi ndege tulizonazo pia zina matatizo. Baadhi ya ndege hizi za abiria ni mbovu. Mimi nimeshawahi kupanda ndege moja sitaki niitaje inavuja ikinyeshewa na mvua. Jamani hii ni aibu kwa taifa hili. Hizi ndege zimechakaa, hata huko zilikotengenezwa inaonekana hazitumiki tena, sisi

hana bado tunazitumia. Jamani tusicheze na maisha ya Watanzania. Sisi tuna jukumu kubwa na tutakwenda kujibu mbele ya Mungu. Tukiwa na majukumu haya tuangalie nini tunachokifanya, tuvisimamie hivi vyombo vifanye kazi yake sawasawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nizungumzie kuhusu *TAZARA*. Kwa kweli *TAZARA* ni mhimili mkubwa unaoleta maendeleo katika nchi yetu lakini inavyoonekana hii *TAZARA* iko karibu na kukata roho. Yote haya yamesababishwa na Sheria Na.4 ya mwaka 1975 iliyofanya Makao Makuu yawepo Tanzania na Mkurugenzi Mkuu atoke Zambia. Huyu Mkurugenzi Mkuu ndiyo chanzo cha matatizo yote haya ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na-*declare interest* ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu. Walikuja kwenye Kamati yetu wanalia, inafika miezi mitatu mtu hajapata mshahara, aishi vipi nchi hii na mfumko wa bei tulionao? Si kuwafanya hawa wakipata mwanya na wao waibe? Kuna wastaa fu wa *TAZARA* ambao wanadai shilingi bilioni 22.96/. Nmeangalia katika bajeti hii hakuna hata kasma ndogo waliowekewa kulipwa mafao yao, wataishi vipi watu hawa? Hebu jamani tuwaonee huruma hawa Watanzania wenzetu. Hawa ni watu wazima, wamepoteza muda wao kwa kuitumikia nchi hii, leo wastaa fu hawa ni miaka mingapi hawajalipwa chochote? Hivi kweli sisi hatuna huruma na hawa wananchi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali yetu ifanye mazungumzo na Serikali ya Zambia, hii ya

kila siku Mkurugenzi Mkuu anatoka Zambia ni kama *dictator*. Mkurugenzi huyu anatoa maamuzi peke yake, haweki vikao, hawashauri wenzake, yeye ndiye anaamua kila kitu. Hapo zamani ilikuwa ikikidhi haja kwa sababu watu walikuwa wanaaminika lakini leo mambo yanabadilika na watu pia wanabadilika. Naomba tuishauri Serikali ya Zambia ili mfumo huu uondoke na iwe kwa *rotation*. Awamu hii Mkurugenzi Mkuu kutoka Tanzania na baada ya miaka fulani anawekwa Mkurugenzi Mkuu kutoka Zambia. Kwa kufanya hivi ndiyo tutaweza kweli kuiendesha hii reli ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha, reli hii inafanya kazi kama ya kichaa. Reli ina mabehewa mapya yamekwenda kukodishwa mbali, reli hii inakodiwa mabehewa mengine. Hii ni ajabu na sijui hii reli na hawa wafanyakazi vipi. Huyu Mkurugenzi Mkuu Msaidizi yupo lakini ni *figure* tu hana maamuzi yoyote, yeye yupo tu anaangalia jinsi reli inavyozidi kukandamizwa na Watanzania wanavyozidi kukandamizwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema, mwenye kurehemu katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan, kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge

Iako Tukufu kutoa mchango wangu na naomba Serikali izingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia na mimi kama wenzangu walio tangulia kuchangia, napenda kuchukua nafasi hii niwapongeze Mawaziri walioteuliwa kushika Wizara hii Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe na Dkt. Tizeba, naamini watayaona maovu yaliyomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nataka nimpongeze Mheshimiwa Hamad Masoud kwa kuwajibika. Huu ni mfano mzuri wa kuigwa, naomba watendaji wengine wa Serikali na Mawaziri wanaoona kama wameshindwa au hawawezi kuwarekebisha walio chini yao basi waachie ngazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niende kwenye bandari. Bandari ina nafasi kubwa ya kuchangia uchumi wa nchi yetu. Kama mnavyojua, bandari ni mlango wa maendeleo. Nchi nyingi hazikujaliwa kuwa na neema ya bandari, Tanzania kutokana na jiografia yake ilivyo, Mwenyezi Mungu kaibariki, kaipa bandari nyingi lakini bandari muhimu inayotumika ni ya Dar es Salaam ambayo kwa kweli ni tegemeo kubwa la kuingiza mapato lakini uzembe ulioko bandarini unakwamisha mapato kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mizigo inayotoka nje na kutoka Zanzibar. Mizigo inayotoka Zanzibar itarundikana bandarini pale na inaleta usumbufu. Sijui kuna tatizo gani *TRA* kuizua mizigo kutoka Zanzibar. Kwa hiyo, tunaomba Serikali kwa kushirikiana na

bandari pamoja na TRA tatizo hili walimalize ili wafanyabiashara wanaopitishia mizigo yao Dar es Salaam wasisumbuke, iweze kuondoa tatizo hili la kuweka mrundikano ambapo hivi sasa bandari yenye we ina mrundikano mkubwa wa mizigo inayotoka nje. Uwezo wa bandari sasa hivi kuhimili mizigo ni mdogo kutokana na udogo wa bandari yenye we ilivyokuwa imezidiwa. Lakini pia mizigo ya Zanzibar inazidi kusubiri pale inacheleweshwa zaidi. Naomba tatizo hili litafutiwe ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia bandari kwa nafasi yake ya kuinua uchumi inatakiwa ipanuliwe katika gati namba 13 na 14 lakini bado Serikali inasuasua kuipanua bandari hii. Wenzetu Kenya tayari wanaendelea kutengeneza bandari yao katika gati 17 na 18 lakini Serikali yetu bado ina kigugumizi katika kuiongeza bandari iweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizotuzunguka kama Burundi, Rwanda, Uganda, Zambia na Congo DRC zinategemea sana sisi Tanzania kwa kupitishia mizigo yao na bandari wanayoitegemea kwa sasa hivi ni bandari hii ya Dar es Salaam lakini bado hatujaliona hilo. Sasa hivi bandari ya Dar es Salaam uwezo wake wa kupitisha mizigo ni makontena laki nne kwa mwaka na nchi hizi kama Burundi wanategemea karibuni kuanza kuchimba madini ya *nickel* ambayo wanatakribani tani milioni tatu na nusu kwa mwaka ambayo ni zaidi ya kontena laki mbili. Kwa hiyo, makontena haya ikiwa yatakuja Dar es Salaam sijui tutayadhibiti vipi au tutakuwa tunaangalia wenzetu wachukue mizigo hii na kuiongeza uchumi wa nchi zao

ikiwa sisi tumelala. Naiomba Serikali kama kuna uwezekano ikachukue mkopo iipanue bandari hii kwa haraka ili tuweze kwenda na wakati. Bandari ina umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongezee hapo kwamba sisi tulikuwa na mchakato wa kutengeneza hiyo gati 13 na 14 kwa mkopo kutoka China. Lakini tuliambiwa na Benki ya Dunia kwamba kampuni hii ya *China CCC* iko katika *black list* lakini cha kushangaza ni kwamba wenzetu Kenya kampuni hii ndiyo wanaitumia kujengea bandari yao. Sasa sisi inakuwaje tunashika tu yale tunayoambiwa bila ya kutafakari? Sisi ni taifa ambalo sasa hivi lina miaka 50 na naamini viongozi walioko huko Serikalini wana upeo, kwa hiyo lazima wanapopewa ushauri watafakari kwanza, watizame yale wanayoambiwa yana maslahi na nchi yetu au ni kwa maslahi ya wale wanaotuambia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano hapa na *declare interest* hapa kwamba mimi ni *Executive Secretariat Member* wa *APNAC Tanzania Chapter*. Tulikuwa na semina karibuni hapa, walikuja wawezeshaji kutoka Canada na changamoto kubwa tuliyowaambia kwamba nchi zetu hizi zinakabiliwa na rushwa lakini rushwa kubwa ni rushwa za mikataba ambazo nchi kubwa kampuni zao ndiyo zinakuja kuchimba hapa madini au kujenga bandari au miundombinu mikubwa lakini mikataba mikubwa wanayoingia ni ya kuikandamiza nchi hizi. Kuna Mbunge mmoja kutoka Canada ambaye tulikuwa naye hapa alisema viongozi wenu wanakubali. Kwa

hiyo, jambo hili sisi lilitupa mshangao mkubwa kuwa vipi viongozi wanaambiwa tu halafu wanakubali, hawana mawazo ya kutafakari wakapima yale wanayoambiwa hili zuri na hili baya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kwanza tutizame maslahi ya nchi yetu kuliko kusikiliza yale tunayoambiwa kwa sababu hawa wanaotuambia na wao wanaangalia ugali wao unatoka huku kwetu. Kama tunavyojuua Afrika Mwenyezi Mungu ameipa neema kubwa. Neema ya madini, neema ya rasilimali na neema ya kila kitu. Afrika ina takribani theluthi mbili ya madini yote yaliyoko ulimwenguni. Kwa hiyo, lazima sisi tutafakari na uchumi ulioko Afrika kama utafanyiwa kazi kwelikweli basi sisi tunaweza kuwasaidia Ulaya. Ulaya hawana kitu zaidi ya baridi tu, labda wana hizo akili za kutuyumbisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe angalizo kwa Serikali yetu kupima yale tunayoshauriwa, jambo lenye maslahi tusilicheleweshee muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kidogo niingie katika Chuo hiki cha *Dar es Salaam Maritime Institute (DMI)*. Katika chuo hiki kuna tatizo sasa sijui Mawaziri hawa wapya walioingia wameliona au bado? Kama hawajalionna nataka niwakumbushe kidogo. Kwanza hapa nafasi muhimu za utumishi wa chuo hazina watendaji waliothibitishwa aidha wanakaimu au ziko wazi. Kwa mfano *Principal* wa Chuo anakaimu, *Deputy Principal Academic, Research and Consultancy* anakaimu. *Deputy Principal Finance Planning and Administration* anakaimu, *Internal Auditor* nafasi iko

wazi, *Tutorial Assistant Engineering* nafasi iko wazi, *Tutorial Assistant Science Management* nafasi iko wazi, *Senior Accountant* nafasi iko wazi; sasa chuo hiki kitakwenda vipi kama nafasi zote za juu ziko wazi. Je, tuna nia ya kukiendeleza chuo hiki au tunataka kife kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari nilizonazo mpya ni kwamba nafasi ya *Principal* na *Tutorial Assistants* zimetangazwa, lakini nafasi zingine zote zilizobaki zinasubiri kibali kutoka Wizarani. Hivi nini kinazuia Wizara kutoa kibali kwa nafasi hizi kushikwa? Huku ni kukimaliza hiki chuo. Chuo chenyewe kimekalia mguu mmoja. Mabaharia kama tunavyoona kama hivi wanasona lakini sijui kama usimamizi wa shahada zao uko vipi maana habari nilizopata sijazithibitisha kwamba hata huyu Nahodha aliyekuwa anaendesha meli hii ya MV Skagit hana sifa ya kuendesha meli. Sasa sijui kama Serikali jambo hili imelitizama. Kwa hiyo, naomba Serikali ikitizame chuo hiki. Chuo hiki kina nafasi nzuri ya kutuongezea nguvu kazi na pia ya kutuongezea mapato. Kwa hiyo, lazima mkitazame hiki chuo ili tuweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije hapohapo katika Chuo cha Bandari kwamba kuna pesa za madeni ya chuo zilitolewa na Wizara shilingi milioni 385.1 kwa ajili ya malipo ya madeni hayo lakini pesa zilizolipwa kwa ajili ya madeni hayo ni shilingi milioni 205.8 tu fedha nyingine milioni 179.3 hazikutumika kama zilivyoagizwa na Wizara kulipia madeni lakini zimetumika kwa mambo mengine ambayo wenyewe chuo hicho wanajua walifanyia nini. Lakini je, Serikali imechukua hatua gani

kwa watu hawa, watendaji ambao fedha za Serikali hizi wameagizwa wafanyie mambo mengine na wao wakafanya mambo mengine? Sijui wamepata wapi idhini hiyo ya kuharibu fedha hizi za umma? Jambo hili pia tunataka litizamwe ili viongozi hawa ambao wanaharibu fedha za umma waweze kufanyiwa zile stahiki zao. Kufuja fedha za umma ni jambo baya. Mimi hapa utakuta tunasaini hapa, kama hujaja siku moja basi unakuwa hupati chochote chako lakini watu fedha hizi zinagawiwa kwa ajili ya kazi maalum wao wanazifuja tu. Kwa hiyo, lazima Serikali iwe macho juu ya hili ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nzungumzie kidogo kuhusu *Air Tanzania*, nasema hili kwa uchungu sana. Juzi hapa kulikuwa na swali la Mheshimiwa Khalifa na nililiuliza kwa niaba lakini mimi kwa kweli naona aibu. Najivunia kuwa Mtanzania lakini naona aibu kuwa Tanzania haina ndege. Hili ni jambo la aibu sana, nchi zote zina *National Carrier*, hapa siku za nyuma kidogo kulikuwa na ndege lakini hata hivyo ilikuwa inaitwa *Any Time Cancelation*. Ilikuwa inafanya kazi za kwenda Dubai na nchi za karibu...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shamis, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Sasa nimwite Mheshimiwa anayefuata Mheshimiwa Mussa Haji Kombo atafuatiwa na Mheshimiwa Muhonga Ruhwanya.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na sijui ni maamuzi ya mbali sana maana yake muda mrefu tukiomba kwa sisi wengine huwa hatupewi nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kwanza nizungumzie *Railway*. Mimi siitizami kama *railway* naitizama katika uchumi. *Railway* ndiyo nguvu ya kuzalisha na kuwa na uchumi mzuri na leo tuangalie reli haidhuru Mheshimiwa Waziri anasema sasa anaendelea kuifufua. Tuitizame *railway* kutoka tangu Dar es Salaam ambapo sisi tunapanda mabasi kuja Dodoma inavyohujumu Wizara ya Ujenzi. Watu wa Ujenzi wanafanya kazi nzuri ya kujenga barabara nzuri lakini reli au uchukuzi inaua barabara zile kwa sababu ya jambo moja tu la *railway* na kama mnataka ushahidi angalieni mkitoka Dara es Salaam tukija Dodoma barabara ina matuta, ukienda Dar es Salaam barabara ina matuta lakini ukitoka Dodoma kwenda Dar es Salaam haina matuta sababu yake ni nini? Sababu ni mizigo mingi inayotumika kwa kuchukua magari makubwa kuliko *weight* ambayo inatakiwa kutumika katika barabara zile na inaporudi kutoka kupeleka mizigo magari hayana *weight* kubwa kwa hivyo njia haiharibiki upande mmoja, sasa ni matatizo ya *Railway*, ni matatizo ya Ujenzi na ni matatizo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati *railway* inafanya kazi kila kituo kilikuwa kina kazi au kina watu

wanaofanya kazi. Watu wakichukua ng'ombe kutoka Shinyanga na Mikoa mingine kwa *railway* leo ng'ombe amekuwa akipata adhabu kabla hajauliwa, anapakiwa na gari kubwa huku anasukumwa, hilo sasa linatoka Shinyanga kwa muda wa wiki ng'ombe atateremshwa njiani na mambo mengine kwa sababu ya *railway*. Usafiri wa *railway* ni usafiri wa Watanzania wengi ambao uwezo wao ni mdogo sana. Humu ndani Watanzania wanajua kila kituo kuwa *railway* itapita saa ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Chama cha Mapinduzi kitizame Sera zake katika *railway*, ni maamuzi gani wanataka kuyafanya illi kuondoa matatizo kwa wananchi wetu wa Tanzania. Ilani ya Uchaguzi wa CCM inasema kuwa itasaidia kuondoa tatizo la *railway*, wamefikia wapi katika Wizara hii kwenye Ilani yao ya Uchaguzi, watueleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni bandari, tutaendelea kutoa rambirambi, Mungu awajalie, walale mahali pema, Mungu awasamehe madhambi yao, Mungu afanye kila kitu lakini sisi tutaendelea kuaswa na Mwenyezi Mungu kwa kutotimiza majukumu yetu. Hii ni meli ya pili kwa mkondo huu wa Zanzibar lakini kuna mambo mengi yanatokea humu ndani hayaonekani leo jambo la kwanza meli inazama Bukoba, inazama Mwanza kina cha kuzama meli hata kasa anafika lakini wamekufa watu wangapi? Mwisho wakaenda wakapasua juu na maji yakaingia ndani maana yake hatuna *rescue* ya kuokoa watu wetu, hizi boti zinazozama ukiacha ile *Spice Islanders* iliyozama kwenye kina cha mita 15,000 lakini kulikuwa na nafasi

ya watu kuokolewa. Kwa kuwa ilizama *almost* saa kumi na moja za alfajiri lakini hakuna *diver*, hakuna chochote, hakuna uokozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kusema maneno haya lakini ni jambo la msingi kwa sababu Bunge liliniruhusu niende Zanzibar, meli imezama, Polisi wanaleta boti mbili za *fiber* ambazo ni nzuri kwa kuokolea, ziko chini hazina mafuta, zimekaa pale *almost two hours*, mtu mmoja akasaidia lita 200. Naiomba Wizara hii kwa sababu bandari ni muungano, watuambie maendeleo ya muungano waliyofanya kwa bandari ya Zanzibar na *expert* yote iliyofanywa ni ya upande mmoja lakini ninapenda kusema kuwa Serikali ya CCM inahitaji kuondolewa na kichukue chama kingine lakini ni chama gani chenye uwezo wa kuiongoza Serikali ya Tanzania? Ninawaomba wananchi na Wabunge wenzangu wakubali kuwa ni *CUF*. Kwa sababu gani? Tuko wa kweli na tumekuwa wawazi na uongozi wake unafahamika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Waziri akija hapa atueleze Sera ya Uchaguzi ya CCM inasemaje juu ya mambo haya ambayo nimeyazungumzia. Kwa sababu sipendi nipigiwe kengele mtu mzima, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Haji Kombo, ungesema tu kuwa una maslahi binafsi kwenye chama cha *CUF* kwa mujibu wa Kanuni kama Mbunge wa *CUF*. Nitamwita Mheshimiwa Mhonga, atafuatiwa

na Mheshimiwa Dkt. Kikwembe na Mheshimiwa Eugen Mwaiposa ajiandae.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo katika hotuba hii ya Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uhai kwa kuweza kusimama mbele yako hapa ili kuweza kutoa mchango wangu lakini vilevile ninawapa pole watu wote waliopata ajali ya meli na anajali nyingine zinazotokea kila siku lakini pia ninawatachia Ramadhani njema Waislamu wote wote wanaofunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze na ukurasa wa 60 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na ATCL. Kwa mujibu wa taarifa yake Mheshimiwa Waziri inaonekana kwamba Serikali imekodisha ndege aina ya 737-500 *Boeing* na ndege nyingine ambayo ilikuwa ikitumika ni *Dash 8-Q300* iko kwenye matengenezo. Hivi ninavyoongea, ndege hiyo ambayo ilikuwa imekodishwa imesimamishwa kufanya kazi kwa sababu hawajalipwa na ATC. Maana yake ni kwamba safari zote ambazo zilikuwa zimepangwa leo hazitafanyika. Aidha, taarifa za nyuma kabla ya hii ya leo ni kwamba ndege hii 737-500 ilikuwa inaendeshwa *on cash basis* na ukiangalia ni kwamba uendeshaji wa ndege hii tulikuwa tunatumia ma-Pilot wa nje, ninataka kufahamu kuwa ma-Pilot wetu walikuwa hawana uwezo wa kuendesha ndege hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeleo yake aliyotupa alisema tu kuwa imekodishwa, hajatuambia imekodishwa kwa kiasi gani, mimi ninapenda kufahamu Waziri atakapokuja kutujibu atupe majibu haya kuwa ilikodishwa kwa kiasi gani na imesimamishwa, Serikali inachukua hatua gani za haraka kwa sababu kama tunavyofahamu tulianza na ndege tisa, Shirika limeendelea kufa matokeo yake ni kuwa na ndege iliyokuwa imekodishwa haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wameongelea sana ajali ambazo zimekuwa zikitokea nchini na hasa ajali za sasa hivi za ndani ya maji lakini kuna ajali zimekuwa zikitokea kila siku za kwenye mabasi na tumekuwa tukishuhudia ajali nyingi za pikipiki. Ukurasa wa 29 na 30, Mheshimiwa Waziri ameelezea mwaka 2011, ajali zimeongezeka mpaka 9.37% kwa maana kuwa vifo kwa mwaka 2010 vilikuwa 640 lakini sasa hivi vimefika 700, hizo ni ajali za mabasi. Ukija kwenye usafiri wa pikipiki, ni usafiri rahisi, watu wengi wanaukimbia. Mimi ninapenda kuwashauri Watanzania wenzangu, tunapopanda pikipiki, usikubali kupanda pikipiki kwa mtindo wa mishikaki na pia usikubali kupanda pikipiki kama dereva hana *helmet* ambayo inaweza kukusaldia, wewe uwe nayo na dereva awe nayo, vifo vimeduwa ni vingi sana. Sasa hivi kuna ongezeko la vifo kwa 38%. Ukiangalia mwaka 2010 majeruhi walikuwa 4471, vifo 683 lakini sasa hivi majeruhi ni 5506 na vifo vimeduwa 945. Sasa tutafakari tunaelekea wapi na ninapenda kufahamu Serikali imejiandaaje kuwatunza watu ambao wanapata ulemavu kutokana na ajali hizi kwa sababu hizi ni ajali ambazo zimekuwa zikitokea kila mara hata ukienda

barabarani sasa hivi unaweza kukuta pipipiki tatu au nne zimedondosha watu na watu wamekuwa wakipata ulemavu na wengine kufa, Serikali imejiandaaje na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye usafiri wa reli. Ufanisi duni wa reli umeifanya Serikali yetu kutumia gharama kubwa kutengeneza barabara kwa sababu mizigo mingi ambayo ingepita kwa njia ya reli inatumia barabara. Tuboreshe reli ili wananchi au watu ambao wanataka kusafirisha mizigo yao waone kuna ufanisi wa kutosha, waiamini reli, waweze kupitisha mizigo yao hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa reli kutoka Dar es Salaam - Kigoma na Kigoma ndiko ninakotokea, nikianza kwanza na treni yenyewe, naomba nirudie haya maneno niliongea kipindi cha hotuba ya Waziri Mkuu, treni yetu au mabehewa ambayo tunatumia sasa hivi yamechakaa sana, mengi ni machafu, vioo hakuna, vyoo vimeharibika, ukisafiri kwenye treni maji hakuna mpaka ubebe mwenyewe, kuna wadudu wengi wakiwemo kunguni na mende, *fumigation* hazifanyiki kwa nini, yaani tunahitaji mtaji ili tuweze kufanya *fumigation*? Vioo madirishani hakuna, kwenye mabehewa mengine unakuta wanaweka mbao na kuna mti wa kuegeshea ili angalu usiku kujikinga na baridi na wakati mwingine jua likiwa kali sana mchana wanajikinga na jua na vumbi kwa mbao. Serikali ina mpango gani wa kuboresha mabehewa yaliyopo sasa ingawa tumeonyeshwa kuna mipango mingine lakini yaliyopo sasa yanaboreshwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanalazimishwa kukata tiketi siku hiyo ambayo ni ya safari, wanapanga mstari, wakifika watu ishirini, mstari unakatwa, wanaelekezwa duka la kununua. Kwanza mnawalazimisha watu kulala *station* kwa sababu *station* ya Kigoma kama mnavyojua inahudumia watu wengi kutoka Wilaya mbalimbali za Mkoa wa Kigoma maana yake ni kwamba mnaendelea kuifanya *station* yetu iendelee kuwa chafu kwa kuwa watu wanalundikana pale, treni ni siku mbili, siku ya Alhamisi na Jumamosi kwa hiyo, inabidi mtu atoke anakotoka aje alale *station* awahi asubuhi kupata tiketi lakini bahati mbaya tiketi haipatikani kama anavyotaka kwa sababu zinaishia katikati wanaambiwa wakanunue kwa walangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi *station* zote wanalazimishwa kununua tiketi mpaka uwe na kitambulisho. Sielewi kama usafiri mwingine kama wa mabasi watu wanalazimishwa kuwa na vitambulisho ili kukata tiketi zao, wanafanya usafiri kuzidi kuwa mgumu. Halafu unalazimika wewe mwenyewe unayetaka kusafiri ndiyo uende ukakate tiketi, sasa inaweza kuwa ni mgonjwa unaenda kumkatia tiketi, hivi mgonjwa mwenyewe atakuja dirishani ili apewe tiketi? Mimi nadhani tuangalie kama lengo lilikuwa ni kuepuka ulangazi wa tiketi lakini ulangazi bado unaendelea, kwa hiyo, Shirika la Reli au Serikali ninawaomba muende mkawashughulikie wale watu ambao wanauza tiketi kwa sababu ndiyo wanaofanya *ma-deal* na watu wanaorusha zile tiketi. Tiketi sasa hivi ni Sh.19,100 ndiyo bei halali lakini watu wanunua

mpaka shilingi 35,000, hii siyo sawa! Ninaomba muangalie utaratibu mzuri wa wananchi kukata tiketi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa pia ninaulizia usafiri wa Tabora - Kaliua mpaka Mpanda, usafiri huu unaanza lini kwa kuwa usafiri ni mgumu sana kwa watu wanaotokea maeneo ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Ardhi na Wizara ya Uchukuzi washirikiane kutatua matatizo ambayo yanababishwa na *TPA* ambao wamekuwa na maeneo yao yaani kama wana bandari kavu lakini wamekuwa wakitaka kuingilia maeneo ya wananchi wanapokaa kwa mfano Gungu kuna eneo la Katosho, *TPA* wana eneo lao toka mwaka 1964 lakini sasa wametaka *ku-expand* kwa nini wanataka kuingia maeneo ya watu na wasiende kwenye maeneo ambayo hayana watu? Kuna eneo moja karibu na Bwawa la Katosho, kuna nafasi ya kutosha, mshirikiane na wananchi ili muweze kujua mipaka yenu inaishia wapi na wao wanaishia wapi ili kuondoa matatizo ambayo yanaendelea. Ninawashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi wamelisimamia jambo hili na Mkuu wa Mkoa na ameweza kusimamisha, hakuna kinachoendelea sasa hivi lakini wananchi wamekaa hawaelewi ni nini kinachoendelea, mlimalize hili ili watu waendelee na shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *RAHCO* ni kampuni ambayo illanzishwa chini ya Sheria Namba 4 ya 2002 katika kuhakikisha kuwa inakuwa msimamizi wa mali za shirika wakati reli inapokuwa imebinafsishwa lakini mimi

sioni haja ya hii kampuni kuendelea kwa sababu lengo lake sasa hivi linaweza likafanywa na *TRL* wenyewe, kwa sababu kumekuwa na mwingilio wa kazi na itasaidia kupunguza gharama ambayo ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda harakaharaka, napenda kufahamu kuhusiana na dola milioni tatu ambazo pia tumeandika katika hotuba yetu zilitengwa kwa ajili ya kurejesha vichwa vyta treni 25 na mabehewa 23 pamoja na makontena 25 ya vipuri, zile pesa zimetumikaje kwa sababu sasa kuna matangazo kuwa viuzwe kama vifaa chakavu, ninataka kujua zimetumikaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda sehemu ya mwisho, naomba Serikali iangalie vyuo vyetu vilivyo chini ya Wizara hii, ni vyuo muhimu sana. Kwa mfano, Chuo cha Hali ya Hewa cha Mkoa wa Kigoma, ni chuo pekee ambacho kinatoa elimu hiyo. Haya maneno ya kutuambia kila siku kuwa pesa ni ndogo, haitusaidii kwa sababu tunahitaji wataalam, tuangalie ni kiasi gani tunaweza kuboresha pamoja na vyuo vingine bila kusahau Chuo cha Reli cha Tabora, ni chuo muhimu sana. Nasikitika baada ya kubinafsisha *TRC* chuo nacho kikawa kimekufa, sijui lengo lilikuwa ni nini kwa sababu tunatakiwa kuwa na madereva na watu wa kuendelea kutengeneza reli yetu kwa sababu ilitakiwa iendelee kutoa huduma nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri Lake Tanganyika ni mgumu, tunatumia meli ya zamani ya MV Liemba ambayo inakaribia kufika miaka 100. Ninaomba Serikali

iangalie ni jinsi gani inavyoweza kutusaidia tupate meli nyingine na hii igeuzwe kama hoteli ya kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya kwa mchango wako, nafikiri Kigoma wamekusikia.

Waheshimiwa Wabunge, nilisema nitamwita Dkt. Pudenciana Kikwembe lakini simwoni ndani ya ukumbi wa Bunge, kwa hiyo sasa naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Eugen Mwaiposa na atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza sana Waziri pamoja na watendaji pamoja na Serikali kwa ujumla kwa namna ya pekee kwa namna ambavyo wamekuja na mpango mzuri katika kuhakikisha kuwa sekta hii au Wizara hii ya Uchukuzi inafanya vizuri na kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, mimi naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kuchangia kuhusu sera ya uchukuzi au usafirishaji wa mizigo kwa kupitia barabara. Nadhani kwa wananchi wote lakini hata Waheshimiwa Wabunge ambao wanatoka Dar es Salaam kuja Dodoma wanaona ni namna gani ambavyo barabara hii inayotokea Dar es Salaam imeharibika. Hii inasababishwa na mizigo ambayo inasafirishwa kupitia barabara hiyo kwa kutumia malori makubwa. Kwa hiyo, nataka kumwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba anaimarisha sera ya usafirishaji ili mizigo hiyo mikubwa iweze kusafirishwa kwa reli ili kuhakikisha kuwa barabara zetu zinazojengwa kwa gharama kubwa zinaweza kukaa kwa kipindi ambacho kinastahili, lakini kwa kufanya hivyo kutasaidia sana kuimarisha reli yetu hasa katika uchumi kama mizigo mingi itaelekezwa katika kusafiri kwa reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuimarisha reli, namwomba sana Waziri ahakikishe kuwa sekta hii ya reli inaimarika ili kuwezesha bidhaa zetu nyingi kusafiri ili kutumia reli. Hilo likifanyika ni kwamba litakwenda sambamba na kupungua bei ya bidhaa mbalimbali kwa sababu reli usafiri wake ni rahisi zaidi, lakini pia itasaidia sana kuwapatia vijana ajira kama nilivyosema na itapunguza sana msongamano na ajali katika barabara zetu kubwa. Kwa hiyo, namwomba sana Waziri, ninajua ni mchapakazi, wembe ule ule aliotoka nao Wizara ya Ujenzi, basi aendelee katika Wizara hii ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la reli, nimwombe Mheshimiwa Waziri aniambie reli

inayotakiwa kutoa huduma ya kusafirisha wananchi kutoka Pugu kuelekea Mjini na maeneo mengine kama Ubungo kuelekea Mjini itaanza lini? Kwa sababu alishatuahidi kwamba hilo analifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie kidogo suala la bandari. Bandari yetu ya Tanzania kama walivyoongea Wabunge wengi inatia aibu. Inatia aibu kwa sbabu watu wengi wanalamika kuibwa vitu vyao, hata akiangalia takwimu, mwaka hadi mwaka takwimu zinashuka kwa sababu watu wengi wamekata tamaa sasa kusafirisha mizigo yao kupitia bandari yetu. Jambo hili likiachiwa bila kuchukuliwa hatua stahiki, tutajikuta wateja wengi tuliokuwa tunawategemea ambao ni nchi jirani, wamekata tamaa kusafirisha mizigo yao kupitia bandari hii. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba anaweka mikakati mizuri ya kuhakikisha kwamba usalama wa mizigo ya wateja wetu na wananchi wetu inafika salama kama inavyotegemewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijikite kwenye sehemu nyingine ya usafirishaji wa wananchi kutoka katika maeneo yao hasa pale ambapo Serikali inataka maeneo ya wananchi kwa ajili ya kupanua shughuli mbalimbali za kimaendeleo. Nianze na eneo la Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 Serikali iliwahamisha wananchi kutoka katika eneo la Kipawa, Kigilagila ili kupisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere, lakini kuanzia

wakati huo, niipongeze Serikali kwamba ilijitahidi kuwalipa na kuwafidia wananchi, lakini bado kuna changamoto kubwa. Kwa sababu Serikali ilichukua muda mrefu sana kuwahamisha wananchi hao wakati walipofanya tathmini katika maeneo hayo waliyopelekwa baada ya kuchukua muda mrefu sana, wananchi wengine waliuza maeneo yale, pamoja na wenyeviti wengine wa Serikali za Mitaa. Serikali ilipokuja kufanya *allocation*, ilikuta kwamba maeneo waliyopelekwa wananchi, tayari wananchi wengine wameuziwa na wameshaweka makazi yao. Kwa hiyo, hili limeleta mgogoro mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali iendelee kuingilia kati kuhakikisha kwamba wananchi wote hawa wawili, wale waliouziwa, aidha na vyombo vingine vyta kiserikali kama wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Watendaji wanapata maeneo ya kuishi. Lakini pia wale ambao walisafirishwa kutoka katika maeneo yao kuelekezwa kule na wao pia wanapata maeneo yao. Hii itasaidia sana kuhakikisha kwamba wananchi wanaelekeza nguvu zao katika shughuli za maendeleo badala ya kuendeleza migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika suala hilo, wapo wananchi wengine ambao kuanzia mwaka 1992 maeneo yao yalifanyiwa tathmini. Wananchi hawa ni wale wanaoishi pale Kipunguni karibu na *Airport*. Kwa kipindi chote hicho wananchi hawa hawajaweza kuendeleza maeneo yale. Nawaomba sana Serikali iwafungue sasa wananchi wale kutoka kwenye kifungo cha miaka zaidi ya 15 bila kuendeleza, bila kufanya shughuli yoyote ile ya kimaendeleo katika

eneo lao, ili wananchi wale waweze kujenga maisha yao na kuhakikisha kwamba wanakuwa na amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wanapata msongo wa mawazo kwa sababu hawajui wafanye nini katika maeneo yao ambayo wameyamiliki kisheria. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha ahakikishe kwamba wananchi hawa wanapata tamko kwamba wafanye nini. Je, waendeleze maeneo yao au inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi, lakini pia nitamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kama atakuja na majibu ya hoja zangu. Ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Eugen Mwaiposa kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge nilisema nitamwita Mheshimiwa Stephen Ngonyani, simwoni ndani ya Ukumbi wa Bunge, naomba sasa nimpe nafasi Mheshimiwa Omari Nundu atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Moses Machali halafu nitaendelea na wengine.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa leo na kuchangia kwa niaba ya wapiga kura wa Wilaya ya Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naisifu Wizara na Mawaziri kwa kazi nzuri ya mwaka uliopita na kwa mipango mizuri ya huko mbele tuendako. Kwa sababu hiyo basi, mimi nimetumwa na wananchi wa Tanga kuiunga mkono hoja hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa sababu kadhaa. Sababu ya kwanza, tumeambiwa na Mheshimiwa Waziri hapa kuwa wananchi wa Tanga ambao ardhi yao waliambiwa waiweke kwa ajili ya kutumika kwa matumizi ya *RAHCO*, sasa Septemba mwaka huu watalipwa. Wananchi hawa wameahidiwa mara nyingi na mara ya mwisho wameambiwa wangalipwa Aprili, sasa hii ya kusema watalipwa Septemba, wananchi wameona waipongeze Wizara kwa kazi nzuri kama hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna matatizo mengine ambayo ningeomba Wizara iyashughulikie. Kuna tatizo la wastaa fu ambao mpaka leo hajalipwa pesa zao, mwanzo ilikuwa mafaili hayaonekani, mafaili yameonekana na orodha ipo wao pia tungeomba washughulikiwe ili walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Wizara kwa sababu ya kazi ya ziada. Tatizo la Dar es Salaam, reli ilianza kushughulikiwa, lakini sasa naona linakwenda kwa kasi nzuri na msongamano wa Dar es Salaam tunategemea utaondoka. Tunayo Kampuni ya *S/NOTASHIP* ambayo ni ubia na Wachina, waliomba Kampuni ile ishughulikie kuleta meli katika bandari zetu na hilo sasa linatokea. Kwa hiyo, tunawapongeza sana kwa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Reli ya Kati ina pande mbili mbili. La Kwanza ni kuchanganya usafiri kwa muda mfupi, na pili ni lile kubwa la kujenga reli ya *standard gauge*. Mwaka uliopita 2011 Wizara ilijitahidi sana kushughulika kwa kujaribu kuwekeza kwenda kwenye ukarabati na kununua mabehewa. Ilifika mahali ikaonekana hili linagonga mwamba. Lakini kuna jopo la Watalaaam wa Tanzania wengi wenye uwezo, ambao walikaa na kujadili hili wakaja na njia nyingine mbadala ya kuweza kufanya reli ile ianze kufanya kazi mara moja wakati tunangoja kuwekeza kwa *standard gauge*.

Katika bajeti, nimeona tumerudi kule kwenye kuwekeza kwa kununua mabehewa, kukarabati mabehewa, na kununua vichwa vyta treni. Ununuzi unachukua muda, kukarabati pia inachukua muda, hatujajua hapa kukarabati huku na ununuzi huu, vifaa hivi vitapatikana lini. Kwa sababu kama vitapatikana ndani ya miaka mitatu halafu ukichukulia tena vitatumika tena kwa miaka kadhaa labda kumi, wakati hapo papo haviwezi kutumika katika *gauge* mpya ya reli inayokuja itakuwa tumewekeza mahali ambapo sipo. Ni ombi langu kuwa hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wakati tunafanya hivyo, lakini pia kuna reli ya Tanga mpaka Musoma, ambapo reli hii Uganda wanataka kuitumia kweli, kiasi cha kuwa Rais wa Uganda alikuja hapa siku nzima kulijadili suala hili na Rais wa Tanzania. Tumeshaingia mikataba na Kampuni ya Kichina ambayo inafanya *feasibility study* pale pamoja na wenzetu wa Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ule mradi wa Tanga mpaka Musoma ambao una vipengele sita sasa hivi utumike kama mfano wa kwanza wa kujenga reli ya *standard gauge* hapa Tanzania kwa sababu kule hakuna matatizo, reli ile haifanyi kazi sasa hivi. Kwa sababu haifanyi kazi, haina matatizo ambayo yapo kwenye reli ya Kati wakati inafanya kazi. Kwa hiyo, tutumie mradi ule siyo kwa sababu hiyo tu ambayo iko wazi kufanyiwa hivyo, lakini pia kwa ule umuhimu wa kutumika kwa Uganda ambao wana mori sana wa kuitumia reli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati hilo linafanyika, tuangalie na vitu vingine ambavyo vinajitokeza. Korogwe kuna sehemu kubwa ambapo watu wa Korogwe wanataka kuweka bandari ya nchi kavu. Imepatikana sehemu kubwa Musoma sehemu ya Ikundi kwa Bandari ambayo bado tunahitaji imilikiwe. Bukasa - Uganda wameweka hekta 800 lakini Bandari ya Tanga ni hekta takribani 200 tu, ambayo ndiyo Bandari Mama katika mfumo mzima huu, inahitaji kuongezwa. Ndiyo maana suala la kuweka bandari kavu Musoma, Korogwe ni suala la kutilia maanani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bandari ya Dar es Salaam, Serikali iliamua tangu mwaka 2008 kuwa tujenge gati ya 13 na gati 14. Tungeingia katika mchakato wa kawaida wa manunuzi kwa kujenga bandari hiyo, ukichukulia mabenki ambayo walishaonesha nia kwa kusaidia katika hilo, leo hii tungekuwa tuna gati ya 13 na gati ya 14. Mwaka 2008,

2012, tungekubali Benki za ndani ya nchi na jirani watukopeshe tungekuwa tumefika huko. Hatukufika huko kwa sababu mwaka 2009 walijitokeza hapa, hii kampuni tunaifahamu, tumeendelea na mchakato huo mpaka leo. Juzi hapa tuliambiwa fedha za *Exim Bank* ziko tayari, lakini mpaka sasa hivi tunaambiwa bado mchakato unaendelea na sijui itafika wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kumejitokeza mambo mengine *PPRA* wameifungia Kampuni hii pamoja na Kampuni nyingine karibu 340. Sasa tutake tusitake kwa sababu hawa wanafuata sheria za kufungua Kampuni ambazo zimefungiwa kwa sababu zimejihusisha na rushwa na udanganyifu mwingine. Hizo ndiyo sababu mbili kubwa. Tutake tusitake, aidha tudharau yale ya *PPRA* tuendelee kuipa au twende na malumbano ya kujua tutafika wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri umefika wakati wa kuamua na kufanya maamuzi. Kama mkopo wa *Exim Bank* unapatikana, zitafutwe Kampuni za Kichina ambazo hazijaingia kwenye matatizo kama haya ili ipatikane. Haupatikani mkopo kwa Makampuni yaliyopo. Mabenki ya ndani ambayo yanataka kutukopesha, tuamue twende tujenge hizi gati. Haiwezekani hivi, maana yake huu ni mradi mdogo sana ukiangalia miradi yote, hii miradi mikubwa ya Reli na kadhalika, tingoje watu ambao wana pesa.

Kwa mradi huu hata Watanzania wenyewe wanaweza wakaugharamia, zile pesa zinazopatikana pale zikawa ni za Watanzania. Tulianza kuongea tayari na baadhi ya Watanzania kuona watakuwaje wao

kama ni *nucleus* ya kutengeneza *special purpose vehicle* ya kufanya hivyo. Ninachotaka kusisitiza, tusiendelee kuendeleza malumbano katika hili, mradi huuujengwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Philipines CCCC walifungiwa tarehe 12 Januari kwa kashfa hizo, Machi 2009 likatoka jopo letu hapa kwenda kuwafanya *due diligence*. Sasa tangu wakati ule tungejua tuna matatizo. Sasa turudi huko tutafute mbinu za kuendelea kufanya hivyo. Mambo ambayo yamefanywa hapo katikati yanaashiria rushwa. Haya ni mambo ambayo yako wazi, isijekuwa nasi hapa tukapitisha vitu halafu Bunge likaonekana limepitisha vitu ambavyo vinaashiria rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee kuhusu Viwanja vya Ndege. Serikali imeshalenga viwanja vingi ambavyo vitatumika baadaye na ni vizuri kufanya hivyo, kwa sababu baadaye utakapokuja kulipa malipo ni pesa nyingi. Lakini katika ukurasa ambao viwanja hivyo vimetajwa nimeona vimetajwa baadhi ya viwanja tu, kuna kiwanja cha Nyasurura kule Musoma hakikutajwa katika ukurasa wa 89, labda hiyo ni kusahau tu. Lakini naomba tuweke ardhi sasa hivi ambayo haitatugharimu katika malipo wakati tutakapo hitaji mbinu hizo zizidi kuendelea. Kile Kiwanja cha Tanga siyo kiwanja cha kukidhi matakwa kwa siku za mbele. Zipo sehemu za Tanga kama Madanga, Mkinga tunaweza kwenda kule tukapata sehemu tukaweza kuepukana na kuja kulipa pesa nyingi baadaye.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Nagu, unakatisha mbele ya mzungumzaji.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika zangu zilindwe. Mashirika yetu yana uzoefu wa kupewa ruzuku na huko tulikuwa tunataka kuyafanya yapate *working capital* yajienteshe. Kama ajali imetokea, ile ndege kule Kigoma hatuna thamani nayo tena. Tumelipwa Shilingi bilioni 12, *Air Tanzania* mwaka 2011 tulisema tuwapatie *working capital* wafanye kazi kibashara, *Air Tanzania* tunahitaji, lakini tunahitaji Menejimenti ambayo inaweza kuendesha *Air Tanzania*. Tatizo hili lipo *Air Tanzania*, kwa bahati mbaya hata bandarini tatizo hili lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bahati mbaya sana, kule TAZARA pia tatizo hilo lipo sana na kule tulishaanza kulishughulikia na kuondoa baadhi ya Mameneja na wana bahati kwa sababu nilichelewa kidogo tu, wote wangetoka pale!

Mheshimiwa Mwenyekiti, namsifu sana Mheshimiwa Waziri kwa mambo anayoyafanya, lakini ayafanye kwa bidii. Lakini kwenda kwa vitendo sehemu za kazi, tulikwenda Ubungo mara kadhaa, tukaingia kwenye daladala na kadhalika, *incognito*, kuweza kukusanya mawazo, na mwamko huu ambao ulianza kwenye Wizara naona unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kuunga mkono na kuwaombea kila la kheri katika safari hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nami nianze kwa kuwapongeza Waziri wa Uchukuzi, Naibu wake na Watendaji wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hali ya uchumi wa Tanzania, katika sekta ambazo zinaleta pesa nyingi kiuchumi ya tatu, ni Sekta ya Uchukuzi. Lakini tukiamua, Sekta ya Uchukuzi inaweza ikaongoza kwa kuleta pesa Tanzania. Ndiyo Wizara pekee, kwa sababu Mungu ametusaidia, tunayo jiografia nzuri sana kama nchi yetu, Tanzania ni kati ya nchi chache ambazo zina nchi karibia saba ambazo zingetutumia sisi kufanya biashara, nasi tungepata pesa nyingi sana. Lakini kwa bahati mbaya sana, aidha tunajua, ama hatujui. Kama tunajua, tunaona ni kawaida tu. Lakini hii ni biashara ambayo ingeingiza pesa nyingi kuliko hata dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mzigo ulipo Congo, Burundi, Rwanda, Malawi, Zambia; kama wote tungefanya kazi kuchukua ipitie kwenye bandari zetu kwa maana ya Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Tanga na Bandari ya Mtwara, leo Tanzania Idara hii ya Uchukuzi ingeleta pesa nyingi sana. *Transit trade* ni biashara kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ili watu watumie bandari yetu, ni lazima tufanye nini? Tunalo tatizo kubwa la *efficiency*. Bandari zetu pamoja na njia zetu za kupeleka mizigo, hii *efficiency* ni ndogo sana. Lazima tuhangaike na tatizo la ufanisi ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wenzangu wamesema tunalo tatizo la reli, tunataka reli. Tunaihitaji reli kuliko kitu chochote ili iweze kusaidia katika uchumi wa nchi yetu. Haya ninasema katika *transit* trade peke yake, lakini kwa maisha ya watu wa Mikoa ya Kigoma, Mwanza, Kagera, Tabora Mpanda kwa maana ya Katavi na huko Mbeya, wote kama reli hizi zingefanya kazi vizuri, ugumu wa maisha ya watu yangepungua sana ama yangeimarika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mfuko wa simenti unauzwa Sh. 14,000/= Dar es Salaam ukienda Kigoma ni Sh. 25,000/=. Kwanini Sh. 25,000/=? Ni kwa sababu ya gharama ya usafirishaji. Hivyo hivyo kwenye unga, sukari na kwenye bidhaa zote ambazo zinatoka viwandani. Kule unakopeleka vijijiini kwetu vinauzwa kwa bei kubwa sana. Lakini kinyume chake mazao yanayotoka Rukwa, Kigoma ukienda kununua kule vijijiini bei ni ya chini sana. Kwa hiyo, mtu anauza mahindi yake kwa Sh. 5,000/= lakini anakuja kuuza huku kwa Sh. 20,000/= ama Sh. 30,000/= lakini ye ye atakapotaka kununua bidhaa kutoka viwandani anazinunua kwa bei ambayo ina gharama za usafirishaji.

Kwa hiyo, unaweza ukaona tuna-run economy mbili *in this country*. Kuna economy za watu wa vijijiini ambazo wanaponunua vifaa vyaa viwandani wanatumia fedha nyngi sana. Lakini biashara zao kwa maana ya mazao yao yananunuliwa kwa bei ya chini sana. Inabidi mtu auze mikungu ya ndizi mitano kununua kanga moja. Lakini mikungu mitano kule Kalinzi, mkungu wa ndizi ni Sh. 500/= na hata hapana

wanunuaji. Kwa hiyo, ili mwanamke wa kijiji pale aweze kununua khanga ya Sh. 3,000/= inabidi auze mikungu ya ndizi sita. Lakini mkungu huo mmoja ukifika Dar es Salaam ungenunua kanga tano. Kwa hiyo, unaweza ukaona hapa tunalo tatizo na jibu pekee kwa kweli ni reli peke yake. (*Makofii*)

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri tuhangaike na reli. Mimi nasikitika sana, wenzetu nchi zinazotuzunguka hawako kwenye barabara, wako wanatafuta fedha kujenga reli zao. Nitakupa mfano mdogo tu.

Juzi kulikuwa kuna Mkutano mkubwa kwa ajili ya kujadili maendeleo ya Afrika na China. Rais wa China ame-*pledge* Dola bilioni 20 nchi ya Kenya, amekwenda Waziri Mkuu na Mawaziri sita kwenye Mkutano ule, sisi wamekwenda watu wa kutoka Wizara ya Fedha, watu wa kawaida tu. *You can see how hatuko serious katika haya mambo.* Wao wamekwenda pale wameshika miradi mikononi, sisi tuna miradi tunaiiongea tu hapa mbele ya Bunge, tunaongea kwenye magazeti, tumeshikilia miradi. Lakini kwenda kutafuta fedha, hatufanyi. Sababu ni nini? Mimi sielewi. Tukizubaa tunadanganywa na nchi za Magharibi. Sasa kuna vita kubwa ya Magharibi na China inataka ku-*take over Africa*, nchi ambazo zimejiandaa, China watawasaidia. (*Makofii*)

Juzi tarehe 11 Julai, Kenya wamesaini Mkataba na China wa kujenga reli kutoka Bandari ya Mombasa wakielekea *2.6 billion dollars*. Mwaka 2011 mwishoni watu wa Ethiopia wamesaini Mkataba pamoja na

China 1.5 billion dollars kujenga reli. Sisi reli tunaihitaji, bandari tunazihitaji, sisi tunahitaji maendeleo lakini tunaringa. Yaani tunavyofuutilia mambo yetu ni kwa kuringa, tatizo ni nini? (*Makofi*)

Wenzetu wa Angola, wamekwenda China wamekaa pale wame-negotiate wamepata Dola bilioni tatu kwa ajili ya kujenga reli na barabara zao. Sisi bado tuko kwenye mchakato, bado tunajadili, tuko kwenye mkakati, tumefika mbali sasa, mpaka lini? Matokeo yake tunaingia kwenye sehemu ya hizi *wrangle* za wafanyabiashara, zinataka kutu-*derail* kujenga reli zetu, zinataka ku-*derail* kujenga bandari zetu. Mheshimiwa Waziri kati ya watu wachache wanaokuamini mimi nakuamini sana. Nakuomba toka nenda katembee ufuutilie fedha hizi. (*Makofi*)

## TAARIFA

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa. Kwa mujibu wa kifungu namba 68 (8) ningependa tu kusahihisha kwamba kwenye Mkutano wa China na Afrika mimi ndiye niliongoza ujumbe wa Tanzania pamoja na *Deputy Minister* wa Viwanda na Biashara. Ni kweli kwamba Kenya walimtuma *Prime Minister* kwenda kule, lakini alikwenda kwa *capacity* ya kuwa Mwenyekiti wa *East Africa*, kwa sababu viongozi wote wa *Regional Cooperation's*, wa *Regional Groupings* za Afrika ndio walitakiwa kwenda China pamoja na wengine. Kwa hiyo, Mzee Kibaki alikuwa na afya mbaya. Kwa hiyo, *Prime Minister* wake ndiye alikwenda kule. Ujumbe tuloutuma kule katika nchi 54

zilizokwenda kule nchi 39 ziliongozwa na Mawaziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Mawaziri wengine. *So it was a highly powered delegation. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Serukamba taarifa unayopewa ni kwamba, Serikali yetu ilituma Mawaziri, na sio watumishi tu wa Wizara ya Fedha kama ulivyosema. Taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea.

**MWENYEKITI:** Naomba uendelee.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado *whatever* tutakavyosema, bado hatuchangamkii ipasavyo hii miradi. Hili lazima tulikubali. Hata tusipolikubali tumeamua tu, lakini tunavyochangamkia fedha hizi *pace* yetu ni ndogo kuliko wenzetu. Iko miradi ambayo tulikwenda China na Wakenya wao wameanza kujenga sisi bado tunapiga maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema, nia yetu ni moja. Tunasema bajeti ilivyo hatuwezi kujenga *infrastructure* hizi kwa kasi ambayo tungeipenda. Tukiamua kusema tujenge reli hii ambayo leo tumetenga Shilingi bilioni 250 kwa reli ya kati ambayo ni kwenda kukarabati, tutaka tuijenge kwa *standard gage* tujenge reli ya kwenda Musoma, tujenge reli ya kwenda *Mbamba Bay*, tujenge reli ya kutoka Mtwara kwenda mpaka Liganga kwa bajeti hii ya Shilingi bilioni 250. Hii ni ndoto ya mchana, hatuwezi kufanya! Mtu

asimame hapa aniambie, kwa bajeti hii tuliyotenga tunaweza kuyafanya haya yote? Haiwezekani! Kwa hiyo, tutaishia kwenye ukarabati, kwenye kuweka mabehewa ambayo baada ya siku mbili yanakatika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema, Serikali yetu hii ina uwezo, Tanzania tuna *resources*. Tukiamua kutumia *resources* tulizonazo, hata kukopa kwa kutumia *resources* hizi, tunaweza tukafanya haya yote ambayo tunataka kuyafanya. Kwa kweli tusipofanya, wale wenzetu, kesho kutwa miezi 18 ijayo Msongati wanaanza kuzalisha *Nikel* kama itakuwa reli haipo, bandari yetu hatujafanya hawataleta mzigo wao hapa. Leo tumeambiwa *Copper* inayotoka *DRC* pamoja na baadhi ya *copper* inayotoka Zambia imeanza kwenda Beira, imeanza kwenda Durban. Kwa hiyo, kama tutaendelea kusema sisi tuko kwenye utaratibu, tunafuatilia na sisi tuna nia njema, ni jambo jema. Naamini kabisa, lakini watatuacha. Siyo lazima watutumie sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu anachukua lori lake amepakia mizigo Dar es Salaam inafika mpakani baada ya siku 50 na akipitia Mombasa itafika mpaka baada ya siku 20 atakwenda wapi? Atakwenda kule ambako atafanya biashara kwa haraka. Dunia haitusubiri! Dunia hii sasa hivi ni mapambano. Tusipopambana, tutabaki tunaangaliana, tunatafutana uchawi, tunafanya nini huko ndiko tutakakokwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema, maendeleo yanahitaji tuwe *very aggressive*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, namwomba Mheshimiwa Waziri, Kigoma kwa maana ya reli na uchakachuaji wa zile tiketi, wazisimamie. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, namshukuru sana Mheshimiwa Peter Serukamba kwa mchango wake. Sasa ni zamu ya Meshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nianze tu kusema kwamba siungi mkono hoja kwa asilimia 100 kwa sababu za msingi. Naomba nieleweke ni kwa nini siungi mkono hoja. Moja, bajeti ya mwaka 2011/2012 hajiatekelezwa kwa asilimia 100 kama ambavyo Bunge letu Tukufu mwaka 2011 liliweza kuidhinisha fedha za miradi za maendeleo takribani Shilingi bilioni 262 kwa ajili ya kuiwezesha Wizara kufanya kazi zake vizuri.

Kwa hiyo, kigezo hiki ambacho ninakitumia, imekuwa ni mwaka hadi mwaka, Bunge linapitisha bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Uchukuzi, fedha hazikutolewa zote, kwa hiyo, ndiyo maana yake. Tafsiri yake nini? Tafsiri yake, ndiyo maana kuna kusuasua kwa Reli ya Kati, kuna kusuasua kwa reli ya TAZARA na Taasisi mbalimbali ambazo ziko chini ya Wizara hii. Kwa hiyo, siungi mkono hoja kwa sababu bajeti zetu tunazopitisha hapa inakuwa ni kama vile tunafanya maigizo.

Kwa hiyo, nategemea labda pengine kwamba sijui kwa mwaka wa 2012/2013 kama inawezekana *style* ile ile ikaendelea kuweza ku-exist kwa sababu ya misingi na mazoea ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze moja kwa moja kuhusiana na TAZARA. Kuna kitu kimoja cha kukiangalia. Ni kwamba Watanzania inawezekana tulikuwa tumelala wakati tunapitisha Sheria ya TAZARA ya mwaka 1975. Sheria ina-state wazi kwamba Mkurugenzi Mkuu wa TAZARA ni lazima atoke Zambia na kwamba *always* Msaidizi wake atatoka Tanzania. Hivi najiuliza, Wabunge waliokaa na kupidisha sheria hii walikuwa wanafikiria nini kusema kwamba kila wakati Mkurugenzi Mkuu atoke Zambia? Hivi hatuna watu ambao wanaweza waka-*hold* hii *position* ya kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TAZARA kwamba kila wakati atoke Zambia?

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, tumeonana na wafanyakazi wa TAZARA kwa upande wa Tanzania, wanalamika kwanza ni wachache, lakini pia hata *position* kubwa kubwa, kama *Finance Manager* anatoka Zambia, Meneja Mkuu wa TAZARA anatoka Zambia. Sasa unajiuliza, hawa watu ambao walipitisha sheria hii, inawezekana na wengine wako humu humu bila shaka, hata *Madam Speaker* alikuwa ni Mbunge labda miaka hiyo, sijui na wenzangu sijui mlifanya kitu gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali naomba ujielekeze kwenye hoja zako, nadhani siyo vizuri sana pia kutumia mfano wa Mheshimiwa Spika.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Naomba uendelee. Endelea.

*(Hapa Mheshimiwa Ali Mohamed Keissy alisimama)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Ahsante. Mheshimiwa Keissy kaa chini kidogo, Mheshimiwa Mwenyekiti, ameshatoa mwongozo wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali unaongea na Kiti, hauongei na Mheshimiwa Keissy humu ndani.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ahsante. Kwa hiyo, ninachokisema ni kwamba, maamuzi ya Bunge ya kupitisha Sheria hii hayakuweza kuangalia mbali sana juu ya suala hili kwamba Mkurugenzi Mkuu wa TAZARA atoke pande zipi.

Nafikiri kuna haja Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi na Serikali kwa ujumla mlete Muswada juu ya mabadiliko ya Sheria hii ili kuhakikisha kwamba fursa ya kuweza kukalia kiti cha Mkurugenzi Mkuu wa TAZARA iwe ni kwa kubadilishana. Haingii akilini kuona kwamba kila wakati anatoka kule nchini Zambia halafu kuna madudu makubwa ambayo yanaendelea kufanyika hata umesikia kwamba kuna yale mabehewa ambayo mengine yalipelekwa Congo kwenda kufanya kazi,

ambayo ni mabehewa yanayomilikiwa na TAZARA yamekwenda kuwanufaisha wenzetu wa Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake atueleze ni lini mabadiliko ya sheria hii yataletwa ndani ya Bunge letu? Mmefanya *efforts* zipi kwa kuwasiliana na Serikali ya Zambia juu ya suala hili ili kuhakikisha kwamba kunakuwa kuna *checks and balances* kwenye suala la *ku-hold* hii *position*? Vinginevyo nafikiri nashawishika kuweza kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, waikatae bajeti hii kwa kuwa hili jambo tumelizungumza sana kuanzia kwenye Kamati. Kwa hiyo, ningependa tuweze kupata ufanuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kuzungumzia juu ya suala la ujenzi wa *gate 13* na *gate 14* kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam. Naomba nichukue fursa hii kuishauri Serikali hii ianze mchakato wa kuweza kufanya *feasibility study* na kujua gharama halisi za ujenzi wa mradi ule, uletwe haraka ili kusudi pengine lile *gate* liweze kujengwa mapema kwa sababu ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu. Pengine labda nisisitize tu kwamba yale Makampuni ambayo yalikuwa ndiyo yanaonekana kuweza kumendeamendea na kuweza kupewa *tender*, ninashauri mchakato uanze upya kabisa. Mheshimiwa Waziri nina imani kubwa sana na wewe.

Kwa hiyo, tungependa tuweze kupata taarifa. Kwa sababu nikiangalia kwenye hotuba yake umeeleza tu kwamba mchakato unaendelea na pengine umekuja kutoa taarifa. Tulitegemea kwamba

kwenye Bunge hili ungetupa kitu kizima kwamba mpaka dakika hii mmeweza kufanya kitu gani. Lakini inaonekana kwamba mchakato bado unaendelea. Sasa hebu uje utueleze kwa kina juu ya suala hili na pengine tujue sasa kwamba ujenzi wa *gate 13* na *14* utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikishatoka hapa, naomba nzungumzie Reli ya Kati. Ukajaribu kuangalia hivi sasa utaona kwamba Reli ya Kati imekuwa inasuasua. Tunaelezwa kila siku hapa kupitia maswali mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wamekuwa wanauliza, hivi ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge* utaanza lini na utakamilika lini? Imekuwa kwamba michakato inafanyika, *feasibility study*, hizi *feasibility study* zitakwisha lini? Naomba Serikali itueleze *feasibility study* hizi zitakwisha lini? Inawachukua muda gani? Ningeomba tuweze kupata ufanuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia vile vile, binafsi nina mtazamo ufuatao, kwamba kusuasua kwa Sekta ya Reli hapa nchini ni kwa sababu ya uwepo wa malori mengi, Makampuni mengi ya usafirishaji hapa nchini. Inawezekana kabisa ukijaribu kuangalia watu wenye malori hawataki kuona reli ikifanya kazi kwa sababu itaweza kuua biashara zao.

Mheshimiwa Waziri naomba nitoe wito kwenu na niwashauri ninyi ambao ndio sasa mnatuongozea Wizara hiyo. Mmeaminiwa na mmepewa heshima kubwa sana kuweza kuhakikisha kwamba moja ya Taasisi ambazo zinafanya kazi vizuri, iwe ni Sekta ya Reli

nchini, hebu mtueleze na mjaribu kufuatilia kwa kina, hivi inawezekanaje vitu vyote ambavyo ni via *public*, kwa maana vitu ambavyo vinamilikiwa na Serikali vinakuwa vinasuasua? Nenda kwenye ndege, ndege zinasuasua, nenda kwenye reli, reli inasuasua, lakini malori ya watu, watu ambao wanamiliki Makampuni ya Usafirishaji kila siku yanafanya kazi ya kuitisha mizigo na yanatuharibia barabara zetu.

Kwa hiyo, upo ushahidi wa kimazingira, wala hatuhitaji kwamba mpaka kuwe kuna *document*, maana yake Watanzania wamekuwa ni mabingwa wa kuangalia kama una ushahidi wa maandishi. Wanauliza, una ushahidi wa maandishi? Ila ushahidi wa kimazingira hawaangalii. Kwa nini malori yanafanya vizuri halafu reli inasuasua? Hii ni dalili ambayo iko wazi kwamba hawa watu wana mkono mrefu. Inawezekana kuna watu ambao kwenye Wizara yako Mheshimiwa Waziri wanaweza kuwa wamekamatwa, matokeo yake hata fedha kidogo ambazo zinapatikana kwa ajili ya kwenda kuhakikisha kwamba reli inafanya kazi, wao wanazitia mfukoni kwa ajili ya maslahi yao binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba fedha kidogo ambazo Serikali imekuwa ikitoa kwa ajili ya reli, hebu zikafanye kazi vizuri kuhakikisha kwamba Reli ya Kati inaweza ikaendelea kama ilivyokuwa miaka ya nyuma. Haingii akilini kuona kwamba malori yanafanya kazi vizuri, Makampuni ya Ndege yanafanya kazi vizuri, lakini Makampuni ya Ndege kwa upande wa Serikali hayafanyi vizuri, lakini reli choka mbaya. Mheshimiwa Kafulila jana alizungumza hapa kwamba tutakuja

kushushana misuli bure! Lakini tutaendelea kuchoshana na kutunishiana misuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, zipo taarifa ambazo zimewahi kuandikwa na magazeti kwamba Kampuni ya *RITES* ambayo ilikuwa ikijihuisha na uendeshaji wa Reli ya Kati haikulipa kodi inayodaiwa takribani Shilingi bilioni tatu. Ningependa niweze kupata ufanuzi wa Wizara, nini *position* ya Serikali kuhusiana na hizi Shilingi bilioni tatu ambazo zinatajwa kwamba Kampuni ya *RITES* haikulipa kodi Serikalini? Nitaomba katika majumuisho yenu Mheshimiwa Waziri tuweze kupata ufanuzi wa kina, hizi Shilingi bilioni tatu zililipwa au hazikulipwa, maana hata magazeti yalivyoandika, hamkutoa kauli ya Serikali. Tunaomba tujue na kama hawajalipa, nini mustakabali wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo. Nakushukuru sana. Ahsante. (*Makofii*)

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mheshimiwa Jenista Mhagama. Nashukuru kwa kupata nafasi hii kuweza kuchangia katika Wizara hii. Kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi nyingine tena niweze kuchangia katika hii Wizara. Kwanza, napenda kusema, nafurahi kuchangia katika Wizara hii baada ya mabadiliko ya Mheshimiwa Rais wetu kumteua kaka yangu Dkt. Mwakyembe na ndugu yangu Mheshimiwa Tizeba. Ninaamini na nitawaombea kwamba mtafanya kazi vizuri, wananchi watafurahi kwamba kwa kweli Bunge litasema tukifanya kazi, kazi

inatendeka kwa sababu CV ni nzuri. Naomba mzifanyie kazi.

Baada ya kusema hayo, naomba nichangie mambo kama mawili au matatu. Jambo la kwanza kabisa ni kwamba, nakubaliana kabisa na msemaji aliyeppita. Mambo mengi ni ya ajabu kabisa kwamba yapo lakini hayatekelezwi. Sisi Wabunge humu ndani kama tunavyosema, kila mara tunakaa tunalamika, lakini kwa nini tunaendelea kulalamika wakati ni sisi wenyewe ambao hayo mambo tunayajua, tunayo, lakini hatuyafikishi mwisho?

Kwa mfano, kama suala alilosema; mimi nilikuwa naijuliza, na nikawa nafikiri nkipata nafasi nitauliza swalii kama hili, kwamba reli zetu tunajua bila kuelezwa, toka tumeanza kujifunza katika Shule za Msingi kwamba reli ndiyo chombo muhimu sana kwa ajili ya kubeba mizigo na kwamba hata Wakoloni hawakuwa wajinga wakatengeneza reli kutoka kwenye vitu vinakopatikana, mfano, mazao na kadhalika, zikaenda bandarini kusudi zipeleke mizigo. Lakini sisi tulipochukua tukaanza kufanya kinyume chake. Matokeo yake tuko hapa tunalamika. Hiyo Reli ya Kati iliyojengwa na Mjerumani ikamaliziwa na Mwingereza.

Mimi nilikuwa naijuliza, baada ya Watanzania wenyе nia njema na nchi hii kulalamika na kuona mambo yaliyotokea na wafanyakazi wenyе uzalendo wakajitolea kwamba wangeweza kufufua vitu vingine mpaka hadi sasa hiyo reli ikarudi mikononi mwetu, lakini jamani hatujulizi kwamba huu si ndiyo utakuwa mtindo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wote ambao walifanya mkataba mbovu wa hii reli mpaka wakatuletea mateso makubwa kama haya ambayo hata sasa hivi tunashindwa kutoka huku kwenye *RITES*: Je, hawa walichukuliwa hatua gani? Ningependa hili pia Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Mwakyembe ajaribu kututonya, wamechukuliwa hatua gani? Narudia usemi wangu na wito wangu kila wakati kwamba, kama mtu akifanya jambo baya, akavurunda, sijui kaiba, sijui kapewa rushwa, sijui kafanya nini, halafu anapokuja mnamtua tu mnambwacha anabaki na zile mali, anaendelea *ku-paralyze system*. Ingefika wakati huu tuwe na kitu cha *ku-monitor*, kufuatilia mpaka mwisho, wale tuwaangalie maisha yao na tuchukue na wawajibike. Suala hapa tunakuwa tunarudia mambo yale yale, hayafiki mwisho, tunagombana! Nilikuwa naomba tujue watu wote walioleta ubovu wa hii Reli ya Kati, akina *RITES* na watu wao wa mikataba waliobebana, walifanywa nini? Tuweze kujua na walichukuliwa hatua gani? Kusudi tuwe tunachukua kama masomo kwa wale wengine ambao wana nia ya kusema na mimi nikienda pale nitabeba *change*, halafu nitaondoka na imikuwa ndiyo mtindo sasa hivi. Kwa hiyo, hilo nilikuwa naomba lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo nilikuwa napenda nizungumzie, ni suala linalohusu kule *TAZARA*. Kwa bahati mbaya, wenzetu sijui wametuzidi nini? Wanapopanga kitu, wanapanga na jinsi gani kitakavyokuwa kinaendelezwa, *sustainability*. *TAZARA* ilivyokuwa inajengwa, mimi kwa fahamu zangu.

Nafahamu kwamba wale Wachina walitujengea, sijui walitupa zawadi karakana iliyokuwa inaitwa Mang'ula. Ile Karakana ya Mangula, ulikuwa unaweza kutengeneza vipuri vya aina zote na ilikuwa haipo katika Afrika Mashariki. Sasa kitu cha ajabu, nilipokuwa katika safari za Kamati, mimi niko katika Kamati ya Viwanda na Biashara, nikasikia kwamba ile Karakana eti iliuzwa. Sijui iliuzwa kwa vipi? Sijui kwa nini? Lakini kilichonisikitisha ni kwamba imebadilishwa matumizi yake, ile Karakana badala ya kutengeneza vipuri vya kuendeleza treni, Reli sio tu ya *TAZARA* pia hata Reli ya Kati sasa inabadilishwa sijui inakuwa Sekondari, sijui inakuwa kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikafikiri, nikamwambia Mwenyezi Mungu, kwa nini sisi tumekuwa hivi? Tumelaaniwa? Tumelaaniwa kwa kweli, kama kitu muhimu kama hicho, bado tuna Reli, magari, bado tutahitaji vipuri, badala ya kuendeleza, sisi tunaanza kuuziana. Afadhali tunapouza tungkuwa tunauza kwa hekima. Yaani unapouza kwa hekima, unauza kwa mtu atakayeendeleza kile chombo kwa ajili ya kazi ile iliyokuwa imekusudiwa. Kuna faida gani wewe unauza kitu muhimu, halafu unachukua kitu ambacho ni cha hovsky? Ni sawa na vile Marehemu Baba wa Taifa alivyosema kwamba mtu unabdalishana almasi na kioo. Ndiyo mambo tunayofanya yanayoendelea sasa hivi. Tumekuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunarithisha nini kwa watoto wetu hawa kama sisi tabia yetu ni hiyo? Yaani kila mara huwa nashangaa sana. Tunakaa tunafikiria hapa tu! Lakini hatupangi kwa ajili ya miaka 200, 300

inayokuja! Utafikiri tulikoma kuzaa wakati bado tunaendelea kuzaa na tunapaswa turithishe kwa watoto wetu vitu muhimu kama hivyo! Lakini sisi hatufanyi hivyo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba nipate jibu kuhusu hii karakana imefikia wapi na mna mpango gani wa kuishughulikia hiyo karakana irudi kwenye matumizi yake ambayo yalikuwa ni ya maana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nilikuwa naomba nizungumzie suala moja ambalo pia limezungumziwa sana, la upande wa *ATCL* au Uchukuzi wa Anga. Hili suala linatugusa, linatusikitisha, kwa kweli linatudhalilidha kwamba hii Tanzania na ukubwa wake wote huu ambapo hata kama ingekuwa na mfumo wa kuwa na ndege za kusafiri humu ndani tu, bado tungefanya faida, lakini sisi tunashindwa, majirani zetu wanakuja sijui nasikia 540 wanaazana na kandege kamoja mara unakuta wana ndege nyingi, mandege makubwa! Majirani zetu Wakenya wanakuja na ndege moja, sasa hivi wana mindege, wana *system* wanakwenda ulimwenguni kote. Yaani jamani ni aibu! Yaani jamani tunasikitika. (*Makof!*)

Sasa jamani, ebu tujiangalie, tujipeleleze ndani ya mioyo yetu, tusiwe tunaishlia kusema tu hapa. Hata hiyo pia ichunguzwe, wale wote walioanzisha ubovu wawe angalau wanasesmwa na pia wanajulikana, wasiwe watu ma-*gentleman* kumbe ni mafisadi wakubwa. Yaani tunakuaje machoni kama watu, wengine tunawapa heshima kumbe ndiyo hao wahujumu wakubwa. Tupeleleze, tutafute mpaka tuwapate na wenyewe wawajibishwe hata angalau kwa kusemwa, watu wajue kwamba huyu lakini alituhujumu hata

kama ana kitu chake alichochukua anafanya huko, ametuhujumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna suala linalohusiana na urithishaji, *succession plan*. Pale nilikuwa nimekwenda kuzungumza na Marubani wetu vijana wanaosoma muda mfupi tu, wakasema hivi: sisi Marubani tunaotaka kuinukia Watanzania, hatupewi nafasi ya kuweza ku-practice ili tupate *mileage* zetu ambazo zitatu-*qualify* kama Marubani. Watu wa ndio ambao wanapewa nafasi hiyo, sisi hatuthaminiwi pia na Serikali kwa sababu hela ni nyngi za kuweza kupata uzoefu wa kuweza kuendesha hizo ndege na Marubani. Kwa hiyo, ndege sasa hivi inahujumiwa, watu wa *South Africa* na watu wanaofahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niungane na Wabunge wenzangu kuchangia hoja ya Waziri wa Uchukuzi aliyoiwasilisha hapa Bungeni tangu jana. Kwanza, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe pamoja na Mheshimiwa Dkt. Tizeba kwa kukabiliana na changamoto nyngi zilizoko kwenye Wizara yao na napenda kuchua nafasi hii kuwatakia kila la kheri na utendaji mzuri ili Taifa hili la Tanzania liweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili niokoe muda, mimi nitakwenda haraka haraka na moja ya mambo

ambayo nitakayochangia, la kwanza leo, naomba Wizara hii iangalie kwa mapana na kwa kina Chuo cha *Dar es Salaam Marine Institute* kisaidie Taifa letu na hasa kwa watu wa Lindi na Mtwara ambako sasa kuna uvumbuzi mkubwa wa gesi. Chuo hiki kikitumika vizuri, kinaweza kikawafundisha vijana wetu wa Lindi na Mtwara kwenye mambo mbalimbali ya Baharini na hivyo kuweza kusaidia sana kupata ajira kwa watu wale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo vijana wa Mtwara wakiwa wako tu *idle*, wakiwa hawana kazi, wale wanaofanya utafiti wa gesi na mafuta kule hata *mwelders* tu wanatoka nje na siyo maeneo ya Mtwara, kwa nini? Mimi natoa rai, basi kwa Serikali iangalie kwa kina, haja ya kukitumia Chuo hiki kusaidia ili kiweze kutoa ajira na kazi kwa vijana wetu wa Lindi na Mtwara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Lindi na Mtwara tumeachwa muda mrefu. Ziko sababu. Pengine ziko sababu za msingi tu za kiusalamu na nini, basi wakati huu ambapo mambo yale yamekwisha, vijana wale watumike sasa wasiachwe kama walivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili ni suala la Reli ya Mtwara hadi *Mbamba Bay*. Kama nilivyotangulia kusema, gesi iliyovumbuliwa ni nyingi, tafiti zinaendelea kule, lakini makaa ya mawe yaliyoko Mchuchuma na Liganga, *Uranium* iliyoko Namtumbo ingetegemewa sana itumike. Jirani yangu ananiambia chuma cha Liganga. Ingetegemewa sana rasilimali hii itumie Bandari ya Mtwara na namna ya kufika huko,

namna rahisi na nyepesi ni kuwepo kwa Reli. Lakini inaonekana hakuna uamuzi muafaka wa ujenzi wa hii Reli. Kwenye ile miradi ya *Mtwara Corridor* linatajwa sana suala hili la Reli, lakini hatuoni uamuzi, haja na nia ya dhati ya kuanzishwa kwa Reli hii. Mimi nadhani wakati umefika wa kujenga hiyo reli ili rasilimali zilizopo zitumiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko Nangote anajenga kiwanda kikubwa cha saruji kule, wako wawekezaji walioko tayari kujenga kiwanda cha mbolea. Bila kutumia reli haiwezekani. Sambamba na hilo, naishauri Wizara iamue kwa makusudi kuwepo na meli itakayokuwa inaunganisha kati ya Dar es Salaam na Mtwara ili ipunguze uharibifu wa barabara tuliyonayo sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inaendelea vizuri, inaendelea kujengwa, lakini kwa mizigo mikubwa kutumika kwenye barabara itatuharibia na tutaendelea kupata adha tuliyokuwa tunaipata kule nyuma katika muda mfupi tu ujao. Njia mbadala ni kuwa na meli maalum itakayofanya kazi kati ya Mtwara na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Uwanja wa Ndege wa Mtwara, matumizi ya uwanja huo kwa sasa ni makubwa. Ndege zinazotua pale kila siku, ni nyingi, na hata uwekezaji ulioko Mtwara, unalazimisha matumizi makubwa ya Uwanja ule wa Ndege. Naomba Wizara ipandishe hadhi uwanja ule uwe Uwanja wa Kimataifa ili kuendana na hali halisi ya sasa. Aidha, vifaa mbalimbali viwekwe pale, *lounge* ile iwe

kubwa, ipanuliwe, vitendea kazi vingine kama zimamoto na kadhalika viwekwe vinavyofanana na hali ya sasa, lakini pia kuwe na taa zitakazoruhusu kutua kwa ndege hata usiku kwenye uwanja ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja huo tangu mwaka 2010, umekuwa ukifanyiwa ukarabati, lakini umefanyiwa ukarabati duni mno, yaani *sub-standard* kabisa. Ningeshauri, na kwa sababu namfahamu Dkt. Mwakyembe *he is very serious*, hebu aangalie pale, ile inatia aibu. Ukarabati gani ule umefanywa? *Sub-standard* kabisa na tuupokee! Sitafurahishwa na wala sipendezwi na ukarabati uliofanywa pale ni wa kiwango cha chini na duni mno. Hebu angalieni upya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo. Mheshimiwa Murji jana alipokuwa anachangia, alilitaja kidogo kuhusu usiri wa Mamlaka ya Bandari. Mamlaka ya Bandari imekuwa na usiri mwangi kweli kwenye mambo ya uwekezaji yanayohusiana na Bandari ya Mtwara na wanatuletea adha sana kwa wananchi kujibu maswali ambayo yalikuwa siyo ya lazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaambiwa, kule Bandari imeuzwa, wanafanya vikao. Nilipata barua hapa, kikao cha mwisho walichofanya, nilipata barua siku hiyo hiyo na huko ningeendaje? Lakini nafikiri ilifanywa kwa makusudi ili Wabunge wasijue kinachoendelea. Hivi kuna tatizo gani la kuwa wazi? Haya mambo si ya Umma? Haya mambo si kwa manufaa ya Watanzania? Usiri siri ni wa nini? Ili iweje? Mheshimiwa Mwakyembe na Ndugu yangu

Mheshimiwa Tizeba hebu wasimamieni Bandari, wanatutia aibu kulazimika kujibu mambo ambayo wala hayana sababu ya kuyajibu. Maana ukiwa wazi, kila mtu anaelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nimeona kwenye bajeti hapa, uko mpango wa kuifanya Bandari ya Mtwara base maalum kwa ajili ya maendeleo ya Bandari ile. Lakini sioni bajeti, wala palipotengwa fedha, wakati mnasema kuna mpango huo. Sasa tunataka kujenga na nini? Mawe? Wakati anahitimisha Mheshimiwa Waziri hoja yake, ningependa nielezwe mpango huu umetengewa kiasi gani na utachukua muda wa miaka mingapi? Ili tuwe wazi, tulielewe jambo hili kwa uhakika, tunapokutana na wapiga kura wetu, wananchi wetu wa maeneo yale tuwaambie mambo yaliyo ya ukweli na uwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nilikuwa na mchango huo. Ahsante sana na kwa kweli naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Uchukuzi. Nami nianze kwa kutoa pongezi nyingi sana tu kwa Dkt. Harrison Mwakyembe na Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba kwa kukabidhiwa haya majukumu makubwa na mazito. Naamini katika utendaji wao wa kazi, watatusaidia sana katika kuiendeleza hii Sekta ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahjeshimiwa Wabunge wengi wameshachangia, hususan katika maeneo mengi ya msingi kuhusiana na Reli, Bandari na Shirika letu la Ndege na mimi niongeze tu kwa kusema kwamba nyanja hizi zote ni za muhimu sana na tukiweza kuzitumia vizuri na kuziendeleza, zitakuwa tu siyo uti wa mgongo katika nchi yetu, lakini itatusaidia sana kutuongezea biashara katika eneo zima la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mahitaji ya huduma ya Reli kwa upande wa mizigo, tumeona kabisa sasa hivi biashara ya malori ya mizigo inazidi kukua na gharama ya uendeshaji wa huduma hii ni kubwa sana. Tungekuwa na Reli madhubuti, biashara hii yote ingekuwa inaingia katika pato letu la Taifa. Lakini isitoshe bado usafiri wa Reli ya Kati bado mahitaji ni makubwa sana. Nashukuru kuona kwamba katika kitabu ya bajeti kuna mikakati ambayo mnaiweka ili kuongeza safari za reli. Hilo tunataka kuwapongeza na ikiwa mtafanikiwa katika hilo, kwa kweli, tutakuwa tumepiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Shirika la ndege, bado tunahitaji kwa kweli kuliangalia vizuri zaidi. Ni fedha nyingi tumekuwa tunawekeza katika Shirika hili, lakini kwa kweli tunaona kwamba bado ile hali ambayo tungependa kuiona ya ufufukaji wa hili Shirika hajifikia kiwango chake. Sasa nilikuwa napitia kitabu hapa cha bajeti, tuna ndege mbili na nkipiga hesabu za haraka haraka Mheshimiwa Waziri tuna zaidi ya wafanyakazi 200. Hii inamaanisha kwamba ndege moja ina takribani zaidi ya watu 100. Sasa mimi

nadhani pamoja na kuweka fedha katika Shirika la Ndege, lazima tuangalie vile vile mfumo mzima wa uendeshaji wa Shirika hili, lakini vile vile tuuangalie mfumo mzima wa utendaji wa Shirika hili. Pasipo kuwekeza katika kurekebisha mfumo, na pasipo kuungalia utendaji wa Watendaji wa Shirika hili, juhud zote ambazo mtakuwa mnazifanya, hazitakuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, mimi ninadhani kuna umuhimu mkubwa sana Wizara ya Uchukuzi sasa ikaja ikawaeleza Wabunge mikakati ambayo wanayo na mipango mikakati ambayo wanayo ambayo wanataka kuifanya katika ufuufuaji wa reli, bandari na hili Shirika letu la Ndege, ili na sisi tupate fursa ya kutosha ya kuweza kuwasaidia na kuwachangia mawazo ya jinsi gani na nini kiweze kufanywa. Naamini hii itatusaidia sana na sisi kuanza kupata ule mwanga wa nini kinachoendelea. Lakini na sisi kuweza kutoa mchango wetu wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niwapongeze tena Wizara ya Uchukuzi kwa kuanzisha utaratibu wa matumizi ya reli kama sehemu ya kuondoa msongamano wa foleni Mkoa wa Dar es Salaam. Nikiwa kama Mbunge wa Dar es Salaam, naipongeza hatua hii na ninaamini kabisa na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Dar es Salaam wanaafikiana na hilo. Tuko tayari na tutaendelea kutoa ushirikiano kuhakikisha kwamba juhud hizi zinafanikiwa. Ninaamini tukiweza kufanikiwa katika hili, kwa kweli na sisi itatupunguzia sana adha ambazo tunazipata kama wakazi na wananchi wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia vilevile katika Kitabu cha Bajeti hiki, na hususan nilikuwa nataka kulenga katika masuala ya ujenzi wa *Airport*. Naona kwamba, *projects* nyingi sana, hususan katika ukurasa wa 57 pale, kuna *projects* nyingi sana; sasa Waheshimiwa Wabunge wa Mbeya, hapa jana walikuwa wanalamika sana kwamba, Uwanja wa Songwe umechukua miaka takribani 12. Sasa hizi *projects* tunazifanya *in piece notes*, kwa vipande vipande, hivi ni kwanini tusiwekeze kwamba, katika mwaka huu wa fedha, tutakuwa na *project* labda mbili, tatu, tuzifanye kwa ukamilifu, tumalize, tuhamie *project*nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, tunasema tunapokuwa tunaendelea na ukarabati na ukiendelea kukarabati miaka 10, 20, nadhani hata ile *value for money* inakuwa haipo. Kwa hiyo, nilikuwa nataka nitoe ushauri tu kwa wenzetu wa Wizara ya Uchukuzi, walione hilo, tufanye *projects* chache, tuzifanye kwa ukamilifu, tuzimalize ili tuweze kwenda kuhamia katika *project*nyingine.

Mheshjimiwa Mwenyekiti, nilitaka nigosie tena Taasisi nyingine ambayo iko chini ya Wizara hii, na hii ni ya *SUMATRA*. Kwanza, nitoe pole kwa wananchi wa Zanzibar, kwa ajali ya Meli ya *MV. Skagit*. Lakini tutumie fursa hii na sisi kuangalia na kufanya mapitio ya mfumo mzima wa masuala ya usafiri majini; Sheria zake, Usimamizi wake, Taratibu za Uokoaji na vitu vyote na ile *sea worthness* ya vyombo vyote ambavyo vinatumika majini, ili tena matukio kama haya yasiwe yanajirudia katika siku za mbele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikiendelea katika Taasisi hii ya *SUMATRA*, sisi Dar es Salaam tuna matatizo makubwa sana. Mheshimiwa Waziri, ulianza vizuri, lakini sasa hatu hawa watu wa daladala wanasema, hizi nguvu za Mheshimiwa Mwakyembe, ilikuwa ni nguvu ya soda. Tuna matatizo makubwa sana ya ukatishaji wa *route*, mabasi ya daladala na upandishaji wa holela, *especially*, katika muda wa jioni, huwa mabasi ya daladala hawafuati *route* na bei wanapanga jinsi wanavyotaka. Kwangu kule Kigamboni, maeneo ya Chamazi, Tuangoma, Somangila, Kimbiji, tunapata shida sana. Kwa hiyo, naomba sana hili, Mheshimiwa Waziri nalo aliangalie na watu wa *SUMATRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilikuwa nataka kuligusia ni suala la upanuzi wa Bandari. Kimsingi, naunga mkono kabisa suala la upanuzi wa Bandari, na ninasikia eneo langu la Kigamboni, sehemu ya Vijibweni nayo iko katika eneo ambalo litahusika na upanuzi wa Bandari, nasikia. Nasema kwamba, nasikia, kama Mbunge wa eneo.

Nakumbuka Mheshimiwa Waziri, nimekuandikia barua nikiomba nipate kidogo ufanuzi wa nini mnachotaka kukifanya. Nakuomba tu Mheshimiwa Waziri, ili kupata ushiriki mzuri wa Mbunge wa eneo husika na wananchi wa eneo husika kwa sababu, mwisho wa siku mtaishia kwa wananchi. Kama Mbunge halielewi vizuri na wananchi hawalielewi vizuri, inaweza ika-*defeat purpose* nzima ya lengo zuri ambalo mlikuwa mnataka kulifanya. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana baada ya zoezi hili, tuweze kupata hayo

majibu ya msingi ili na sisi kama wakazi wa Kigamboni, tuweze kutoa ushirikiano wa kutosha katika zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kumalizia na suala jingine ambalo linahusu usafiri Dar es Salaam, *UDA*. Tuna Shirika la *UDA* ambalo ni mali ya wananchi wa Dar es Salaam, ambalo tumepewaa taarifa kwamba Shirika hili nalo limeuzwa, tukaambiwa kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuwa inaliangalia suala hili. Sasa hivi ni takribani mwaka mzima, wananchi Wana-Dar es Salaam, wanaulizia hatima ya Shirika hili ni ipi? Wanataka kujua uuzwaji wake ulikuwa halali? Matokeo ya hiyo ripoti ya *CAG* na maamuzi ya Serikali ni yapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba kwa sababu, hili suala tulitarajia kwamba tungekuwa tumeshapata majibu ya kina sasa hivi. Kuendelea kuchelewesha ni kutowatendea haki wananchi wa Dar es Salaam, hata yule mmiliki mpya ambaye mlikuwa mmempa. Tunataka tupate uhakika kama kweli bado ni mali ya wananchi wa Dar es Salaam au kama kweli, mmeshaliiza ili basi tuweze kujua nasi tuwe na uhakika kipi cha kwenda kusema kwa wananchi wa Dar es Salaam. Tulikuwa tunaomba sana katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri, suala hili na sisi tupatiwe tamko la Serikali, kuhusu hatima nzima ya suala la *UDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa hapo, kwa kuchangia hayo. Lakini naendelea kuwapongeza kwa hatua nzuri ambazo wamefikia. Sina shaka kabisa na utendaji wao wa kazi. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi. nianze moja kwa moja katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 21, 22 na 23 wa *speech* ya Mheshimiwa Waziri, anazungumzia mambo haya ya TAZARA. Nasikitika tu kwamba, Shirika ambalo lillianzia mizigo tani milioni tano, sasa ni tani milioni 40; Shirika lililoanzia abiria milioni tatu, mpaka sasa hivi ni 752,000. Halafu wakati huo huo, juzijuzi wamepewa hela Shilingi bilioni 59, lakini ndiyo hizo hizo zilinunuliwa mabehewa ambayo mengine yamekodishwa DRC. Hivi karibuni, mwezi Machi, tayari wamesaini Zambia, Tanzania, China, mkopo mwingine wa Shilingi bilioni 67.2. Sasa na wenzangu wote waliochangia, kuna matatizo TAZARA, sijui hizi fedha zitatumika vilivyo, wakati Shirika lina matatizo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa mimi niseme tu kwamba, aah, mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu. Kwamba, matatizo ya TAZARA ambayo Wabunge wameyalalamikia, hayana tofauti yoyote na matatizo ya Zanzibar. Mwalimu Nyerere na Rais Kaunda, walikuwa na *good faith*, ndio likazaliwa Shirika la Reli TAZARA. Mambo leo yamebadilika. Ni sawasawa na Mwalimu Nyerere na Rais Karume, walipokuwa na *good faith* ya Muungano; sisi tunapolalamika kuhusu Muungano, wenzetu wengine hawafahamu. Juzi Kamati ya Miundombinu tulipokwenda, Watanzania ndio wanalamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti ni moja tu, Zanzibar kijinchi kidogo, Tanzania Bara ni kubwa, wanaolalamika wadogo. Lakini huku kwa *TAZARA*, Tanzania kubwa, *TAZARA* ndogo, inayolalamikiwa huyu mkubwa; yatatuliwe matatizo yaliyopo, na ni matatizo ya Marais wawili na Mawaziri wanaohusika. Vinginevyo, tutalaumiana bure. Walikuwa na *good faith*, lakini mambo yamebadilika. Hilo limekwisha, pesa zilizokopwa Shilingi bilioni 67.2 zisije zikaharibika, mabehewa mengine yakaenda *DRC*. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ukurawa wa 75 aya ya 72, Mheshimiwa Waziri amezungumzia miradi mbalimbali itakayokuwa chini ya usimamizi wa bandari. Katika miradi hiyo, kuna mkopo wa Shilingi bilioni 482.4 ambazo Tanzania, asilimia 19 ni Shilingi bilioni 94, zitatokana na Mamlaka ya Bandari. Sasa Mheshimiwa Waziri atufafanulie, hizi Shilingi bilioni 387 ambazo alisema ni kwa Wahisani, kwa mikopo na wawekezaji katika taarifa, sisi kama Bunge na Kamati inayohusika, ili kuweza kufanya kazi ya *oversight*, kuliweka jambo hivi tu, zilizobakia Shilingi bilioni 387 zitapatikana kwa hisani, mikopo na uwekezaji, bila ya kufafanua? Halikai vizuri. Ukija hapa utueleze, Wahisani kiasi gani? Ni nani? Mikopo kiasi gani? Kutoka nchi gani? Wapi? Benki gani? Wawekezaji ni akina nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuliacha tu hivi hivi au kama ndiyo hiyo *Ophir*, *BG* na *Statoil*, *Petrobras*, ndio wawekezaji wenyewe, basi utueleze. Lakini ikikaa hivi hivi, haipendezi. Wewe ni Mtaalamu hata wa Kiswahili na mambo mengi sana. Wataalamu wako

wasituwekee wekee watu hivi hivi bila ufanuzi. Tuweze kutajiwa vizuri tuweze kufanya kazi yetu ya *oversight. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, utanisamehe kwa sauti eeh, kuna hiki kitu *SUMATRA*. *SUMATRA*, tunaambiwa wamekagua, ukaguzi uliofanyika wamekagua kaguzi 186 kwa mwaka huu, ukilinganisha na mwaka 2011 ni kaguzi 118. Halafu hapa tumetajiwa, kuna meli nne zilikutwa na kasoro na zikasimamishwa; zimeachwa hivi hivi, hatuzijui. Mheshimiwa Waziri atutajie akija hapa, meli nne zipi zilizosimamishwa? Eeh! Zimesimamishwa kwa muda gani? Milele hazitafanya kazi tena? Au zitafanya kazi? Kuacha hivi hivi pia siyo vizuri, wajanja pengine hizo hizo meli zilizosimamishwa, keshokutwa wajanja wanatembeza meli hizo na ajali ndiyo kama hizo. Mheshimiwa ukija hapa, utueleze ni zipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la *MRCC*, Kituo cha Utafutaji na Uokoaji kilichoko Dar es Salaam. Mheshimiwa Waziri, kwanza mimi nataka atueleze hiki Kituo ni cha Muungano au ni cha Tanzania Bara tu? Kwa sababu, sote tunaelewa Bandari ni jambo la Muungano. Liko katika nyongeza ya kwanza toka mwaka 1964, lakini Bandari hajakwenda Kimuungano hata siku moja! Kila mtu kivyake! Sasa hiki Kituo tena kilichoko Dar es Salaam cha Utafutaji na Uokoaji, hebu Mheshimiwa Waziri atuambie kimeanza lini? Kwa Sheria gani? Iliyopitishwa na Bunge lipi? Mamlaka yake ikoje? Kama ni cha Muungano, aje utufafanulie. Kweli kina sura ya Muungano hiki? Menejimenti yake na mambo yote, kina sura ya Muungano au tunatajiwa tu? Mimi ni

mara yangu ya kwanza kukisikia hiki. *Funding* yake iko vipi? Kuliacha hivi hivi, haipendezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kituo hiki kipo, *MV. Skagit* ilipozama hivi karibuni, mbona hatukuwaona? Tuliona *Helicopter* tu iliyokwenda mwishoni. Tukio lilitokea saa 5.00, kama kipo Kituo hiki, kazi yake ni uokoaji na utafutaji, kwa nini hatukukiona mpaka saa 10.30? Vyombo vilivyoonekana ni vya Zanzibar na *Helicopter* ya Jeshi tu, halafu tunaambiwa kuna Kituo kama hiki! Naomba Mheshimiwa Waziri akija, atufafanulie, tusiambiwe maneno juu juu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri, katika ukurasa wa 59, 60, 61, 68 amezungumzia mambo ya anga na ndege. Katika suala hili amezungumzia usalama wa ndege, mambo ya abiria na mambo ya viwanja. Lakini hapa nina jambo moja leo nataka Mheshimiwa Waziri, anipatie jibu. Kama Waziri wa Uchukuzi hana jibu, bahati nzuri Mheshimiwa Membe leo yupo, nimemwona na Waziri mwenzie wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kama Waziri wa Uchukuzi hana jibu la suala hili, basi Mheshimiwa Membe, siku ya kuwasilisha, atupatie jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinaitwa *Airline Insectside*. Kitu hiki kimekuwa *packed* katika kijichupa, wanaita *Servo Pack*. Ndege, hasa hizi za *South African Airlines*, zikiondoka Dar es Salaam, lazima ipulizwe na kile kijichupa, bahati nzuri mimi nimefanya ujanja nikakipata kwa kukiazima, kimeandikwa *Avoid Excessive Inhale*, usivute sana. Lakini ndege hizi, nimeshuhudia ikitoka Tanzania, ndiyo inapulizwa hiyo

*insectside*; ilipotoka *Mozambique* pia nimepeleleza inapulizwa, lakini ikitoka Namibia hakipulizwi kidawa hicho; ikitoka Botswana, haipulizwi. Hivi sisi Tanzania, kwenye hewa chafu na *Mozambique*, tuna matatizo gani kama kinafuata Sheria za Kimataifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu naambiwa hiki kimetengenezwa kwa *Act Number 36* ya Mwaka 1947. Sasa hebu tuelezwe, ni nini? Kuna ndege inaonekana maalum kwamba, kipulizwe kwenye ndege za *A300*, 707 kwa 747, 727, 737, lakini kwa nini kuwe na ubaguzi? Naomba tupatiwe jibu la suala hili. Nyote mnasafiri, mnayashuhudia hayo, ni ubaguzi wa hali ya juu. Sasa hivi ndiyo tuna hiyo *SADC*, kama *within SADC* kuna ubaguzi wa namna hii, nini tunachokifanya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala ambalo ni mtambuka, Mawaziri wawili hawa, mmojawapo atupatie jibu kinagaubaga na atuambie hiyo Sheria ya mwaka 1947, *Act* ya 36, kweli, ilikuwa na maana kama hiyo ya ubaguzi wa namna hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya kifua, sijui lakini ngoja nije na jipya. Ajali. Katika ukurasa wa 49, Mheshimiwa Waziri alizungumzia kwamba, kuna idadi ya ajali 15 zilizoripotiwa na watu 581 waliokolewa na watu 17, kupoteza maisha.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hii ripoti ilikusudiwa kwa Tanzania nzima au Tanzania Bara tu? Maana kama kwa Tanzania nzima, hizi takwimu siyo sahihi hata kidogo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nimemaliza muda?

**MWENYEKITI:** Ndiyo, umemaliza.

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, nakushukuru hivyo hivyo. Siyo haba! Hayo siyo kidogo. Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye mjadala wa Wizara ya Uchukuzi. Sasa naomba nianze kwa kusema kitu ambacho nimeona ni cha ajabu kidogo katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Mwalimu wangu, Dkt. Mwakyembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba, moja ya majukumu ya Wizara yake na Taasisi zake ni pamoja na kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vyia usafiri majini. Amelieleza pia Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yake imeendelea kutekeleza majukumu mbalimbali ya usalama, ulinzi na uhifadhi wa mazingira majini. Lakini kitu cha ajabu ni kwamba, katika maelezo yote ya Wizara, katika hotuba yote ya Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, hakuna mahali hata pamoja ambapo Mheshimiwa Waziri ametaja ajali mbili ambazo

zimetokea katika kipindi cha chini ya mwaka mmoja uliopita. Ajali ambazo kwa ghamama ya maisha ya Watanzania zinapitwa tu na ajali ya *MV. Bukoba*, ya mwaka 1996, ajali ya *MV. Spice Islander* na *MV. Skagit*, ya juzi, hazijatajwa kabisa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hicho tu, kwa sababu kumekuwa na utamaduni hapa, kila anayesimama anatoa pole kwa waliofiwa na ndugu zao, hotuba nzima ya Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, siyo tu haitaji *MV. Skagit* na *MV Spice Islander*, vilevile hakuna hata hiyo pole ambayo imekuwa *Customary* kwenye hili Bunge. Hotuba nzima!

Sasa sitaki kumhukumu Mwalimu wangu, inawezekana amepitiwa tu, lakini suala la kutokutaja hizi ajali mbili kubwa wakati ametaja ajali za barabarani, ajali za ndege ambayo haikuwa imeharibika kabisa kwa kweli kutokutaja hizi ajali mbili, kunahitaji maelezo ya Mheshimiwa Waziri, na nitaomba asiache kueleza kwanini hiki kitu kikubwa kilichotokea ndani ya mwaka huu, hakipo katika hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, kwa sababu ya kutokutaja hizi ajali mbili kubwa hata takwimu ambazo amezitumia Mheshimiwa Waziri siyo sahihi. Watanzania zaidi ya mia ngapi wanakaribia 1,000 wamekuwepo kwa ajali mbili, siyo hawa tisa wanaozungumzwa. Waliokufa ni Watanzania na hii ya juzi tunaambiwa kuna raia wa kigeni. Bunge hili linahitaji kupewa taarifa sahihi, hii hotuba inaonyesha hakukuwa...

## **TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Rajab.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni zetu, naomba nitoe taarifa kwa msemaji anayezungumza.

**MWENYEKITI:** Kanuni namba ngapi?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Kanuni namba 68(8), taarifa hii inahusiana na maelezo ambayo msemaji alikuwa anayazungumza hapa kwamba Mheshimiwa Waziri hakutoa pole wala hakuonyesha majozi yake kwa meli zilizozama Zanzibar juzi. Nataka asome katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa tatu kifungu cha sita. Mheshimiwa Waziri anasema: "Naungana na Wabunge wenzangu kwa majonzi makubwa katika kutoa pole kwa viongozi wa Taifa letu na wananchi wote kwa ujumla kwa msiba mkubwa uliolisibu Taifa kutokana na ajali ya MV. Skagit iliyotokea karibu na Kisiwa cha Chumbe." Kwa hiyo, naomba nitoe taarifa hiyo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu Mheshimiwa Tundu. Hiyo ni taarifa kwa sababu kwa kweli nadhani nikiifuatilia hapa na mimi naona kabisa kwamba siyo kweli. Anakupa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kweli kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri ametoa pole tena kwa maneno mazito sana pale katika ukurasa wa tatu, kifungu kile cha sita. Kwa hiyo, hiyo ni taarifa kwako. Mheshimiwa Tundu unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Mheshimiwa kwa kuipokea.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Naomba nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kunikumbusha hili, wala si kitu cha fedheha.

**MWENYEKITI:** Sawa naomba uendelee.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Naomba niendelee, isipokuwa wakati pole inatolewa, pole kutokana na vifo vya watu waliokufa kwenye MV. Skagit ni wangapi waliokufa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Wametajwa wapi?

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, natumia kanuni ya 64. "Bila ya kuathiri masharti ya lbara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Lissu amekiri kwamba alipitiwa na hapa tunatengeneza

kumbukumbu za miaka nenda rudi, nilikuwa naomba ayafute yale maneno yasije yakaingia kwenye *Hansard* kwamba Mheshimiwa Waziri hakutoa pole kwa wananchi waliokufa kwa meli.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu, nadhani kwa kuwa Mheshimiwa Tundu Lissu alishakubali, kwa vyovyote vile niwaombe tu watu wa *Hansard* kwamba waondoe tu ile kauli ya Mheshimiwa Tundu Lissu ili tusipoteze muda hapa aweze kuendelea. (*Makofii*)

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naona sijui kuna vitu gani vinaendelea!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema kwamba pole imetolewa, lakini waliokufa kwenye hizi ajali ni wangapi? Kwanini taarifa ya vifo hivyo hazipo? Hiyo ndiyo ilikuwa hoja yangu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema kuhusiana na ajali mbili, inafahamika na imeshasemwa huku Bungeni kwamba hizi meli mbili siyo tu zilikuwa zinasafiri katika Bandari za Unguja, zilikuwa zinapakia abira na mizigo katika Bandari za Tanzania Bara vilevile, na kwa sababu hiyo tu, pamoja na kwamba masuala ya usafiri wa majini siyo masuala ya Muungano kwa sababu ya kupakia abiria kwenye Bandari za Bara, *SUMATRA* kama chombo chenye mamlaka ya kudhibiti usafiri wa majini na nchi kavu, ilikuwa na mamlaka ya kukagua hizi meli mbili zilizosababisha maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu, nataka kujua kwa Mheshimiwa Waziri: Je, *SUMATRA* iliwahi kufanya ukaguzi wa hizi meli mbili? Pili, kama jibu ni ndiyo, ukaguzi huu ulifanyika lini na matokeo ya ukaguzi yalikuwa yepi? Hayo maswali ni muhimu kwa sababu hiyo niliyoisema kwamba siyo tu kwamba zilikuwa zina-*ply route* za Unguja na Pemba lakini vilevile zilikuwa zina-*ply route* za Dar es Salaam na Bandari nyingine za Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie usafiri wa reli, na reli imezungumzwa sana. Naomba niseme kwamba katika *system* ya Reli ya Kati, reli ya kati Naibu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani jana alisema inapitia Singida kidogo tu. Naomba nikumbushe Bunge lako kwamba Reli ya Kati siyo tu kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma na Mwanza, lakini vilevile ni kutoka Manyoni kwenda Singida. Hiyo njia iliyojengwa na mafundi wetu wa *TRC* miaka ya tisini na ikaanza kutoa huduma mpaka mwaka 2009 huduma zilipositishwa, na Mheshimiwa Waziri anasema kwamba huduma za reli ya Dodoma mpaka Singida Mjini zilisitishwa kwa sababu ya ukosefu wa injini na mabehewa. Kwenye hotuba yake amesema hivyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema katika mwaka huu fedha zimetengwa Shilingi bilioni 104 kwa ajili ya *ku-re-manufacture engine* za zamani kununua *engine* mpya, kukarabati mabehewa ya zamani na kununua mabehewa mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua katika hizi Shilingi bilioni 104 za kufanya hivi vitu nilivyovisema: Je, Reli ya kutoka Manyoni mpaka Singida Mjini nayo itapatiwa mabehewa na injini ili huduma zake zirudi kama ilivyokuwa? Kama jibu ni hapana, nitaomba Mheshimiwa Waziri atueleze, kwanini haya? Kwa sababu kama sababu ni injini na mabehewa hakuna, na kuna mpango wa kununua, basi tuambiwe, kwanini reli hii ya Manyoni Singida haipo katika mpango wa injini mpya pamoja na mabehewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swal i la mwisho linahusu uwekezaji katika reli. Nchi hii tangu uhuru tumewekeza sana katika barabara, na ukweli wa Mungu ni kwamba katika miaka 15 iliyopita Serikali yetu imewekeza sana katika ujenzi wa barabara mpya za lami. Hilo ni jambo zuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hatujawahi kuwekeza katika ujenzi wa reli mpya tangu uhuru ukiachia reli ya TAZARA iliyojengwa na Wachina, ukiachia vilevile ukarabati wa reli ya Manyoni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Ni ya kwanza Mheshimiwa Mwenyekiti? (*Kicheko*)

Acheni roho mbaya. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mimi ndiyo Kiongozi wa meza endelea.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujawekeza katika ujenzi wa reli mpya, na nadhani sitakosea, mimi sio injinia wa mambo haya, lakini nadhani sitakosea. Uchumi wa kisasa na uchumi wa kiviwanda hauwezekani bila kuwa na *infrastructure* ya reli. Nchi zote ambazo zimeendelea, kitu cha kwanza utakachoki-*note* ukienda mahali popote ambapo kuna uchumi wa kisasa wa kiviwanda ni mfumo wa reli. Hatujawekeza katika mfumo wa reli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesema, ukilinganisha uwekezaji wetu katika barabara, naomba kujua na pengine itanufaisha Bunge lako Tukufu, gharama za ujenzi wa reli kwa kilomita ukilinganisha na gharama za ujenzi wa barabara kwa kilomita, ni kiasi gani, ili Bunge lako Tukufu liweze kuona kama hii *emphasis on road construction* imekuwa inatokana na urahisi wa gharama za ujenzi wa barabara *vis-a-vis* ujenzi wa reli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo limezungumzwa sana vile vile, ni suala la usafiri wa majini katika *in land water ways*, katika maziwa yetu. Ni fedheha kwa Taifa letu kuendelea kutumia meli iliyioletwa wakati wa utawala wa kikoloni wa Kijerumani. Itakuwa vizuri Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, aeleze kama kuna sera au kuna mkakati wa kuboresha kufanya *our*

*shipping* katika *in land water ways*, katika maziwa yetu, iwe ya kisasa ili kuendana na hii karne ya 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu yalikuwa hayo na nakushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa ya kuzungumza. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushuruku sana Mheshimiwa Tundu Lissu kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, nilisema nitamwita Mheshimiwa Dkt. Pudensiana Kikwembe na atafuatiwa na Mheshimiwa Steven Ngonyani na Mheshimiwa Barwany ajiandae.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii. Kwanza napenda nianze kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe na Mheshimiwa Dkt. Tizeba kwa mipango yao mizuri waliyoionyesha ili kuweza kuwasaidia wananchi katika kutatua matatizo yao yanayowakabili hasa katika Sekta ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nianze suala la ukatishaji tiketi. Kumekuwa na malalamiko makubwa sana kwa wananchi hasa Kituo cha Mpanda Dar es Salaam na sehemu nyingine kama Kigoma, Tabora na Mwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakatisha tiketi wamekuwa wakiwalangua wananchi tiketi bila sababu za msingi. Tiketi hizo zimekuwa zikikatwa siku hiyo hiyo

ya safari. Kwa mfano, mtu anatoka Mamba au Karema anakuja Mpanda Mjini siku hiyo yeye kule ataondoka saa moja afike siku ya treni ambako pale Mpanda Mjini atafika saa 5.00 au saa 6.00. Treni inafika saa 7.00, tiketi zinaanza kukatwa saa 1.30 asubuhi. Je, mtu huyu anaweza akapata tiketi kweli? Matokeo yake sasa huyo abiria atalazimika kulala pale stesheni kwa sababu amekosa tiketi ya siku hiyo, na pale hakuna choo, hakuna nyumba ya wageni, hakuna sehemu ya chakula, atashinda pale, atakula kwa mama ntilie, na atahangaika pale na watoto mpaka siku ya tatu ambako treni itakuja tena. Kwa kweli kitendo hiki ni cha kusikitisha na ninaomba Wizara iangalie utaratibu mpya wa kukatisha tiketi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini juu ya hilo, pia kuna ukatishaji wa tiketi kwa mfano, mtu anatoka Dar es Salaam anakwenda Mpanda au anakwenda Mwanza, au Kigoma - Mwanza na Kigoma kutoka Dar es Salaam, ni tofauti kidogo kwa sababu wao wanaunganishiwa mabehewa, yaani abiria anakata behewa lile atakalopanda kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza hatabadilisha behewa. Kwa Mpanda iko tofauti. Watafika pale Tabora, watakatishwa tiketi kutoka Dar es Salaam mpaka Tabora, afike Tabora pale aambiwe apange tena foleni upya akate tiketi ya kutokea Tabora kwenda Mpanda. Kwa kweli hilo kwa wananchi wa Mpanda linawakera sana na wanasikitika sana, kwani wamekuwa wakiumizwa kwa muda mrefu bila suluhu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kupitia Wizara hii iangalie utaratibu kukatisha tiketi Dar es

Salaam moja kwa moja mpaka Mpanda kwa madaraja yote, kuanzia daraja la tatu, la pili na la kwanza ili wananchi hawa wasipate taabu tena kufika Tabora, aanze kushusha mizigo, aanze tena kupanga foleni. Kwa kweli pale wanafika jioni. Ukifika jioni pale ofisi zimeshakata tiketi, ina maana pia pale watalala, na kwa ushahidi, nenda pale Tabora hata kesho utakuta abiria wamelala pale stesheni. Sio wote wana hela ya kwenda kulala kwenye *guest house* na wala sio wote wana hela ya kusema kwamba watabeba kwa ajili ya kununua chakula au kuishi pale Tabora kwa siku tatu, nne. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tunamwongezea mwananchi wa kawaida gharama ambazo hazina msingi. Naomba Serikali, hili iliangalie. Siyo hivyo tu, kukata tiketi moja kwa moja ni rahisi zaidi kuliko ukikata tiketi ya vipande vipande. Kwa hiyo, naomba hilo katika majumuisho waweze kulielezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika aya ya 22 na 23 page 12 na 13. Katika aya hizi, kwanza Mheshimiwa Waziri anaongelea suala la kukarabati injini 20 ambazo zinafanya kazi, ambazo zimekuwa na teknolojia iliyopitwa na wakati, na amekiri kwamba karibu viwanda hivyo vyote vinavyotengeneza treni, zimeingia kwenye teknolojia mpya ama viwanda havipo kabisa. Lakini katika aya ya 23 ameongelea suala la kuboresha utendaji wa *TRA*, kwa maana kwamba kuna Shilingi bilioni 104 zimetengwa kwa ajili ya kukarabati ku-*re-manufacture engine* nane za treni aina ya 88XX kufanya malipo ya awali ya ununuzi wa injini za treni

mpya 13. Malipo ya awali ya ununuzi wa mabehewa mapya ya abiria 22 na kukarabati mabehewa mabovu ya mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kwamba huku amekiri kwamba hiyo teknolojia haipo na viwanda si ajabu havipo, lakini huku kuna ununuzi wa mabehewa na injini mpya. Sasa hofu yangu hapa inakuja: Je, hizo *engine* mpya na hayo mabehewa yatakuwa ni ya mfumo wa hizi behewa zetu tulizonazo na hizi reli tulizonazo, ama ni katika hiyo *standard gauge* wanayosema itakayokuwa inatakiwa kukarabatiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika aya ya 31, ukurasa wa 19 Mheshimiwa Waziri ameongelea suala kwamba katika mwaka 2011/2012 Wizara iliendelea na juhudzi za kuimarisha njia ya reli, kati ya Kaliua na Mpanda, na inaonyesha kabisa kwamba hizi shughuli zilikuwa zinaendelea kufanywa, na kadhalika. Lakini katika hotuba hii sijaona mahali ambapo ameeleza kwamba hii shughuli inaendelea kufanyika ama ilikwishafanyika ama imesisitishwa ama ni vipi.

Kwa hiyo, katika majumuisho yake, napenda sana Mheshimiwa Waziri awaelimishe wananchi wa njia hii hususan kutoka Tabora mpaka Mpanda na siyo tu ukarabati wa kuanzia Kaliua mpaka Mpanda, hapana, tunataka ukarabati uanzie kule kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mfutakamba, kuanzia Igala, kuja mpaka Urambo; Kaliua mpaka Tabora, ile njia yote ni mbovu, ukipanda treni inarukaruka kama umepanda lori, ni vumbi, mabehewa yake ni machafu, kuna panya wale

wakubwa, mende, yaani ukiwa daraja la pili huwezi kulala, unaongopa kudondoka kutoka kwenye kitanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ile njia ifanyiwe ukarabati na siyo vipande vidogo vidogo, kwa sababu mnaelewa kwamba ule ni ukanda ni wa mvua, na udongo wake ni mlaini. Kwa hiyo, tunaomba sana hii reli ikarabatiwe na ikarabatiwe ipasavyo na ipitike vizuri. Ikiwezekana siyo tu tena kwa ile mara mbili kwa wiki, tunataka *at least* mara nne, watu wanatoka Sumbawanga wanatoka Kigoma, Karema, Kasanga wote wanataka kutumia ile reli, wanatoka Inyonga wanataka kutumia ile reli. Kwa hiyo, tusiwape watu taabu kwa sababu tu ya kusema kwamba bajeti ni ndogo. Ndiyo maana naungana na Mheshimiwa Serukamba aliyesema kwamba ifanyiwe mikakati ya kutafuta *special fund* kwa ajili ya kukarabati miundo hii ya reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda pia niongelee suala la ndege. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wote waliotangulia kuchangia katika sekta ya anga. Kwa kweli ni aibu, ifike mahali Tanzania sasa tuondokane na hii aibu. Waheshimiwa Wabunge, mmekuwa mkisafiri kwenda nchi za nje, mnaona jinsi gani Ethiopia inavyotegemea ndege katika kuongeza mapato yake ya nchi. Sasa tufike mahali hata ndege moja basi ya kuanzia tununue mpya. Hii biashara ya kukodi ndege kutoka Nigeria au Afrika Kusini na Mikataba yenyewe haijulikani ya ukodishwaji kwa kweli tuikomeshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Stephen Ngonyani atafuatiwa na Mheshimiwa Barwany.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwanza nianze kwa kuwapa pole wote waliopatwa na msiba katika ajali ya meli iliyotokea.

Pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniletea Mkuu wa Wilaya katika Wilaya yangu ambaye ni Ndugu Gambo, anafanya kazi za dhati zinazohusiana na maendeleo katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa mpango mzima ambao umeonyeshwa kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, nimeona haya ni maendeleo makubwa. Lakini ninachoomba sana, nimeona kumeongeleta sana katikati lakini eneo lingine hili linalohusu upande wa pembezoni hasa bandari ya Mwambani ingesaidia sana kupunguza kero za wananchi ambao wanafanya biashara nzito za usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya bandari ya Mwambani mpaka sasa hivi hatuambiwi itaanza kujengwa lini. Kwani toka enzi ya Mheshimiwa Nundu mpaka leo ni Mwambani, Mwambani, Mwambani. Naomba Serikali ituambie sasa, kwamba hii bandari ikifika mwaka fulani itakuwa imekamilika na watu watakuwa wanatoa mizigo yao. Inakuwa ni aibu watu

wa Zambia waende wakatoe mizigo Afrika Kusini wakati tuna Bandari kubwa zenyе uwezo wa kufanya kazi na zenyе uwezo wa kuleta maendeleo katika nchi yetu, lakini kwa sababu ya baadhi ya watu wachache tu wanatusababishia watu wanakimbia bandari zetu. Kwa hii hali, kwa kweli kama Mbunge, sitakubaliana nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Uchukuzi ni Wizara nyeti sana na inahitaji watu makini sana, na safari hii wamepata watu makini sana. Lakini mnapozungumzia masuala ya reli mzungumzie reli ya kutoka Tanga kwenda Moshi - Arusha mpaka Musoma. Zitakapokarabatiwa hizi reli, barabara ambazo Mheshimiwa Magufuli kila siku anabomoa nyumba za watu, zitaacha kubomolewa kwa ajili ya kupanua barabara. Kila siku barabara zinabomolewa kwa sababu ya kuharibika kwa barabara na kuharibika kwa barabara ni kwa sababu barabara zinabeba mizigo mizito inayoshindana na barabara.

Sasa kama reli ya Tanga mpaka Arusha ingekuwa imetengenezwa, sidhani kama kuna malori yangepita kwenye barabara zinazopita mabasi. Sana sana yangekuwa yanapita magari madogo, na magari haya ni pamoja na mabasi na mabasi hayawezi kuharibu barabara. Mheshimiwa Waziri, yuko makini sana ndugu zangu, naomba suala hili aliwekee maanani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumzia bajeti ya mwaka uliopita kwamba kuna bajeti ya kujenga bandari ya nchi kavu Korogwe, lakini hili suala

limekuwa ni la mdomoni tu. Naomba mniambie Serikali imefikia wapi? Kati ya mambo ambayo mlikuwa mmeyapanga na mambo ambayo Serikali ilikuwa imetumia gharama kubwa kwenda kuangalia eneo la bandari ya nchi kavu Korogwe mlikwenda kuangalia lakini leo nataka mtuambie, Serikali ije izungumze rasmi kwamba bandari ya nchi kavu Korogwe itafanya kazi lini na itaanza kutengenezwa lini? Lakini bandari ya nchi kavu haizungumzwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti wenzangu wamezungumza sana na ninapenda niwashukuru sana kwa sababu Wabunge wote waliochangia wamechangia kwa dhati na kati ya mambo waliyochangia ni yale ambayo nilitaka kuyarudia. Lakini kitu kingine cha nyongeza nilichokuwa nakiomba ni masuala ya viwanja vya ndege. Viwanja vya Ndege msiviangalie vikubwa tu, kuna Kiwanja cha Tanga kinafanya kazi, Kiwanja cha Mombo ambacho Viongozi wa ngazi za kitaifa wanashuka pale, kuna Kiwanja cha Same watalii wanashuka.

### **MBUNGE FULANI: Cha Nzega!**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Kuna Kiwanja cha Nzega, watalii wanashuka kwa ajili ya kwenda kununua dhahabu, kuna Kiwanja cha Moshi Mjini na kadhalika, lakini mbona hatuvioni hapa? Kwani hivi siyo viwanja? Au mnataka tu vyenye lami? Hata vyenye vumbi pia ni viwanja. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapomaliza mchakato wake anipe majibu ya hivi viwanja, vimetengewa kiasi gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuzungumza sana, kwani wenzangu wamezungumza vya kutosha, ila tu nataka niwapongeze baadhi ya Mawaziri hasa Mheshimiwa Kitwanga, nilikupeleka kwenye Jimbo langu lakini leo hii nina mawasiliiano eneo la Bungu na ninaomba vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwani nilikuwa nimelia kilio cha Mkonge lakini leo wananchi wangu waliokuwa hawalipwi haki zao sasa hivi wanalipwa kwa sababu wenzangu wamechangia kwa dhati. Naipongeza sana Serikali na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongea sana haitapendeza, lakini tu haya machache niliyozungumza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stephen Ngonyani kwa mchango wako. Atafutia Mheshimiwa Salum Barwany na Mheshimiwa Anna Marystella Mallac naye ajiandae.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nakushukuru. Lakini kabla ya yote kwanza nitoe shukrani kwa nafasi hii muhimu ambayo umenipa mchana huu wa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza katika hoja ambazo mara zote huwa nazungumza ndani ya Bunge hili kuhusu suala la mgawanyo wa raslimali katika nchi, ni suala muhimu na suala ambalo linaweza

likatuunganisha Watanzania katika kuendeleza umoja wetu kwa ajili ya maendeleo yetu. Lakini hadhari hii huwa tunaitoa mara zote, lakini Serikali bado haijawa tayari kuona ni namna gani tunaweza tukajenga umoja wetu, tukajenga nchi moja na tukagawana raslimali hii chache tuliyonayo kwa maslahi ya nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili kwa sababu, bajeti zote ambazo zinakuja katika Bunge hili bado kila Mbunge akisimama anakuwa na malalamiko, eneo fulani hatutendewi haki, eneo lile hatutendewi haki na kadhalika. Mimi naamini kabisa kwamba labda hatuna *formula* maalum ya kugawana raslimali katika nchi hii. Ni baadhi ya watu tu wanakaa katika meza na kupanga taratibu za kugawana raslimali hii bila kuzingatia uwiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii haijazungumza lolote juu ya maendeleo ya Mikoa ya Kusini hasa katika maeneo ya bandari, maeneo ya Viwanja vya Ndege na maeneo ya reli. Hii inatupa mashaka.

Juzi tu katika Wizara ya Nishati na Madini tulikuwa na mgogoro katika suala la gesi. Tuliridhia kwa namna nyingine kwamba haya Serikali inaendelea vizuri, lakini kwa kauli hii na bajeti hii, inaendelea kutukatisha tamaa. Inaendelea kutukatisha tamaa kabisa! Inaonyesha dhahiri kabisa kwamba, Mikoa ya Lindi na Mtwara bado hakuna mkakati wa makusudi wa kuitoa mahali ilipo kwenda katika maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Lindi na Mtwara tuna masikitiko makubwa na tunakatishwa tamaa na Serikali iliyopo madarakani sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaleta migogoro ya kisiasa. Mara nyingi katika nchi nyingi duniani, maeneo yanaonekana hayatendewi haki, migororo ya kisiasa inaibuka, inatupa fikra mpya kwamba: Je, tunaweza kuendelea katika mfumo huu? Kwa muda gani? Hili natahadharisha mara zote kwamba iwe agenda muhimu kwa Serikali kuona kwamba haya manung'uniko yanaondoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri aliyetangulia kabla ya Mheshimiwa Mwakyembe amekuja Lindi zaidi ya mara tatu, yaani Mheshimiwa Mfutakamba na akakutana na wananchi wa Lindi na kuzungumza juu ya ujenzi wa Bandari ya Lindi. Tumezungumza hapa na nikataka anieleze juu ya maendeleo ya ujenzi wa Bandari ya Lindi ukoje kwa sasa. Amekuja mara tatu akitoa matumaini makubwa kwa wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara kwamba Serikali sasa itahakikisha kwamba Bandari ya Lindi inafanya kazi. Akasema, Mkandarasi mwelekezi ameshatoa maelekezo yake kwamba tutakwenda mita nne chini na tutakwenda mita 100 mbele ili kuiboresha Bandari ya Lindi. Lakini katika bajeti ya sasa, haionyeshi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aieleze Lindi, aeleze maeneo ya Mikoa ya Kusini ina mkakati gani juu ya ujenzi wa bandari zao? Tuna ushahidi wa kutosha, wa kutosha

kabisa! Mnazungumza habari ya reli hapa, tulikuwa na reli sisi kutoka Nachingwea kwenda Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wazungu Wakoloni waliweza kujua umuhimu wa reli, Serikali iliondoa reli ile kutoka Nachingwea. Kulikuwa na mashamba ya Mkonge kukajengwa bandari mwaka 1950 Mtwara, wakati Lindi kulikuwa na bandari kwa sababu kulikuwa na umuhimu wa kuweka vitu hivi. Wakokoni walijua hivyo, lakini Serikali yetu inashindwa kuona umuhimu huo. Kuna nini hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatukatisha tamaa! Mnataka tufikirie vingine, mnatulazimisha watu wa Mikoa ya Kusini tufikirie zaidi ya hapa tulipo leo na hili tunaweza. Raslimali za Kusini tulizokuwanzo zinaweza kutufanya tuwe nchi sisi tukaendesha mambo yetu. Inawezekana kabisa! Inawezeka! Kwani tuna gesi, tuna bandari na ardhi nzuri yenyе rutuba, kwa nini mnatufikisha hapa? Naitahadharisha Serikali tena, naitahadharisha kwa makusudi kwamba mnatufanya tufikirie zaidi ya hapa, na imeshatokea katika nchi nyingi duniani katika hali kama hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Kiwanja cha Ndege Lindi ambacho ni kizuri zenye sifa zote, Kiwanja cha Ndege cha Lindi kina *six runners*, ni Uwanja wa Kimataifa. Kabla ya Uhuru kulikuwa kunatoka ndege Cairo Misri *transit* Lindi kwenda Johannesburg Afrika Kusini, lakini leo Kiwanja cha Ndege cha Lindi kinafugia ng'ombe, ni machungani kwa kufugia ng'ombe, na Serikali imekitelekeza, na katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri haipo taarifa yoyote inayohusu

habari ya Lindi. Kuna nini hapo? Wakoloni walijua umuhimu wa vitu hivi, lakini tunaangalia ni namna gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi inawafikisha Watanzania hasa watu wa maeneo ya Kusini kwamba pamoja na uwezo wetu wa mchango mkubwa katika Taifa hili, sisi tunaamini kabisa kwamba mchango wetu ni mkubwa, hakuna sababu ya kutokuingalia upya Mikoa ile. Hivyo, tunaishauri Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba ni vyema sasa...

**MBUNGE FULANI:** Kama mmeshindwa!

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Kama mmeshindwa, basi mtuambie ni namna gani tunaweza tukafanya vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza kwa uchungu mkubwa!

**MBUNGE FULANI:** Sana!

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Nazungumza kwa uchungu kwa sababu ni kauli ambayo mara zote inatolewa hapa, lakini masikio mmeweka pamba, hamtaki kusikia tunasema nini. Tunataka muwe na dira katika utawala wenu, muwe na mpango madhubuti. Mlizungumza kwamba kuna maeneo ambayo yako nyuma kimaendeleo ndani ya llani ya Chama cha Mapinduzi na mliwaambia Watanzania kwamba maeneo ambayo yako nyuma kimaendeleo tutayatilia mkazo ili kuvuta hoja za malalamiko mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Kigoma wanalamika na kadhalika, na watu wa Kusini pia. Litakwisha lini hili? Mimi natahadharisha tena ili tuweze kujenga umoja wetu, tuwe na imani na Serikali zetu ambazo zinakuja baadaye, ni lazima muangalie maeneo ambayo yako nyuma kimaendeleo na ambayo yanahitaji kuendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati umebadilika, siyo ule ambao unafikiriwa kwamba hakuna watu. Ndiyo tu leo, watu wamebadilika na wanataka maendeleo na watu wanataka kujua tunakwenda wapi? Tumeona athari za utawala wa kikoloni, lakini tukasema tunataka tupate utawala wetu ili tukidhi haja ya maendeleo yetu. Hatukumtoa mkoloni kwa sababu ni mweupe ili tumlete mkoloni mweusi, hatukuwa na dhamira hiyo! Tulitaka maendeleo ya kweli ili watu wafaidi uhuru wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miaka 50 leo, makumi matano, yaani nusu karne, kwa nini tunalamikia bandari yetu na Viwanja vya Ndege? Kwa nini tunalamikia bandari ambazo zipo na zilishajengwa wakati ule? Ni kuboresha tu, lakini kimefanyika nini leo? Bandari zile zile! Ukarabati tumeambiwa itajengwa Bandari ya Bagamoyo, kwa lipi? Hizi zilizokuwepo zimefika wapi mpaka mnazungumzia Bandari ya Bagamoyo? Au zinajengwa bandari hizi kwa sababu tu ya kulipa fadhila ya mamlaka ambayo mmeyapata? Kuna sababu gani wakati bandari nyingine bado zinahitaji ukarabati na matengenezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivi vitu kwa uchungu na hasira. Nasema bora niachie hapa. Ahsanteni kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, nakushukuru Mheshimiwa Barwany. Sasa nitamwita Mheshimiwa Anna Marystella Mallac.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipatia afya siku hii ya leo na siku zote na nitazidi kumtukuza siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, nitoe pole kwanza kwa wahanga wote waliokumbwa na ajali mbalimbali nchini Tanzania na waliopoteza maisha kutokana na ajali mbalimbali kama meli, magari, treni, ndege na kadhalika. Natoa pole sana na waliotangulia mbele ya haki, Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, na ambao bado ni walemavu wanahangaika, namwomba Mungu azidi kuwafariji. Hii yote inatokana na uzembe wa Serikali. Serikali imekuwa ikizembea vitu vingi, wananchi wanapolalamika na kusema haitekelezi kwa wakati, lakini badala yake huwa tunajifunza kutokana na makosa wakati sasa tumeangalia kwa macho jambo limetokea. Naomba Serikali sasa ijifunze kutokana na makosa yaliyotangulia kutokea ili mengine yasije yakatokea nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu amechangia vizuri sana, yaani Mheshimiwa Kikwembe ambaye tunatoka sehemu moja na kilio chetu wote wana Katavi, Kigoma, na Tabora ni reli ya Kati. Kwa

hiyo, naiomba sasa Serikali kwa mipango mizuri iliyotolewa katika hotuba yake, itekelezwe kwa vitendo, tusishuhudie tu maneno matupu na ahadi. Naomba sasa Serikali iende na vitendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu mara nyingi imekuwa ikiangalia hapa tulipo, haingalii mbele tunapokwenda. Naomba sasa iwe inaangalia kule tunakokwenda, tulijua kabisa Watanzania hili Shirika la TRL litatutesa na kweli limetutesa, yametimia sasa. Kama kweli hii hotuba kutokana na jinsi imeongea mambo mengi ya matamanio kabisa, kututamanisha Watanzania, naomba itokee kwa vitendo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingie ni Uwanja wa Ndege. Naishukuru Serikali kutukumbuka Wana-Katavi Mpanda kweli uwanja tumepata, tunashukuru sana na Wananchi wa Mpanda naona wanashukuru kwa hili. Lakini tunachoshukuru ni hewa, sidhani kama tutapanda hizo ndege, kwa sababu Serikali yetu ya Tanzania naona haina Ndege. Ina Ndege moja. Tulikuwa tunategemea ndege za wenzetu kuja kutua Mpanda. Ni aibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naoimba Serikali kutokana na mapato yake, ijipange na ikae inunue ndege za kutosha, tuwe kama nchi za wenzetu. Tusitegemee tu kuona maendeleo kutoka nchi za wenzetu. Tunataka kuona maendeleo kutoka nchi ya Tanzania kwa sababu nchi yetu ni tajiri sana. Kama Serikali ikikaa ikatulia na kujipanga, sisi ni tajiri sana katika nchi yetu, lakini tunakosa mipango, ndiyo maana siku zote tutazidi kuushuhudia umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema niaongelee suala la reli, mwenzangu ameliongelea kwa mapana sana. Ameongelea usumbufu wa tiketi wanaopata wananchi kitu ambacho na mimi nilipenda kuongelea, lakini nilipenda kukandamiza tu kwenye tiketi za Stesheni za Vijiji. Stesheni za Vijiji vilevile wananchi wamekuwa wakiumia sana kwa sababu treni inapotoka Tabora kwenda Mpanda inasimama kila kituo na kila stesheni ndogo inasimama, lakini wananchi au abiria wanaopanda huwa hawana tiketi, wanapanda tu kwa sababu treni imesimama na wao wanataka kusafiri. Lakini kwa kuwa hawana tiketi Ma-TT wamekuwa wakiwatoza faini. Wanawatoza faini kubwa na hata wakiwatoza faini hawawapatii tiketi mikononi.

Kwa hiyo, nina wasiwasi, wananchi wanalanguliwa kweli kwa kutozwa faini. Lakini vilevile Serikali inalanguliwa na inatiwa kwenye umasikini mkubwa sana kwa sababu zile fedha ambazo wananchi hawapati tiketi mkononi zinakwenda wapi?

Naomba Mheshimiwa Waziri hili alifuatilie sana na aangalie na atujibu, zile fedha ambazo wanalanguliwa wananchi kwa kutozwa faini kwenye Stesheni za Vijiji zinakwenda wapi na zinafanya kazi gani ili kuliingizia Taifa pato? Tunahitaji majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa reli siwezi kuongelea, nahama kwani imeongelewa kwa mapana. Sasa nakwenda kwenye usafiri wa barabara. Naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie sana katika hili.

Mikoa ya Katavi na Rukwa hasa Sumbawanga tuna shida sana ya usafiri kwa sababu kutoka pale Mpanda kwenda Sumbawanga tunatumia basi la kampuni moja ambayo ni Sumry.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni shida sana kwa sababu kila siku basi liko moja na ule mji umekuwa sana, abiria wanaohitaji kusafiri ni wengi sana. Kwa kuwa, kampuni ya basi ni moja Sumry, hivyo tutake tusitake tunajazwa sana kwenye basi lile kama vile kuku wanaopelekwa mnadani, wakati ni Watanzania wenyewe roho zao na wana haki ambazo wanazistahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba kabisa Mheshimiwa Waziri alifuatilie suala hili kupitia *SUMATRA*. Wananchi wa Katavi tunateseka sana kuifikia Sumbawanga kwa kutumia basi la kampuni ya Sumry. Kuna siri gani katikati ambayo inasababisha makampuni mengine hayaji kuwekeza kule na sisi tunahangaika kwa shida ya usafiri? Tunaomba Mheshimiwa Waziri atupelelezee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu siku moja avue suti yake avae mavazi ya kawaida, apige miwani yake apotee kabisa aslonekane kama yeye ni Waziri, kisha apande basi la Sumry kutoka Mpanda kwenda Sumbawanga ili aone siri iliyopo ndani yake na wananchi tunavyonyanyasika na kuhangaika. Tunajazwa sana, mle kiasi kwamba tunashindwa kupumua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta kwenye eneo la korido ambalo mtu unahitaji unyoshe mguu wako au

upite hata kwenda kuchimba dawa, huwezi kwani watu wamesimama, wamebanana hadi kwenye siti ya mwenzake, ukichanganya sasa na kabilia la watani zetu wa jadi kule Sumbawanga ndiyo unakuta sasa mle wamejazana na hewa inakuwa nzito, wananchi tunabaki tukihangaika. Tunahitaji msaada wa Serikali kwani tunahitaji kampuni nyingine zije ziwekeze kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mji wetu umekuwa na sasa ni mkoa, hivyo hatuwezi kutegemea basi moja la Sumry. Ajali zitakapotokea tutakuja kusema nini? Hakuna atakayepona kwani watu tunakuwa tumebanana sana, nafasi hakuna na matokeo yake abiria wengine wanaamua kupanda malori ili tu wapate usafiri. Hebu mtwambie ni sheria kweli kutumia malori kusafirisha abiria? Malori badala ya kubeba mizigo sasa yanabebe watu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atupe siri ya kwa nini wananchi wa Mpanda tunahangaika kwa kutegemea usafiri wa kampuni moja ya Sumry, tunashindwa kupata makampuni mengi ya usafiri pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, imewahi kujitokeza kampuni nyingine ambayo ni *Air Bus*, lakini ilifanya kazi kama muda wa wiki moja na baadaye ikaondoka. Wananchi hatujui na tukabaki tunajiuliza kulikoni? Tunaomba Mheshimiwa Waziri afuatilie suala hili na atupe majibu. Tunahitaji maendeleo na si kurudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Vitu hivyo wakati mwingine pia kwenye vikao vyetu vya *RCC* nadhani ni muhimu sana kuvijadili.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLACK:** Hatupati majibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, nadhani muda unaturuhusu na hivyo naweza kumwita Mheshimiwa Rajab Mohammed.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kukupongeza kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ku-*declare interest* kwanza kabla sijaendelea kuzungumza, kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Niliikataa bajeti hii katika Kamati na leo naendelea tena kuikataa ndani ya ukumbi huu wa Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za kuikataa bajeti hii ni kwamba, haikidhi haja na hivyo hawa Mawaziri tutawaonea tu. Hata lile lengo langu la kumtaka Waziri Mwakyembe pamoja na Naibu wake wajiuZulu, nafikiri sina hata haja ya kulipeleka mbele sana kwa sababu kutokana na fedha ambazo wametengewa katika bajeti hii hawawezi kufanya kazi, mwisho wake watakama tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika randama yao ambao walituletea katika Kamati, mahitaji yao na

fedha za *ceiling* ambazo zimetengwa zinapishana kwa karibu shilingi bilioni 443. Ni vipi wataweza kufanya kazi? Siyo rahisi, hawawezi kutekeleza majukumu yao. Taarifa yetu ya Kamati imesema kwamba, fedha hizi nyingi zitatumika kulipia madeni, bado ni hivyo hivyo. Nafikiri kuna haja ya kuiomba zaidi Serikali kama kweli inawapenda hawa Mawaziri na inahitaji waweze kufanya kazi, kwa kweli hii Wizara lazima iangaliwe upya katika suala zima la kuongezewa fedha, lakini bila ya hivyo wako vitanzini na Serikali itaendelea kubadilisha Mawaziri kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inanifikisha mahali naanza kuamini ule msemo wa marehemu Kolimba, jamani Chama Tawala mmepoteza dira. Mmepoteza mwelekeo, ni kweli? Maneno hayo aliyasema miaka mingi lakini sasa yanaanza kutuingia katika vichwa vyetu. Nafikiri kuna haja ya kufika mahali Serikali ijaribu kuangalia vizuri mapato yake, iangalie umuhimu wa hii Wizara ili tuwapunguzie mzigo hawa Mawaziri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala la usafiri na usafirishaji hususani ajali ambazo zinatokea katika bahari na nchi kavu na nini tufanye. Mwenzangu ameongelea sana kuhusu habari ya Meli. Lakini vile vile tuna ajali za barabarani na zile ambazo zinatokea katika maziwa yetu. Mwaka jana wakati nachangia Wizara hii nilitoa taarifa ya kiulimwengu inayooonesha kwamba karibia asilimia 25 ya vyombo ambavyo viko katika maji ya Tanzania vinaonekana ni vibovu na havifai kutembea baharini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli ya *MV. Skagit* ambayo ilizama juzi ilikuwa Marekani ikanunuliwa na wafanyabiashara wa Zanzibar. Kilichofanyika ni kwamba wafanyabiashara wa Zanzibar walikwenda kuiongezea ile meli. Kwa hiyo, kwanza ilipoteza ile *stability* yake, lakini vile vile baada ya kupoteza *stability* ile meli iliruhusiwa kutembea kilomita saba (7) tu na si zaidi ya hapo. Ni wataalam wetu hawa kukaa kitako wakaangalia zaidi, hicho nafikiri ndicho kilichotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa hii Mheshimiwa Waziri kwamba, tatizo kama hilo linamnyemelea katika Ziwa Victoria. Kuna meli inaitwa Sumari II ambayo ilikuwa inatumika kwa mizigo na inatoka Mwanza kuelekea Nansio katika visiwa vya Ukerewe, baadaye inatoka pale kuelekea Uganda. Meli hii ilikuwa inatumika kwa ajili ya kubeba mizigo, sasa hivi imebadilishwa matumizi. Wameipeleka pale kwenye *workshop* moja inaitwa Songoro, wameiongezea ongezea, wameweka viti ndani, hii meli sasa hivi inachukua abiria takribani 250.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, najua kwamba mzee wangu wa *SUMATRA* hili suala alilionna kwa sababu nilimdokeza na akajaribu kulifuatilia, lakini majibu aliyonipa nina wasiwasi nayo. Naomba Wizara kwa kuitia *SUMATRA* waende wao personally wakaliangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwombe Waziri au hata kama itawezekana Waziri anayekuja kwa sababu nimemwomba Mheshimiwa Waziri wa sasa ajiuzulu katika Wizara hii kutokana na matukio ya kuzama kwa meli iliyotokea Zanzibar. Nilzungumza

wakati nachangia katika Wizara ya Sayansi na Teknolojia na leo narejea tena kwamba, nataka ajiuzulu nikiwa na sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyongeza ya kwanza ya kipengele Na. 11, Bandari ni suala la Muungano, Usafiri na usafirishaji wa anga ni suala la Muungano, lakini vile vile utabiri wa hali ya hewa ni suala la Muungano na haya yote yamechangia katika kuzama kwa meli ile na waliopotea mle siyo Wazanzibari tu bali na wenzetu wa upande wa pili wa Muungano walikuwemo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamwomba Mheshimiwa Waziri hasa rafiki yangu kwamba, sasa tumefika mahali kile kitengo chetu cha *marine rescue coordination* hebu tukiangalie upya, tujaribu kukipa vifaa. Bainya Zanzibar na Dar es Salaam viko visiwa vidogo vidogo, kwa nini tusitafute *point* pale tukajua kwamba hapa tumeweza *camp* ya vijana wetu kwa ajili ya ku-rescue, lolote linaweza kutokea? Wale vijana tunaweza kuwapa vifaa hata helikopta, inakwenda pale ikiwa na nyavyu watu wanadandia na wanaokolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tusiangalie tu huu upande wa Zanzibar na Dar es Salaam, sasa hivi tuangalie huu mtandao wetu wa bahari kutoka Dar es Salaam, Mafia, Kilwa, Lindi na Mtwara. Kutokeana na uchumi unavyokwenda, kufunguka uchumi wa Mikoa ya Kusini kwa kweli safari za kutumia bahari nina

uhakika kabisa zitaanza. Nimemsikia mchangiaji mmoja wa mikoa hii Mheshimiwa Juma Njwayo hapa amesema kutakuwa na meli ambazo zitasafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *it means* hapa usafiri utafunguka. Kabla hatujafika katika matatizo kuna haja ya kuangalia huko nako uwezekano wa kuwa na *rescue team* kwa ajili hiyo. Lakini kubwa zaidi tunategemea kujenga daraja la Kigamboni, kwa kweli pale patahitajika vile vile kuwa na *rescue team* kwa ajili ya uokoaji kwani najua mengi yatatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na msimamo wangu wa kutokuunga mkono hoja hii na kumtaka kwamba kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano Waziri na yeze afuate nyayo za Waziri mwenzake wa Miundombinu wa Zanzibar kwa kujiuzulu. (*Makof/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Rajab Mohammed. Waheshimiwa Wabunge nimebakiwa na dakika chache na wakati ule wakati tunataka kuanza uchangiaji, Wabunge kadhaa walismama kuomba Mwongozo. Busara za Kiti zilinishauri kwamba ni bora tuendelee kwanza na kazi halafu tukibakiwa na dakika chache basi tuzitoe ili tuweze kusikiliza hiyo Miongozo. Nadhani nina dakika kama tatu hivi, kwa hiyo, naomba kwa ufupi sana, kama mtu ataendelea kwa muda mrefu nitatumia Kanuni yangu ya Tano (5) kumkatisha na kuondoa Mwongozo wake.

Haya Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Murtaza Mangungu na Mheshimiwa Moses Machali!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kanuni ya 68(7) kuhusu Mwongozo wako. Suala hili pia ningeweza kutumia Kanuni ya 47, lakini nimeona nisiende kwenye Kanuni ya 47, labda tuitake tu Serikali itoe maelezo. Taarifa nilizozipata kutoka kwa baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya ambao wamekuwa wakipiga simu, lakini pia na gazeti la Serikali la *Daily News* jana lilitoa habari ambazo zinawatia Watanzania wasiwasi hasa wa Mikoa ya Mbeya na Iringa kuhusiana na hali inayojitokeza sasa kule Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Malawi kupitia Katibu Mkuu wake wa Wizara ya Mambo ya Nje, imetamka kwamba Ziwa Nyasa kama lilitovo lote ni mali ya Malawi. Kwa maana hiyo, kwa sababu wao wanasema wanatumia kumbukumbu au wanatambua mipaka iliyowekwa na Mjerumani mwaka 1890 ambayo ilionesha kwamba Ziwa Nyasa lote ni la Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu wa Wizara ile amesema na naomba ninukuu kidogo kutoka katika gazeti la Daily News kwa lugha aliyoitumia: "*We categorically put it to them (Tanzania) that, as far as we are concerned the entire lake belongs to Malawi*" Hiyo ndiyo kauli yake na kwamba wanategemea taarifa hiyo.

Sasa kunapokuwa na jambo kama hili zito na nyeti kwa usalama wa wananchi hasa wa Mikoa ya Mbeya na Iringa na nashukuru pia kwamba Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, alikuwa analitolea ufanuzi jambo hili kwamba ni *serious* na ni lazima tuliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri ni busara ya kawaida Wabunge na Bunge lako lijue jambo hili ni la hatari na linaashiria hali isiyo njema. Kwa hiyo, Wabunge na Bunge hili wangepaswa kuelezwani nini kinachoendelea ili wananchi wanapotuuliza tuwe tayari kuwaeleza ni kitu gani kinaendelea. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Mheshimiwa Felix Mkosamali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Natumia Kanuni hiyo hiyo ya 68(7) kuomba Mwongozo wako kuhusu Kamati ambayo imeundwa leo. Kamati ile Wabunge wengi ambao wanatuhumiwa kwanza ni wa Chama cha Mapinduzi na haina uwiano wa vyama.

Watu watatu kwenye Kamati ile wanatoka Chama cha Mapinduzi, lakini kuna vyama tumekuwa hapa Bungeni kama *NCCR-Mageuzi* hatuingizwi kwenye Kamati hizi za Bunge na wakati tupo watu ambao tuna *integrity* na tuna uwezo wa kushauri na kusimamia mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili Mwongozo wangu kwenye jambo hili nataka nifahamu kuhusu hadidu za rejea ambazo zimetolewa pale kwa sababu kuna Wabunge ambao wamehusishwa kuwa na *interest* lakini imeonesha kwamba, Kamati hii inakwenda kuzungumzia jambo moja tu la Wabunge waliothumiwa na rushwa. Sasa naomba Mwongozo wako, kwa nini vyama vyote visiwe na mjumbe mmoja mmoja katika Kamati ile ili kuwa na haki? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Mheshimiwa Murtaza Mangungu!

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie Kanuni hiyo ya 68(7). Katika Mkutano huu wa Nane ratiba iliyotoka mwanzo ilionesha kwamba Mkutano huu utakwisha tarehe 22 ya mwezi wa Nane. Kumekuwa kuna mabadiliko mbalimbali ambayo yamekuwa yakifanyika katika ratiba hizi, lakini kwa mujibu wa Kanuni zetu tumekuwa tukipewa taarifa za maswali ambayo tulikuwa tumewasilisha kwa Serikali kujibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kadri siku zinavyorudi nyuma maswali yale yanakuwa hayaeleweki kwamba yatajibiwa katika Mkutano huu au yatakuwa katika hatima ipi tukizingatia hata katika siku ya leo kulikuwa na nafasi kubwa ya kuuliza maswali lakini yaliulizwa manne tu.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Mheshimiwa Moses Machali! Kama limekwisha sema usirudie, labda liwe jipya.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) hiyo hiyo kuweza kuomba Mwongozo wako. Suala ambalo nalizungumzia ni hili hili ambalo Mheshimiwa Mkosamali amelizungumzia kuhusiana na Kamati Teule ya Bunge ambayo imeundwa kuweza kuchunguza masuala ya rushwa kwa Wabunge.

**MWENYEKITI:** Kama ni hilo hilo Mheshimiwa hatuna muda, naomba...

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kitu cha kuongezea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali hatuna muda. Umekwishesema ni hilo hilo alilolizungumzia Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** (Aliongea bila kutumia *microphone*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali umeanza kwa kusema suala lako ni hilo hilo alilolizungumzia Mheshimiwa Mkosamali, sasa bora usingeanza na hilo neno. Naomba nisimame sasa nitoe hiyo Miongozo.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Mwongozo wa kwanza Mheshimiwa Zambi amesema hapa kitu kizito na ameomba kupata maelezo ya hali ilivyo katika mahusiano yetu na nchi ya Malawi hususan katika suala la mpaka wa nchi ya Malawi na Tanzania na

yanayoendelea kujiri, matamshi ya viongozi mbalimbali katika vyombo vya habari na kadhalika.

Mwongozo wangu, naomba niseme kwamba, suala hili nilipeleke Serikalini, Kaimu Waziri Mkuu yuko hapa ndani na nadhani amelisikia. Tunaomba walifanyie kazi na tutawasiliana kati ya Serikali na Ofisi ya Bunge kuona namna tutakavyolifanyia kazi na kulitolea taarifa pale itakapoonekana inafaa ili kuwapa taarifa Watanzania wajue kinachoendelea kwa kadri Serikali itakavyokuwa imejipanga kupitia kwenye ofisi yetu ya Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Mkosamali amezungumza mengi lakini amejikita katika kuhoji Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Spika. Kwa mujibu wa Kanuni mambo ambayo yemekwishafanyiwa maamuzi huwa hayaruhusiwi tena kuzungumzwa na kujadiliwa Bungeni. Lakini kwenye hadidu alizozileta Mheshimiwa Spika za kuzungumzia suala hilo na uundaji wa Kamati hiyo, kwanza alisisitiza kwamba Kamati hiyo imeundwa kwa mujibu wa Kanuni yetu ya Bunge Namba 114(18).

Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wanisikie, Kanuni hiyo ya 114(18) inasema: "Kamati yoyote inaweza kuunda Kamati Ndogo kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zake kadri itakavyoona inafaa na kila Kamati Ndogo itapangiwa kazi zake na Kamati ya Kudumu inayohusika".

Sasa kwa mujibu wa Kanuni hii ina maana Wajumbe wanaoingia kwenye Kamati hiyo ndogo inatakiwa watokane na Kamati ya Kudumu ya Bunge

iliyopelekewa suala hilo, iko kwa mujibu wa Kanuni. Sasa leo tukianza kuhoji kwa nini wajumbe wengine hawajaingizwa kwenye Kamati hiyo sijui tunataka nini! Tulikubaliana hapa suala hilo liende kwenye hiyo Kamati Ndogo ya Maadili na Kamati hiyo Ndogo ipo na wajumbe wake wanajulikana na kwa mujibu wa Kanuni ya 114(18) inaitaka kila Kamati ya Kudumu ya Bunge inapopewa jambo mahsus ianaweza kuamua kuunda Kamati yake Ndogo.

Lakini Waheshimiwa Wabunge hadidu za rejea zilizosomwa na Mheshimiwa Spika zimesema hivi; hata Mbunge mwingine yejote ambaye anaweza kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa suala hili hajafungwa kwenda. Sasa jamani tukienda wote hiyo kazi itafanyikaje? Kwa hiyo, kama kuna mtu mwenye jambo lolote hapa hadidu zimeeleza wazi anaruhusiwa kwenda.

Hata kama unataka kuhoji uadilifu wa mjumbe wa Kamati hiyo unaruhusiwa kwenda. Kwa hiyo, wala tusifungwe hapa na wala tusianzishe tena hoja nyingine wakati vitu vyote viko sawa kikanuni na hadidu za rejea zilizosomwa na Mheshimiwa Spika ziko wazi Waheshimiwa Wabunge.

Mwongozo wa mwisho ni ule ulioombwa na Mheshimiwa Murtaza Mangungu kuhusu ratiba ya kazi. Kamati ya Uongozi imeketi, imefanya mapitio na ratiba iliyotoka ambayo nimeipata leo mezani tutamaliza Mkutano wetu wa Bunge tarehe 16 mwezi wa Nane siku ya Alhamisi.

Sasa kuhusu maswali yale ambayo hayatapata nafasi ya kujibiwa katika Bunge hili kwa vyovyote vile Bunge halijakwisha, yataendelea kupangiwa nafasi na yataendelea kujibiwa katika mikutano mingine inayofuata.

Ni lazima tutende haki kwa wenzetu Waislamu, walikwishatoa hoja ya kuomba ratiba iishe mapema ili wapate nafasi ya kushirikiana na familia zao katika kusherehekea sherehe hizi za Iddi. Sasa linapotokea jambo mahususi kama hilo basi hatuna jinsi tena, shughuli nyingi za Bunge itabidi zikatishwe ili kutekeleza azma ya hoja iliyotolewa na hasa kwa kuzingatia mwezi Mtukufu wa Ramadhani unavyoendelea kuishia.

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo miongozo niliyopata na hayo ndiyo majibu yangu.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

*(Saa 7.20 mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 10.00  
jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hoja ambayo ipo hapa mezani kwetu. Hoja iliyowekwa mezani na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Uchukuzi. Tulipomaliza muda wetu wa mchana kwa wachangiaji kuendelea kuchangia mada hii. Sasa nilibakiza wachangiaji wachache ambao nilikuwa nawaita, lakini

hawakuwemo ndani ya Ukumbi wa Bunge na sasa hivi siwaoni tena humu ndani.

Nilifikiri kama Mheshimiwa Said Amour Arfi angekuwepo basi tungempa nafasi ndiyo mchangiaji wetu aliyebaki. Basi kwa hatua hiyo nitamwomba Katibu aniongoze kwa ratiba hii ya jioni. Halafu sasa tuendelee na hatua inayofuata.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokuwa nimesema awali wale wachangiaji ambao nilifikiri wangekuwa wapo ndani ya Ukumbi jioni hii wale niliowaita asubuhi na hawakuwepo nilidhani wangewahi halafu wangeweza kupata nafasi ya kuchangia.

Kwa kuwa, sasa hawapo na Katibu ameshaniongoza kwa hatua inayofuata. Sasa sina budi kuingia kwenye hatua ya watoa hoja sasa moja kwa moja na nitaanza kumpa nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa mujibu wa taratibu walizopanga Mheshimiwa Naibu Waziri atatumia dakika 30 na dakika nyingine zitakazobaki zitatumia na Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Tizeba, karibuni sana.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehemta kwa kunijalia afya njema katika mwezi huu Mtukufu na kuniwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa Nane wa Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu mkubwa, kudumisha umoja, amani na utulivu katika kipindi chote cha uongozi wake. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu kwa kunitua kuwa Naibu Waziri wa Uchukuzi. Naahidi kutekeleza wajibu wangu kwa uaminifu na uadilifu mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kutoa pole tena kwa watu wote waliopoteza wapendwa wao katika ajali ya *M.V. Skagit* iliyotokea hivi karibuni, Mwenyezi Mungu awape moyo wa uvumilivu ndugu wote na azilaze mahali pema peponi roho za marehemu. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe, kwa ushirikiano wake anaonipa katika utendaji wa kazi wa kila siku. Aidha, napenda kuwashukuru viongozi wengine wa Wizara, akiwemo Katibu Mkuu, Mhandisi Chambo, Naibu Katibu Mkuu bwana Mgodo, Wakurugenzi wa Wizara, Wakuu wa Taasisi zetu, pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wao kwangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya pekee kabisa, naomba nimshukuru mke wangu mpenzi Furaha Tizeba yupo hapo juu kwa kunivumilia na kunitia moyo tangu niteuliwe kuwa Naibu Waziri wa Uchukuzi na hasa baada ya kuanza kwa Bunge hili la Bajeti.

Aidha, nawashukuru watoto wangu Hilda na wadogo zake kwa kuwa karibu nami na kunipa moyo wa nguvu ya kuendelea na majukumu ya Kitaifa na Jimbo letu la Buchosa katika kipindi chote ninapokuwa mbali nao. Nawaahidi kuungana nao tena mara baada ya kumalizika kwa Shughuli za Bunge katikati ya mwezi huu. (*Makof*)

Nawashukuru Madiwani wenzangu wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kwa kukubali kuja Dodoma kunitia moyo wakati Wizara yangu ikiwasilisha bajeti yake. Nawashukuruni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naomba nitoe shukrani zangu za kipekee kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Buchosa liliopo Wilaya ya Sengerema kwa imani waliyonayo kwangu na ushirikiano mkubwa wanaonipa. Naahidi kuwa sitawaangusha. Aidha, nawashukuru viongozi wote wa Jimbo langu kuanzia ngazi ya Vijiji, Kata zote 14 hadi Wilaya kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba kuchukua fursa hii kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa katika michango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hoja ya Mheshimiwa wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba. Mheshimiwa Peter Serukamba amesema Kamati inashauri kwa fedha kidogo iliyopo itumike kuimarisha reli iliyopo kwanza mpaka itakapoweza kufanya kazi

kwa uwezo wake ndipo tuingie kwenye miradi mingine ya kuongeza mitandao ya reli nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, Serikali hili inalitambua na ndiyo maana inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ambayo lengo lake ni kurejesha huduma za usafiri wa reli katika hali yake ya kawaida hususani reli yetu ya kati kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma na kutoka Tabora kwenda Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati jana nikijibu swalihapa Bungeni nilielezea kwa kirefu hatua mbalimbali zinazochukuliwa sasa kuimarisha reli yetu hii ya kati, ipo miradi mingi na naishukuru sana Serikali kwamba mwaka huu bado imetuwezesha, imetutengea fedha za kutosha kuendelea na mikakati hii ya uimarishaji wa reli ya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile reli yetu ni ya zamani Serikali inaendelea pia kutekeleza miradi ya upembuzi na usanifu kwa ajili ya kuinua kiwango cha reli au kujenga reli mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili niseme tu kwamba labda nitumie nafasi hii kuwaeleza Watanzania nini hasa kinaigusa reli yetu na kuonekana wengine hata wakiibeza kwamba imezeeka na kupitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli haiwezi kuzeeka kwa maana ya kuzeeka, hivi ni vyuma. Lililotokea ni kwamba Wajerumani wakati wanatujengea hii reli

walijenga reli nyembamba na vyuma vyenye uzito mdogo. Lakini niseme leo na hili nipende kumfahamisha Msemaji mmoja kutokea kundi la Upinzani aliyesema reli hii imepitwa na wakati hatuwezi hata kupata vipuri popote duniani na nini kwa sababu imezeeka na kupitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajenda siyo uzee wa reli. Tatizo kubwa tulilonalo ni tuta letu la hii reli. Naomba niseme tu wazi kwamba, *meter gauge* kwa maana ya upana wa reli wa mita moja ile siyo tatizo kubwa sana linalotusumbua kwa sababu Tanzania siyo nchi pekee, sasa hivi ambayo reli yake ni ya upana huo wa mita moja. Zipo nchi nyingi sana duniani bado zinatumia reli yenye upana wa mita moja na zinaendelea vizuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo letu kubwa la msingi kwenye reli yetu ya Kati ni uwezo wa tuta kupitisha vichwa vyenye uzito mkubwa. Madaraja mengi yaliyopo kwenye hii reli yetu kuanzia Dar es Salaam kwenda Kigoma, mpaka Mwanza yanaweza kupitisha mzigo usiozidi tani 13.7 yaani *the maximum axial load* kwenye reli yetu ni 13.7 tani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vichwa vingi ambavyo vinatengenezwa sasa hivi duniani ni vizito zaidi kwa maana vinavyo *axial loads* kubwa kuliko 13.7. Kwa maana hiyo, hata tukitaka kununua vichwa vyana namna hiyo tunakuwa hatuwezi kuvipata *ready made* ndiyo maana tunalazimika kufanya *order* ili watutengenezee sasa vinavyoweza kupita kwenye reli yetu hii yenye uwezo mdogo. Lakini tukiimarisha hilo tuta tutaweza kupata vichwa hivi vingi tu huko duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo ramani hapa tutawasambazia Waheshimiwa Wabunge waone ni nchi ngapi bado nyingi duniani zinatumia reli yenye upana huu wa mita moja na maisha yao yanakwenda vizuri tu.

La pili, katika reli yetu sehemu kubwa ilikuwa imetandikwa reli zenyе uzito mdogo. Reli zenyе uzito mdogo zinapinda na kuharibika kwa haraka. Kwa hiyo, haziwezeshi reli zinazopita juu yake kwenda kwa *speed* kubwa kama tunavyodhamiria. Leo wastani wa *speed* wa reli yetu ni kilomita 20 kwa saa moja, lakini pale ambapo tumebadilisha na kuweka reli yenye uzito wa kilo 40 kwa mita moja treni zinakwenda mpaka kilomita 50 kwa saa moja. Kwa hiyo, tukibadilisha uzito wa vyuma vile tukaongeza uwezo wa madaraja yetu kupitika kwa treni nzito, reli yetu hii inaweza ikatusukuma mbele miaka mingi bila kuwa na manung'uniko haya yanayojitokeza sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini vichwa ni vizito labda na hili lenyewe ni jambo ambalo lazima tuelewane vizuri. Vichwa vizito tunavihitaji unapokuwa unataka kubeba mzigo mkubwa zaidi. Kichwa kikiwa chepesi na mzigo unaotakiwa kuvutwa ni mkubwa hakiwezi kutoka kwa sababu kinahitaji *resistance* iwe kubwa sana pale kwenye reli ili kiweze kuvuta. Hili ndilo linalolazimisha sasa watengenezaji wa vichwa vyta treni wa kisasa watengeneze vichwa vyenye uzito mkubwa ili viweze kubeba mzigo mkubwa zaidi. Kwa hiyo, *combination* ya haya mambo ndiyo *disadvantage* tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu hapa wamekuwa wanasema ooh, reli yetu hii imezeeka, hapana, tuelewane kuhusu matatizo ya msingi ambayo tunayo. Lakini yote kama nilivyoyataja siyo kwamba hayana suluhisho, yana suluhisho suala ni wenyewe kuamua twende namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mizigo mingi kweli inapaswa kupitia Bandari ya Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu amesema ni kweli, lakini kwa sasa haiwezi kupita kwa *simple reason* kwamba uwezo wa reli yetu ni mdogo kwa sababu hizo nilizozisema. Kwa sababu ya ile miaka 15 ya kutokuwekeza kwenye reli yetu vichwa vingi viliharibika na vikakosa utengenezaji. Kwa hiyo, leo tunasema tunavyo vichwa 22 katika Reli ya Kati vinavyofanya kazi lakini *available locos* kwa siku havizidi vichwa nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunavyo vichwa 20 ndiyo vinavyofanya kazi, lakini ukimkamata Mtendaji Mkuu wa *TRL* kwamba leo vichwa vingapi unaweza ukaviingiza kwenye reli bila shida atakwambia havivuki nane. Kwa maana hiyo, ndiyo maana leo ndugu zangu, Watanzania wenzangu, mnaona inakuwa shida sana kwa Shirika letu la Reli kusema wataanza safari za kwenda Mwanza kwa sababu vichwa vya treni havitoshi na mabehewa hayatoshi. Tunao mzigo mwangi tu lakini uwezo wa kuubeba ndiyo hu, ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwezo mdogo wa reli lakini hata ufanisi wa bandari yetu na

wenyewe siyo mzuri sana. Tunayo matatizo pale na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri atakuja hapa atasema nini kinachofuata. Ipo haja kubwa ya kuharakisha ujenzi wa gati namba 13 na 14 ili tuiongezee ufanisi bandari. Kwa sababu Wizara na Serikali inaamini kabisa kwamba reli ikidorora bandari inadorora, bandari ikidorora na reli inadorora. Kwa hivyo, haya yanakwenda kwa pamoja, ni vitu ambavyo vinahusiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kusema kuwa, tumekwishaunda Kikosi Kazi kuangalia namna gani hivi vyombo vinaweza kufanya kazi kwa pamoja ili viweze kuleta tija zaidi. Pamoja na hatua hiyo ya kuangalia namna gani *TRL* na bandari watafanya kazi kwa pamoja. Lakini zipo hatua mbalimbali ambazo zinaendelea kuchukuliwa na Mamlaka za Bandari na *TRL* na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi juzi Dkt. Mary Nagu alizindua Kituo cha *One Stop Center* ili kwamba wadau wote wa ku-process mizigo bandarini wawe sehemu moja ili kusiwe na hii kwamba unatoka jengo hili unakimbia kwenda kwingine kuharakisha tu ule uwezekano wa kuchukua mizigo bandarini kwa watumiaji wa bandari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, treni ya kwenda Mwanza tumejitahidi kutoa maelekezo, kusimamia na kusaidia kwa kadri inavyowezekana ili angalau agizo la Wizara kwamba ifikapo mwezi Septemba, mwaka huu tuanze kupata treni ya abiria kwenda Mwanza liweze kutekelezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kusema kwamba, kwa mazingira yalivyo ikitokea bahati mbaya na narudia ikitokea bahati mbaya mwezi Septemba, ikatushinda lakini tunaweza tukaguarantee kabisa kwa uhakika mkubwa kwamba mwezi Desemba, mwaka huu haiwezi kufika kabla hatujaanza kupeleka treni ya abiria Mwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna waliouliza kwamba kwa nini *RAHCO* bado inaendelea kuwapo, baada ya Mkataba na *RITES* kuvunjika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *RAHCO* ilianzishwa kwa makusudi maalum na kwa Sera yetu ya Uchukuzi ambayo ipo na tunajaribu kuiboresha. Sasa hivi utumiaji wa reli hautakuwa tena na *exclusivity* kwa *TRL*. Tunatarajia kukaribisha watumiaji wengi zaidi wa hiyo reli na kwa hiyo, lazima kiwepo chombo cha kusimamia utumiaji wa reli yenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sasa bado ile haja ya kuwa na *RAHCO* ipo, mbele ya safari kule tutajua ina *work* namna gani na iliyokuwa pacha wake *TRL*. Lakini kwamba *RAHCO* imekosa umaana wa kuwepo tena siyo hoja ya sasa hivi. Tunayo haja ya kuwa na chombo cha usimamizi wa hiyo reli ili kuruhusu watumiaji wengine ambao siyo Serikali kuweza kutumia reli lile bila ya mgongano wa kimaslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati na uimarishaji wa reli unaofanyika sasa hivi. Ni kweli kwamba kama ilivyokuwa imesemwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa

Waziri, reli ilianza kuharibika sana baada ya mwaka 2007, mvua kubwa zilinyesha zikaizoa reli katika vituo vipatavyo 32 kati ya Gulwe na Kilosa. Uharibifu huu ulifanya treni zisimame kwa karibu miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tutumie nafasi hii kuwapongeza sana *RAHCO* yenyewe, Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kazi kubwa sana waliyoifanya ya ku-*restore* ile reli wakati ule. Wenzetu hawa walifanya kazi kubwa na ya kutukuka kabisa. Kwa sababu katika kipindi kifupi ambacho hakikutarajiwa waliweza kurudisha tena usafiri wa treni kati ya Dodoma na Dar es Salaam ingawa kwa kipindi hicho ilionekane si vyema kupitisha treni ya abiria maeneo hayo kwa sababu yalikuwa bado hayajaimarika vya kutosha. Kwa hiyo, kwa muda mrefu ziliendelea kwenda treni za mizigo na mpaka hivi majuzi ndiyo tuliona kwamba sasa ukarabati na marekebisho yale unatosha kuweza kuruhusu treni za abiria kuanza kwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo mambo mengi yaliyozungumzwa kuhusu viwanja vya ndege. Nianze na lile alilozungumza dada yangu kuhusu Uwanja wa Ndege wa Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja ule wa ndege unaendelea kufanyiwa matengenezo, *runway* inawekewa lami, lakini na jengo la abiria linafanyiwa matengenezo makubwa. Kilichotokea pale katika *design* ambazo Mhandisi Mshauri alikuwa ametayarisha, mjenzi kwa maana ya *contractor* alipoanza kufanya kazi kukatokea ubishi kuhusu zile

*levels, contractor* akaziona kwamba zile *levels* haziko sahihi na *consultant* aki-maintain kwamba *levels* zipo sahihi. Hili ni jambo la kiufundi kidogo, lakini kutokuelewana kule kungeleta ucheleweshaji wa kazi au kuongezeka gharama ya mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima nikiri baada ya kupata habari kutoka kwa Mbunge wa Bukoba Mjini, Mheshimiwa Kagasheki kwamba pale mambo hayaendi vizuri. Mapema tu tuliliona hili tukawapa maelekezo kwamba, badala ya kuendelea na mabishano hebu wakali-survey pamoja, tena wawe na uhakika *levels* gani ni *appropriate* kwa *design* ya sehemu ile. Hiyo ni kazi ambayo inaendelea na nadhani watakuwa wanakaribia kukamilisha ili sasa kazi ifanyike kwa maelewano, asiwepo mtu baadaye kuja kulalamika kwamba sikuwa nimepewa *information* ambayo ni sahihi zaidi katika kutekeleza hii kazi. Kwa hivyo suala la Uwanja wa Ndege wa Bukoba sasa hivi linakwenda vizuri na tuna uhakika kwamba litaendelea na uwanja utakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ya *Consultant* alikuweko *Resident Engineer* pale upande wa *consultant* ambaye bahati mbaya alipata na ugonjwa, lakini tukawa na bahati nzuri tu kwamba *consultant* yule yule ndiye anasimamia na viwanja vya Tabora na Kigoma. Kwa hivyo, alichukuliwa *Resident Engineer* kutokeviwanja vingine amekwenda pale na kazi inaendelea. Kwa hiyo, Uwanja wa Ndege wa Bukoba utaendelea kujengwa bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mazungumzo ya ukatishaji wa tiketi katika Shirika letu la Reli la Tanzania kwamba una usumbufu, watu wanunung'unika kwamba tumeelekeza wasafiri wanunue tiketi kwa kutumia vitambulisho. Napenda tu kuwaomba sana Wabunge waliochangia hoja hii wafahamu kwamba hakuna nia ya kumsumbuu mtu yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ilifanya ziara Kigoma baada ya kulalamikiwa na wananchi pale *Railway*, Kamati ya Bunge ikatoa ushauri kwa Serikali kwamba sasa tiketi watu wasinunue kwa *ku-book*, watu wanunue siku hiyo hiyo ya safari.

Kwa nini walifanya hivyo na mimi nakubaliana nao kabisa, kwa sababu kwanza nafasi ni chache, kwa hivyo tukiruhusu watu wafanye *booking*, wanunue tiketi siku mbili, tatu ama tano kabla ya safari watu wa Kigoma Mjini au Mpanda Mjini pale ndio pekee watakaonunua hizo tiketi watawalangua wanaotoka Kasulu na Kibondo na kwingine. Kwa hivyo, Kamati ya Bunge ikatoa ushauri mzuri tu ambao tuliukubali kwamba tiketi ziuzwe siku ya safari yule anayesafiri afike pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huo umeendelea lakini bado haukuzuia ulangazi kwa sababu watu wakawa wanawahi saa 11.00 alfajiri wanajipanga kwenye foleni, ananunua tiketi 30. Baada ya masaa mawili Karani lazima atangaze tiketi zimekwisha, sasa akitangaza tiketi zimekwisha wale walionunua wanaanza ulangazi, badala ya shilingi 19,000 wanaanza kuuza shilingi 30,000 mpaka 35,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyokwenda kule na kusikia hayo malalamiko, nilijifunza kidogo kinachoendelea pale na ndio nikatoa maelekezo mbadala kwanza kuanzia sasa mtu anunue tiketi kwa kitambulisho na apande treni kwa kitambulisho hicho hicho kilichomfanya anunue tiketi. Kwa hiyo, kama mtu anaweza akachapisha vitambulisho vya watu ambao hajawajua watakuja kuwalangua tiketi basi huyo atakuwa amefanikiwa kukwepa mtego.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huu ni utaratibu ambao sijasikia wasafiri wa anga wakiulalamikia kwa sababu huwezi kununua tiketi ya ndege bila ya kuwa na kitambulisho na huwezi kupanda ndege bila ya kuwa na kitambulisho. Sasa iweje hapa wasafiri wa treni ndio wanunuung'unikiwa sana. Naogopa kusema kwamba wanaosukuma hili jambo ni wale wale huenda wanaonufaika na ulanguzi wa hizo tiketi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa ya kudumu ya kutolanguliwa tiketi ni kuwa na treni nyingi kwa wiki, kuwa na mabehewa ya kutosha, hili sio jambo la kufikiri sana. Lakini katika kipindi hiki ambacho vitu hivyo havipo lazima tuwallinde wale ambao wana nia ya kweli ya kusafiri kutoka kwa hawa walanguzi wanaotaka *ku-take advantage* ya mazingira magumu ambayo leo tunayo katika usafiri wa reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hali ya Hewa tumesikia Mheshimiwa mmoja akisema *TMA* wanacho chuo Kigoma na hakijapewa fedha ya kutosha. Niseme tu kwamba, mafunzo katika chuo

hicho yanaendelea vizuri, wako vijana pale wanapata mafunzo na katika mwaka huu wa fedha chuo kimetengewa fedha za maendeleo shilingi milioni 200 kwa ajili ya kujengea uzio wa chuo hicho. Tuombe tu uelewa, kwa kitu kidogo kama kile, fedha ile kwa miradi ya maendeleo inawatosha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa usafiri ndani ya Ziwa Victoria, Kampuni yetu ya *Marine Services* wamepita nao katika kipindi kigumu sana. Sio siri Bunge hili Tukufu mwaka jana liliwapitishia bajeti ya karibu shilingi bilioni 6.7. Fedha waliyopewa kwa mwaka wa fedha unaokwisha ni shilingi milioni 400. Kwa hiyo, ukiona katika bajeti ile ya shilingi bilioni 6.7 wamepewa shilingi milioni 400 wamechukua fedha hizi wakalipia Bima ya Meli zile ambazo wanazitumia. Kwa hivyo, mwaka wa fedha wote uliopita hawakufanikiwa kufanya matengenezo makubwa yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hapa kwamba, wanaosema Victoria imechoka ni hawaioni hali halisi ya nchi hii. Ni kweli Victoria inahitaji matengenezo makubwa na tumetenga fedha katika bajeti hii kwa ajili ya matengenezo makubwa, mara ya mwisho nilivyokuwa Mwanza nilielekeza kwamba mambo ambayo hayahitaji fedha nyingi yafanywe mara moja. Shilingi milioni 400 waliyokuwa wametengewa *Marine Services* kwa ajili ya bima niliwaelekeza kwamba wasilipe bima kwa meli zao zote hata zile ambazo ziko kwenye cherezo kwa ajili ya matengenezo. Walipie bima meli zilizoko majini ili *saving* ile watakayofanya wafanye angalau ukarabati mdogo ili kuwafanya wasafiri wanaotumia meli hizo waende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelekeza nguo yako hata kama imechafuka huachi kuifua. Kwa hivyo, *Marine Services* wameelekezwa pia kwamba wafanye usafi kadri inavyowezekana ili msafiri hata kama anaingia kwenye ile meli anaona imechoka, lakini angalau ni safi na haikatishi tamaa kuitumia. Kule Ziwa Viktoria labda niseme kwanza naona mama Mkiwa aliuliza nitakwenda wapi, kwa nini hatutoi tena huduma ndani ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari maelekezo yamepelekwa kwa *Marine Services* kwamba wafanye *survey* ya bandari zote walizokuwa wanafika. Huko Ziwa Victoria kulitokea upungufu mkubwa wa kina cha maji, kilishuka sana na kwa hivyo meli zetu nyingi zilishindwa kwenda kwenye hivi visiwa ambako zilikuwa zinakwenda zamani. Kwa hiyo, tumewaelekeza wakafanye *survey* waone bandari zote zile ambazo kina kinaruhusu meli za Serengeti, Clarious, Butiama ambayo inafanyiwa matengenezo itakapopona zitakapoweza kwenda ili waweze kuanza kwenda kutoa huduma sehemu hizo. Wananchi wa maeneo hayo wasidhani kwamba Serikali imewatelekeza kulikuwa na tatizo kwanza la uharibifu wa meli zenyewe, lakini na kina cha maji kilipungua sana kuwawezesha kwenda kwenye vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Tanganyika *M.V. Liemba* itafanyiwa matengenezo na Serikali ya Ujerumanu. Serikali ya Ujerumanu imekwishaagiza Kiwanda cha *Twiga Cement* kutoa euro milioni 2.5 kwa ajili ya matengenezo ya *M.V. Liemba*. *M.V. Liemba* ikitengenezwa itaendelea kutoa huduma kwa sasa mpaka pale *DANIDA* watakajengwa meli nyingine

kubwa ya kisasa ndani ya Ziwa Victoria na mradi huo utaanza hivi karibuni. Kwa sababu sasa hivi *DANIDA* wapo katika mchakato wa kumpata *consultant* atakayesimamia matengenezo ya hizo meli moja ndani ya Ziwa Victoria, moja ndani ya Ziwa Tanganyika na moja ndani ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyozungumza *M.V. Liemba* haifanyi safari moja katika Ziwa Tanganyika kama mmoja wa wachangiaji hapa alivyosema. *M.V. Liemba* inafanya safari mbili kwa mwezi ndani ya Ziwa Tanganyika na sio safari moja, naomba niweke hiyo rekodi vizuri. Ndani ya Ziwa Nyasa, *M.V. Songea* ambayo ilikuwa inafanya kazi kule ilipata hitilafu tukaipeleka *Monkey Bay* kule Malawi kwa matengenezo, imeshafanyiwa ukarabati, tumelipa fedha zote kwa ajili ya ukarabati huo, inafanyiwa majaribio na keshokutwa nitakwenda huko kwenda kuona kama kweli inafanya kazi kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, niseme kwamba kuhusu utendaji wa *Marine Services* nina matumaini kwamba tutauweka tena barabarani, tuombe tu Mungu kwamba fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka huu kama Serikali ilivyoelekeza kwamba, zitakuwa *ringfenced*, kweli ziwe *ringfenced* ili ziweze kutumika kwenye ukarabati wa meli hizi na ziweze kuendelea kutoa huduma kwa wananchi wa maeneo hayo ambako zinafanya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu sasa kutumia nafasi hii kumshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Mwakyembe. Nisiseme sana nimwachie na yeye

mambo mengi ya kuja kusema hapa, lakini niseme kwa maneno ya dhati kabisa kwamba, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.  
*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, ameanza kujibu hoja ambazo zilitakikana hapa zipatiwe majibu na sasa natarajia kumwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Lakini kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri, mchana ultolewa mwongozo kupitia Mheshimiwa Zambi akiomba Serikali angalau ifanye kitu fulani na kutoa ufanuzi kuhusiana na mgogoro ambao umekuwa ukijitokeza kwa namna moja ama nyingine kati yetu na nchi ya Malawi kuhusiana na Ziwa Nyasa.

Wakati ule nikiwa nasitisha Shughuli za Bunge, nilikuwa nimetoa maagizo kwa Serikali kujipanga na kuleta maelezo hayo rasmi hapa Bungeni kwa namna itakavyokuwa imewasiliana na Ofisi ya Spika. Lakini Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu alikuwa amesimama ili kupokea maelekezo hayo kwa niaba ya Serikali, halafu atatupa mwelekeo, lakini wakati huo nikiendelea kutoa nafasi nzuri na ya kutosha kwa Serikali kuweza kujipanga vizuri zaidi ili kuja kuliarifu Bunge.

Kwa hiyo, naomba nimpe dakika mbili Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu aweze kuyapokea maelekezo hayo na kutueleza angalau kwa dakika moja ili Serikali iwasiliane na Ofisi ya Bunge na kuweza kutuletea taarifa hiyo ikiwa imekamilika.

### **MHE. SAMUEL J. SITTA- KAIMU WAZIRI MKUU:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii fupi ya kuweza kutoa maelezo kufuatana na hoja au taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Zambi kabla hatujasitisha shughuli pale mchana. Serikali imeshtushwa na tamko la huyo Katibu Mkuu ya moja ya Wizara kule Malawi. Kwa sababu tunavyofahamu sisi majadiliano yanaendelea ya kuweza kupata muafaka kuhusu mpaka wetu na Malawi ndani ya Ziwa Nyasa. Taarifa kamili itatolewa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Membe siku ya Jumatatu. Hali ya majadiliano ikoje na tumefika wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua tu nafasi hii kuwatoa wasiwasi wananchi wa Mikoa ya Mbeya, Iringa na Ruvuma ambao wanagusana na Ziwa hili la Nyasa kwamba, Serikali imekaa vizuri, wasiwe na wasiwasi waendelee na shughuli zao halali ndani ya Ziwa kama ambavyo imekuwa kwa karne kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tuko tayari kwa uchokozi wowote kwa sababu sisi ni nchi ambayo tunafuata Sheria za Kimataifa na tunadhani hali iliyopo sasa isibadilishwe hadi hapo tutakapopata jibu muafaka. Kwa hiyo, wananchi watulie katika mikoa yote mitatu niliyoitaja na Watanzania wote watulie tuko imara na tumesimama vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge basi hiyo ilikuwa ni kauli kutoka kwa Kaimu Waziri Mkuu na kama tulivyopewa hapa maelekezo, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Bernard Membe kwa siku hiyo ya Jumatatu atatupa taarifa rasmi ya mwendeleo na majadiliano na hali halisi katika suala hili. Naomba nimwite sasa Dkt. Mwakyembe ili aweze kuhitimisha hoja yake. Karibu sana Dkt. Mwakyembe.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa leo kukamilisha hoja niliyowasilisha jana asubuhi. Maoni na mapendekezo ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge yanadhihirisha ni kwa kiwango gani Sekta ya Uchukuzi inahitajika kuboreshwa kwa kufanyiwa kazi ya kina ili ifanye kazi yake ya msingi ya kuwezesha sekta zingine za kiuchumi na kijamii kufanya kazi zinazotegemewa na wananchi na hivyo kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi kwa ujumla na wa mtu mmoja mmoja. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa hoja mlizozitoa kwa maandishi na vile vile kwa kuongea napenda kuwahakikishia kuwa maoni yote mliyoyatoa tutayazingatia wakati wa utekelezaji wa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wenzako wa Bunge na Katibu wa Bunge kwa jinsi mlivyosimamia majadiliano yote kwenye Mkutano huu wa Nane kwenye Bunge hili. Vile vile nampongeza kwa dhati kabisa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi na Waziri

Mkuu kwa upeo wake mkubwa unaoshereheshwa na ubinadamu, busara na umakini alionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini pamoja na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mama Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki kwa kusimamia vizuri Kamati yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati hii chini ya uongozi wao mahiri kwa kweli wamefanya kazi kubwa ya kuchambua bajeti ya Wizara ya Uchukuzi na kisha kutoa maoni ambayo yanatupa mwelekeo thabiti katika ukujaji wa sekta ya uchukuzi. Tutaendeleza ushirikiano mzuri uliojengeka kati ya Kamati na Wizara tukiwa na lengo moja tu nalo ni kuboresha na kuimarisha sekta hii muhimu kwa uchumi na shughuli za kijamii za Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa sekta ya uchukuzi, kaka yangu Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini kwa maoni na mapendekezo yake kuhusu bajeti hii. Wakati wa majadiliano ya hoja ya bajeti ya Serikali na ile ya Waziri Mkuu michango ya Waheshimiwa Wabunge iligusia maeneo sita makuu yafuatayo kwenye Sekta ya Uchukuzi:-

Uboreshaji wa miundombinu na huduma za reli, uboreshaji wa viwanja vya ndege, uimarishaji wa usafiri wa anga, uboreshaji na ueendelezaji wa bandari,

udhibiti na uboreshaji wa usafiri wa majini kwenye bahari ya Hindi na Maziwa yetu makuu matatu na uendelezaji wa Chuo cha Bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge 30 walichangia wakati wa majadiliano ya Hotuba ya bajeti ya Serikali, Waheshimiwa Wabunge 21 wakati wa majadiliano ya hoja ya Waziri Mkuu na Wabunge 13 walichangia wakati wa majadiliano ya hotuba za bajeti za Wizara zingine. Wakati wa majadiliano ya hoja ya Wizara yangu tulipokea michango ya Waheshimiwa Wabunge 35 waliyoitua kwa kuzungumza na michango kwa maandishi ni 149. Nawashukuru sana kwa michango yenu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba, Mbunge wa Buchosa ambaye ni Naibu Waziri wa Uchukuzi ameanza kutolea maeleo maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia na naomba niendelee kutolea ufanuzi wa hoja zilizotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kwanza kutolea maeleo yale ya ujumla yakifuatia yale ya Kamati ya Miundombinu na kisha Kambi ya Upinzani na kuhitimisha na Waheshimiwa Wabunge. Shida tu ni muda na nina uhakika muda hautatosha. Lakini naomba kuwahakikishia kuwa tutajibu hoja zenu zote kimaandishi na kuwapa Waheshimiwa Wabunge wote kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Tisa wa Bunge la Jamhuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza na kwa maandishi hapa Bungeni kama ifuatavyo. Kwanza Waheshimiwa Wabunge waliochangia sekta ya uchukuzi kupitia hotuba ya bajeti ya Serikali tarehe 18 mpaka tarehe 27, Juni, 2012 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Kapt. John Komba, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mheshimiwa Sylvester M. Mabumba, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Conchesta L. Rwamlaza, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Naomi M. Kaihula, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe na Mheshimiwa Sabreena H. Sungura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa *Engineer Athuman R. Mfutakamba*, Mheshimiwa Yusuph A. Nassir, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi Suleiman, Mheshimiwa Mohamed Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma, Mheshimiwa Mansoor S. Hiran na Hamad Ali Hamad. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge waliochangia sekta ya uchukuzi kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 25 – 28, Juni ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Mchungaji Luckson N. Mwanjale, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Assumpter N. Mshama, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Vicent Nyerere, Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina, Mheshimiwa Philemon K. Ndesamburo, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Moshi S. Kakoso, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Ismail A. Rage, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Abdulkarim I. Shah, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis na Mheshimiwa Moses J. Machali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge waliochangia Sekta ya Uchukuzi kupitia Hotuba za Wizara mbalimbali ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Dkt. John P. Magufuli, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Kheir Ali Khamis, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Amina A. Clement, Mheshimiwa

Kapt. John Chiligati na Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja yangu kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mheshimiwa Fatuma A. Mikidadi, Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Agustino Masele, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda na Mheshimiwa David E. Silinde.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Dkt. Haji H. Mponda, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed. Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Dkt. Milton M. Mahanga, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Rukia Mohamed, Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari na Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile walichangia Mheshimiwa Vicent Nyerere, Mheshimiwa Nassib Omar, Mheshimiwa *Engineer Athumani R. Mfutakamba*,

Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Amina Clement, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Anastazia J, Wambura, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina, Mheshimiwa Saada Salum na Mheshimiwa Richard Ndassa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mheshimiwa Stephen M. Wasira, Mheshimiwa Sylvester M. Mabumba, Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani, Mheshimiwa Catherine V. Magige, Mheshimiwa Donald Max, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa *Engineer* Gerson H. Lwenge, Mheshimiwa Dkt. Antony G. Mbassa na Mheshimiwa Susan L. Kiwanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wapo Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Mheshimiwa Alphaxard Kange Lugola, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Israel Natse, Mheshimiwa Rachel Mashishanga, Mheshimiwa Augustine Mrema, Mheshimiwa Vick Kamata, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Gregory Teu, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad na Mheshimiwa Selemani Zedi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Mcemba, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu

Abama, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Anna MaryStella J. Mallack, Mheshimiwa Naomi M. Kaihula, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa James F. Mbatia na Mheshimiwa Desderius Mipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna Mheshimiwa Paulina Gekul, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Omar Nundu, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Salum Barwany, Mheshimiwa Tauhida Galos Nyimbo, Mheshimiwa Dkt. Hussein A. Mwinyi, Mheshimiwa Thuwayba Idris Muhamad, Mheshimiwa *Engineer* Ramo Makani, Mheshimiwa Abdallah Sharia, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani na Mheshimiwa Jerome D. Bwanausi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Joyce J. Mukya, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Albert O. Ntibaliba, Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Mheshimiwa Innocent E. Kalogeris, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Mustapha H. Mkulo, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo na Mheshimiwa Agripina Z. Buyogera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wapo Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Cecilia Pareso, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Seleman Jafo, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, Mheshimiwa Abdulsalaam S. Amer, Mheshimiwa Angellah J. Kairuki, Mheshimiwa Zaynab M. Vullu na Mheshimiwa Agustine L. Mrema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mheshimiwa Moza Abeid Said, Mheshimiwa Iddi M. Azzan, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mheshimiwa Tundu A. Lissu, Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Mheshimiwa Profesa Kalikoyela Kahigi na Mheshimiwa William Ngeleja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja yangu kwa kuzungumza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Charles J. Tizeba, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Kheir Ali Khamis, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Hasnain M. Murji, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa,

Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Agustino M. Masele na Mheshimiwa Sabreena H. Sungura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, Mheshimiwa Musa Haji Kombo, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mheshimiwa Omar R. Nundu, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Naomi M. Kaihula, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Dkt. Faustine E. Ndugulile, Mheshimiwa *Engineer* Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Tundu A. Lissu, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana W. Kikwembe, Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani, Mheshimiwa Salum Khalifan Barwany, Mheshimiwa Anna MaryStella J. Mallack na Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitoe maelezo ya kijumla ambayo yalijitokeza wakati wa majadiliano ya hoja yangu kwa kuanzia na usafiri wa njia ya reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa usafiri kwa njia ya reli hauridhishi kwa sababu tuna safari mbili tu kwa wiki za treni kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma wakati mahitaji kwa kweli ni makubwa mno. Aidha, mizigo ambayo inasafirishwa kwa reli kwa sasa ni chini ya asilimia tano. Hii sio tu kwamba hairidhishi bali hata kwangu mimi ni hatari kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba tukumbuke kwamba usafiri wa treni kati ya Dar es Salaam na Kigoma ulisitishwa karibu miezi sita kutokana na matatizo mbalimbali ikiwemo uchakavu wa miundombinu, injini za treni na athari za mvua kubwa zilizonyesha maeneo ya Kilosa, Morogoro na Gulwe, Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua tulioichukua mwezi mei mwaka huu ya kurejesha treni za abiria na kuongeza treni za mizigo ni ushahidi tosha kuwa Serikali sasa imedhamiria kuupa msukumo mpya usafiri wa treni. Lengo la Wizara ya Uchukuzi ni kuhakikisha kuwa, tunakuwa na treni ya abiria kila siku kutoka Dar es Salaam sio tu Kigoma bali pia Mwanza na maeneo mengine. Tumejipanga kufikia lengo la angalau treni nne kwa wiki kwenda Kigoma na Mwanza kufikia mwezi Juni 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu likipitisha Bajeti yetu hii leo na Sekta ya Uchukuzi ikapata kipaumbele katika mapokezi ya pesa kutokana na muda mrefu wa kusubiri vipuri adimu yaani *lead time*. Aidha, tumejipanga kuongeza wingi wa mizigo itakayosafirishwa kwa treni ili kupunguza gharama za ujumla kwenye uchumi kwa kuwa usafirishaji au uchukuzi kwa njia ya reli ni wa gharama nafuu na salama kuliko njia nyingine zozote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia malengo haya *TRL* ilianza kuvifanyia matengenezo makubwa vichwa vyatreni vinne mwezi Mei, 2012 na tarehe 30 Julai, 2012

mnakumbuka baadhi yenu mlisoma magazeti nilikizindua kichwa kimoja na vingine vitatu vitakamilika kabla ya Oktoba, 2012. Lengo ni kivifanyia matengenezo na kuvijenga upya, vichwa 23 vya treni na uwezo huo tayari umeoneshwa na wafanyakazi wa *TRL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimeuagiza uongozi wa *TRL* uangalie uwezekano wa kupunguza idadi au kuachana kabisa na mpango wa kukodisha vichwa vya treni kutoka nje ya nchi kwa gharama kubwa na badala yake fedha hiyo tuitumie kwa ajili ya ukarabati wa vichwa vyote vinavyoweza kutengenezeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana kuwa uwezo wa kusafirisha mizigo utatoka ulipo sasa wa wastani wa tani 250,000 tu kwa kutumia vichwa kumi tulivyonyavyo kwa mwaka hadi kufikia tani 575,000 kwa kutumia vichwa 23. Aidha, Serikali kupitia *TRL* ina mpango wa kununua vichwa vipyta vya treni 13 kufikia mwishoni mwa mwaka 2014. Vichwa hivi vitaongeza uwezo wa *TRL* kubeba mzigo kufikia tani 850,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali ni kwamba, kumekuwepo na juhudini kubwa za kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa kuharibiwa kwa reli katika maeneo ya Kilosa hadi Gulwe. Kazi iliyofanyika ni kubwa sana hata kwa kuiangalia kwa macho. Lakini kumekuwa kuna malalamiko kutoka kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa kwa maandishi na wengine hata tukikutana nao kuhusu utumiaji wa *force*

*account* katika urekebishaji wa eneo hilo kwa kipindi chote cha mwaka 2010/2011. Hoja ni kwamba, katika hatua fulani zabuni zingeweza kutumika kwa kazi ambazo hazikuwa na uharaka wa kuhitaji matumizi ya *force account*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuwa fedha yao haikutumika vibaya, ilitumika kutengeneza njia hiyo na fedha imetumika sawa na thamani ya kazi yaani *value for money*. Nilishamwagiza *Controller and Auditor General* mapema mwezi Juni, 2012 kufanya ukaguzi wa fedha zilizotumika kujenga reli hiyo kwenye maeneo husika na kutupa mapendekezo namna ya kuendelea na kazi hiyo pale tatizo kama hili litakapojitokeza tena baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya Wabunge hususan Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, Mheshimiwa Sungura, Mheshimiwa Kafulila na wengine sitawataja kwa sababu muda niliopewa ni mfupi kwamba, Tanzania tunatia aibu kabisa kwa kuwa na ndege moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata leo asubuhi nimemwona Mheshimiwa Kafulila akiongea kwenye televisheni kuwa tunatia aibu na tunadharaulika sana duniani kwa kukosa ndege. Pamoja na kwamba siyo suala hili tu, lakini maoni mengi ya Waheshimiwa Wabunge hayakuzingatia yaliyomo kwenye Hotuba yangu pengine kwa sababu mlisajiaandaa kuyasema.

Kwa hiyo, lazima yasemwe hata kama yamesahihishwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna hata mmoja aliyeweza kusema Mheshimiwa Waziri amesema mnanunua ndege mbili mwaka huu ambacho ni kitu kikubwa. Lakini hakuna anayegusia. Ni ileile hoja moja, hoja au suala la kudharaulika. Sidhani kama ni kweli maana hata sisi wengine tunasafiri na bado tunatembea kifua mbele kama Watanzania na tunaheshimika sana. Sasa lisije likawa tatizo lako wewe mwenyewe, umekwenda kwenye semina ya Wabunge nje ya nchi, umevaa suti chini una raba nyeupe. Nani atakusogelea? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye unalalamika kuwa unadharaulika kwa sababu ya ndege. Hakuna cha ndege hapa, ni wewe mwenyewe. Unafika kwenye mkutano wewe kazi kulalamikia tu, huna *constructive ideas* nani atakusogelea baadaye? Ooh wanandidharau kwa sababu tuna ndege moja! (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wenje naomba uzime *microphone* yako.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungukwa na nchi nyingi tu hapa. Uganda hawana *national airline*; Zambia ndugu zangu hawana; hata Burundi jirani na Rwanda wote hawana, lakini wanatembea kifua mbele! Nawaomba Waheshimiwa Wabunge kupanga ni kuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika kama Serikali yetu ilitaka tuwe na *Boeing* 50 hapa za kujivunia, tusingekuwa na barabara kutoka Tunduma mpaka Arusha mpaka mpakani kwa lami. Kupanga ni kuchagua. Halafu tunalinganishwa na nchi ndogo sana ambayo hata Mheshimiwa Magufuli alisema kwa lami hii kidogo tuliyonayo, Rwanda watakosa hata mashamba ya kulimia kwa sababu pote patajaa lami. Kwa hiyo, niseme tu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme hilo, halafu niende usafiri kwa njia ya maji. Kwa ajili ya kutoa mchango unaotakikana kwenye uchumi wetu naizungumzia Bandari. Hapa Wizara inawahakikisha kuwa kwa kweli italiangalia kwa makini sana suala la mizigo bandarini, kwamba tatizo hili linaondoka kabisa. Kwa kweli linakera kuona kuwa Tanzania ni moja ya nchi chache sana katika bara la Afrika zenyewe Bandari zinazohudumia makontena kwa siku nne au zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni aibu na haivumiliki. Kwa sababu imeshakuwa kama donda ndugu hivi. Lakini naamini hili si donda ndugu ni kaupele tu kanahitaji kutobolewa, kutumbuliwa na mambo yaende. Tumejipanga kuondokana na kero hii kuhakikisha kuwa tunaboresha miundombinu iliyopo na pia kuijenga mingine ili kukidhi mahitaji ya huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, baada ya kuondoa ukiritimba wa kuhudumia makontena kwa kweli tumejipanga kuongeza ushindani kati ya watoa huduma na kuleta tija kubwa na ufanisi ambao

utapunguza sana muda wa ucheleweshwaji wa mizigo bandarini na hivyo kupunguza gharama kwenye uchumi wa nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa gati namba 13 na 14, Waheshimiwa wameliongelea sana. Umezua mjadala mzito kuanzia kwenye Mkutano wa Bunge la Saba na mpaka Mkutano huu. Bunge hili lilituagiza na Wizara imetekeleza. Tuliagizwa *specifically* kuwa nenda mkajiridhishe, nenda mkahakiki. Lakini mjadala ulioko humu ndani, Wabunge wengi wanalamika kuwa tunachelewesha tu miradi kwa kufanya upembuzi yakinifu na kadhalika, maana ni utambi tu unageuka, wakati ni nyie wenyewe mmetukwamisha tuisogee mbele. Mnatuambia hapana kuhakiki, tumefanya uhakiki! Tungetumia kampuni moja pale mjini Dar es Salaam tukasema tumehakiki, mngekataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilibidi tutafute kampuni ya Kimataifa ambayo imefanya uhakiki. Sasa tunarudi na jibu kuwa tumehakiki, lakini mjadala unaoendelea sasa hivi hamuoni hilo. Naambiwa kimetokea nini na ni kampuni ipi itajenga. Nashauri Bunge hili liiachie Serikali itekelleze ujenzi wa magati haya ambao utanza ndani ya mwaka huu wa fedha. Kwa sababu kama Bunge litashikiza namna ya kutekeleza mradi huu, nani awajibike ikivurugika? Basi tuwe tayari kuwajibika maana wote tumehusika! Tuachenii tutekeleze huu mradi mmeshatupa kazi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Miundombinu imeagiza ujenzi wa *multistorage car park* katika Bandari ya Dar es Salaam kwa kuitaka TPA kwa kutumia vyanzo vyake yenyewe. Kwa kufanya hivyo, bei ya ujenzi itapungua na mapato yote yatokanayo na jengo hilo yatatumika vizuri. Lakini Wizara haikufurahishwa na suala hilo kwa sababu mbili naomba niwe mkweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu ulikuwa ghali sana. Kujenga jengo tu la kupaki magari billioni 58! Tukasema hapana. Mradi wenyewe ni wa ubia na kampuni moja kutoka Mombasa. Tukasema mradi mdogo kama huu unahitaji mbia kweli? Kwa hiyo, mimi na wenzangu tukasema hapana. Huu ubia kwenye vitu vidogo vidogo kama hivi haiwezekani. Mamlaka ya Bandari inaweza kufanya yenyewe kama ambavyo imeshauri Kamati yetu ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nina sababu ya pili. Waheshimiwa Wabunge naomba mnielewe kuwa bandari jukumu lake kubwa siyo kuhifadhi mizigo ni kupitisha mizigo. Nisingependa tuanze ku-*encourage* mizigo ikae kwa kujenga jengo la kuweka mizigo pale. Kama yule mtu wa Mombasa bado ana *interest* ya kuhifadhi magari, naomba atafutiwe kiwanja nje ya bandari ajenge! Ni ruksa, ni uchumi huru Kifungu cha 42(1) cha Sheria ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya Ushuru na Forodha kinataka mizigo uliokaa bandarini kwa zaidi ya siku 30 bila kuchukuliwa upigwe mnada baada ya tangazo la siku 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku tunajenga jengo la ku-*encourage* mzigo ukae zaidi! Kwa hiyo, naomba hili mtuachie, ni suala la utekelezaji! Mtuachie na mniachie Waheshimiwa Wabunge, ndugu yenu niko pale nitalitekeleza. Mwaka kesho nitatoa ripoti nzuri tu, Mungu yupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri kwa njia ya barabara nao ni muhimu katika kuwezesha huduma za kijamii au kiuchumi. Hata hivyo, Mheshimiwa Kabati alizungumzia suala moja zito sana, mimi naliona ni zito. Waafrika hususan sisi Watanzania, tunatambulika duniani kote na kwa wageni wanaokuja hapa, kwa utamaduni usiotetereka wa kuheshimu usiri wa mwili wa mtu hasa mtu mzima, hata kitu ambacho ni cha kawaida sana. Kwa wenzetu, hasa Wazungu kuvaa nguo za ndani na kuogelea mbele za watu hapa kwetu mabinti zetu hawawezi! Wamelelewa tofauti, yaani ndiyo utamaduni wetu, usiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu hata laana kubwa hapa kwetu inatokea pale mama yako akisema nitakuvulia nguo. Hii ni kwa sababu mwili wa mama ni *sacrosanct*, siyo kitu cha mchezo, ila sijasikia madhara ya baba akivua nguo, ila mama ni hatari kweli. Lakini nasikitika utamaduni huu, maadili haya hupotea mara tu tukishaingia kwenye mabasi. Basi linasimama tuchimbe dawa heshima yote hupotea! Hapo mzee mzima anapeana mgongo na katoto ka miaka sita, kila mtu anafanya kazi yake upande wake! Mama mwenye heshima yako pale pembedi na katoto kadogo au watoto wa kiume! Kufanya hivyo ni kudhalilisha utu wetu Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge mlioliongelea suala hili. Nafikiri huu ni udhalilishaji na hatuwezi kuendelea nao. Nachukua fursa hii kuagiza leo hii kwamba kuanzia tarehe 1 Septemba, 2012, basi lolote la abiria litakalokutwa limesimama eti kwa kuchimba dawa litapewa onyo la kwanza, mnasema mtakwenda Mahakamani, nitawashinda. Mara ya pili tutakupiga *fine* na mara ya tatu tafuta biashara nyingine, tunakufutia leseni yako, heri utafute biashara nyingine unaweza kwenda kokote kule. Tumechoka kudhalilisha utu wetu sisi wenyewe.

**MWENYEKITI:** *Order, order, order!* Waheshimiwa Wabunge tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe radhi kama kuna baadhi ya wenzetu hapa wana mabasi, lakini hiyo ndiyo kazi inakuja kuanzia tarehe 1 Septemba, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamelalamikia uongozi mbovu ulio *TAZARA*. *TAZARA* kuna uongozi mbovu sana, nakubaliana kabisa na Waheshimkiwa Wabunge (*Makofi*).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri samahani, Waheshimiwa Wabunge ningeomba utulivu sijui hii minong'ono ni kwamba kuna watu bado wanapenda kuchimba dawa iendelee? Naomba tutulie Mheshimiwa Waziri amejibu na ataleta utaratibu wake Mheshimiwa Waziri naomba uendelee.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo halina wasiwasi litatengenezewa utaratibu na litafanyika kuanzia tarehe 1 Septemba, 2012 na huo ndiyo utamaduni wa Tanzania. Hili suala la TAZARA Waheshimiwa Wabunge wanasesma hiyo Sheria hapa tuibadilishe, naelewa hasira yenu na naelewa hamasa ya kutaka TAZARA ibadilike, lakini nataka kutoa tahadhari moja tu kuwa hatuwezi kubadili chochote kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu tunafungwa na Kanuni na Sheria ya Kimataifa ya *Pacta Sunt Servanda* kwamba tuheshimu Mikataba ambazo tumeingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii TAZARA mnayoiona imeundwa au iko pale kutokana na mkataba wa Kimataifa. Ni zao la *treaty* kati ya nchi mbili Tanzania na Zambia na ndiyo maana inabidi turudi tena *as partners* tuongee. Kwenye hotuba yangu Waheshimiwa Wabunge nimeshasema kuwa, tumeshakaa kama Baraza la Mawaziri, tumekubaliana kupitia upya Sheria hii ambayo inaunda TAZARA. Tuwe na subira tuache hii fursa marekebisho yafanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa Kamati ya Miundombinu ametuambia kuhusu ATCL kuwa, imekuwa ikiendeshwa kwa matatizo kwa muda mrefu na Serikali imekuwa ikiwekeza fedha nyingi bila mafanikio na ametutaka tuwe na msimamo kuhusu ATCL na Bunge lielewe ni wapi tunaelekea. Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea hili suala, nataka niseme kuwa Serikali inatambua

umuhimu wa kuwa na Shirika la Ndege imara litakalochangia katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Serikali ni kwamba Serikali itaendelea kulisaidia Shirika hili la Ndege ili liweze kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi. Tuwape *opportunity* kama nilivyosema na tayari nimeteua Bodi mpya ambayo nategemea itakuja na *management* ambayo inakwenda na kasi inayotakiwa. Kwenye bajeti yetu tumetenga pesa kuisaidia ATC iweze kunyanyuka na nimewapa muda wa miezi mitatu wanilettee ripoti. Umebakia muda mchache wataniletea taarifa wamefikia wapi, kwa sababu hatutaendelea kuibeba *ATCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea sasa hivi kama Serikali kutafuta Mbia wa kuaminika na nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Mwenyekiti kuwa safari hii *partner* tutakayempata atakuwa mzuri kutakuwa na uwazi kupita kiasi katika kuangalia mkataba maana tumeingizwa mikenge mara nyingi sana. Lazima tujivunie kama Watanzania kuwa tume-*create a very good enabling environment*. Hivi jamani tungakuwa na mazingira magumu nchi hili majitu kama *Precision Air* yangefumuka na kuwa *Airline* ambayo inaheshimika katika sehemu kubwa ya Afrika? Yote haya ni mafanikio ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetokea hoja kuwa tumetoa pesa kidogo kwa *TMA* na upo wasiwasi kama fedha itatolewa kweli ambayo tumeitaja 3.8 bilioni! Nataka kusema kuwa hakuna haja ya kuwa na

wasiwasi kama fedha itatoka au la! Kwa sababu mwaka wa fedha ambao unakwisha sasa tulitenga shilingi billioni 3.481 kwa ajili ya *TMA* na nataka kuwahakikishia leo kuwa mamlaka imeshapokea fedha yote hiyo! Nadhani Waheshimiwa Wabunge wengi mnaangalia mapokezi ya fedha mpaka mwezi wa Nne lakini kwa kweli sisi tunahesabu mpaka mwisho wa mwaka wa fedha wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Serukamba na Mheshimiwa Dkt. Ndungulile mmeongelea sana suala la Vijibweni. Nataka kueleza kuwa Mamlaka ya Bandari iliomba eneo la ziada kwa ajili ya upanuzi wa bandari tumepata eneo la Vijibweni toka mwaka 2009, na tumeahidiwa kupewa hekari 112 na hilo eneo limetengwa kwenye Kigamboni *Master plan*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kuonesha *seriousness* ya Mamlaka tumetoa shilingi milioni 145 mapema mwaka jana ilikuwa Januari mwaka 2011, kama gharama za upimaji na uthamini. Hivi sasa Mamlaka inasubiri kuambiwa tu kiwanja ni chenu na nawahakikishia pesa ya fidia tumeshaiandaa! Mheshimiwa Ndugulile wapiga kura wako watapata fidia bila wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kwamba, bandari ya Mtwara iboreshwe. Mheshimiwa Barwany ndugu yangu akasema Lindi tumeisahau. Naona nijibu kwa pamoja, nimeelezea vizuri sana kuhusu Mtwara. Kwenye hotuba yangu, kifungu namba 66-67 ukurasa wa 41-42, nimelielezea vizuri sana suala zima na siyo timu ya Watendaji ambayo ipo kusimamia hilo suala,

bali vile vile tumeunda Kamati ya Mawaziri. Nakaa mimi na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshakaa nao vikao viwili na tunakaa tarehe 6 au 7 kuangalia uwezekano wa kuweka *deadline*, mwezi huu kwa sehemu ya Bandari ya Mtwara, bandari huru. Ndugu yangu Barwany nakuomba uniamini, hatujaisahau Lindi. Umeongea kwa uchungu sana ndugu yangu, lakini umekaa hapa Bungeni muda mrefu unaelewa kabisa kuwa mwaka jana tumekutengea fedha na mwaka huu tumetenga fedha siyo fedha ya kujenga ni fedha ya maandalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza kwa kutoa mchanga, bandari ya Lindi ina mchanga sana. Mwaka wa fedha uliopita tumetoa shilingi milioni 900 na mwaka huu tumeweka milioni 400 kumalizia utoaji wa mchanga na tukishatoa mchanga tunaanza kazi ya kupanua gati. Hii siyo *theory*, tumeshatangaza *tender* na tayari zabuni zimefunguliwa kumpata mkandarasi wa kupanua hiyo gati ya Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na hoja kuhusu *SPM*, lile boyo kuu la kupakulia mafuta linakamilika mwezi Agosti mwaka huu na tutawatolea taarifa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo na Mwambani uharakishwe kwa kifupi, ni kuwa utekelezaji wa Bandari ya

Bagamoyo uko katika hatua ya kutathmini eneo kama nilivyoeleza katika kifungu cha 69 cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bandari ya Mwambani usanifu tulishamaliza kama nilivyosema. Tuna pesa ya kuwalipa wananchi fidia kuanzia mwezi Septemba na siwezi kuwa nimetoa ahadi mbele ya Bunge hili na isitekelezwe itakuwa ni aibu sana nikirudi na kusema bado haijalipwa. Kwa sababu ya muda siwezi kuelewa umeanza saa ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya kwamba mizigo mingi inakwepa Bandari ya Dar es Salaam inapitia Mombasa, tunachukua hatua gani. Tumelieleza sana hili Serikali kwa kuliona hili imeandaa mikakati madhubuti na mojawapo niwaeleze kuwa hivi karibuni mmemwona Mheshimiwa Waziri wa Nchi Dkt. Mary Nagu akizindua *one stop center* pale Bandari ya Dar es Salaam ambapo tutakusanya wahusika wote wawepo pale badala ya mtu kuhangaika na *documents* huku na kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TICTS* nao ambao nimekuwa nikiwaambia waoneshe mabadiliko ya kuwa na vifaa zaidi kwamba wana vifaa tayari wametengeneza reli mpya na wamefunga *crane* mpya ya kupakia na kupakulia mizigo na sasa hivi wanasubiri mtambo mkubwa zaidi, mimi ninaziita zote *crane* wao wanaita *RMG*. Pia RAHCO wanaendelea na matengenezo ya njia kwa kutandika reli nzito na tumeamua kuwa na *extension* ya sehemu ya kutunzia mizigo Kisarawe na tunaendelea na hiyo *process* ambayo tuko pamoja na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeunda *taskforce* katika Wizara yangu hili liko katika hotuba yangu. Ndiyo maana nasema mengi yameongelewa bila kusoma hotuba yangu ambayo inanishauri je, niunganishe Mamlaka ya Bandari na reli ili iweze *function* vizuri ama tuziache hivi hivi? Maana kuna kitu kinaonekana kama kinakosekana pale. Ushauri utakuwa ni wa kitaalam na tutawafahamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge niseme wote, mmesikitishwa, kama nilivyosikitishwa na ajali ya *M.V. Skagit*. Tumepoteza Watanzania wengi sana. Ni mchawi tu ndiyo atakuwa hajashtuka, wote imetushtua. Mimi nilikuwa Zanzibar lilipotokea. Hili suala kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamechukia sana, wanataka Waziri wa Uchukuzi ajiuzulu. Nataka hili niliongelee kidogo ingawaje sikutaka kuliongea kwa sababu tatu kuu.

Kwanza, Rais wa nchi Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete amelielezea vizuri sana jana jinsi lilivyotokea hatua zinazochukuliwa na maagizo aliyotupa kuweza kuhakikisha vitu kama hivyo havitokei tena, uundwaji wa vikosi vya uokoaji na kazi tuliyonayo ya kumalizia maandalizi ya Sheria na kuiwasilisha Baraza la Mawaziri ili mwezi Februari tuwe hapa kuweza kujadiliana kuhusu Sheria ya Uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Rais wa Zanzibar ameshaunda Tume kuchunguza kwa undani kitu gani kilitokea. Ingawa kulikuwa na kejeli hapa ohh,

zinaundwa Tume tu hazina maana! Mimi nadhani hamkusoma ripoti iliyopita. Watu wamepelekwa Mahakamani, *Zanzibar Maritime Authority* wamepewa sura mpya kabisa, wote waliolaumiwa wameondolewa pale. Ndiyo hatua hizo za kupata ukweli. Napata shida kuanza kuingia ndani kuliongelea suala hili. Nahodha wa meli, Mmiliki wa Meli, Ajenti wa meli, walishatiwa mbaroni na naambiwa kwamba *process* za kisheria zimeanza. Lakini Wabunge mmeongea sana na wananchi wanapata hisia kwamba pengine mtu mkorofi pale atakuwa ni Mwakyembe na Wizara yake ya Uchukuzi, kwa sababu ni rahisi sana kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubaya wake nina tatizo moja; nisiposema ukweli huwa naugua. Imekuwepo *tendency* kwamba *it is ok*, Mbunge kutoka Zanzibar kulalamikia kuhusu masuala ya Muungano, lakini anayetoka Bara kulalamika ni *taboo*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo nashindwa sasa maana kesho inaweza ikapotoshwa zaidi na zaidi. Hivyo, naomba tu niseme kidogo sana kieleweke. Kwanza nataka niwathibitishie Wabunge kwamba kujiuzulu ni kitendo cha heshima sana. Ndiyo maana nashangaa baadhi ya watu anajiuzulu halafu wanaendelea kulalamika. Hapana! Ukijiuzulu *una-take political responsibility*, ni heshima. Kwa hiyo, hata mimi ile ni heshima kubwa, lakini misingi ya kujiuzulu kwenye hili nataka kuwaeleza kwamba haipo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine nisisitize kidogo kwa sababu wengi hapa ni vijana, msingi wa kujiuzulu

una historia yake nchi hii na unatoka kwenye Mwongozo wa CCM. Mwongozo unasema kukosoa, kujikosoa na kukosolewa ni ngao ya Mapinduzi. Ndugu zangu kutokana na hilo tumejenga a *Constitutional Convention*, ni utamaduni wa kikatiba ambapo Kiongozi akikosea anawajibika kwa kujiuzulu. Lakini awe na madaraka, ameshindwa kuyatumia vizuri, awe na madaraka hajayatumia au ameyatumia vibaya kwa kuingiza maslahi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niseme kwamba kabla ya mwaka 2006 tulikuwa na sheria moja kama Taifa ya Usimamizi wa hii shughuli ya majini. Naielewa hii vizuri zaidi kwa sababu nilihusika hata kuipeleka sheria hiyo Zanzibar, wakati huo chombo haikuwa *SUMATRA*, kilikuwa Tanzania *Central Freight Bureau*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hicho naiingiza sheria hiyo Zanzibar, nilikuwa Mkurugenzi wa Bodi ya Wakurugenzi ya *TCFB* na naomba ku-declare hapa ukweli kwamba ni mimi niliyekutana na Waziri wa Mawasiliano wakati huo Mheshimiwa Rais Mstaafu Aman Abeid Karume. *The first thing* nilimwambia, Mzee hii ni kitu *very important* kikaingia Zanzibar. Niseme tu kwamba mimi nina *institutional memory* ya hiyo kitu. Baadaye *SUMATRA* ikaja Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2003 tukatengeneza sheria ambayo ndiyo ilikuwa inatumika kote katika Taifa zima, *Merchant Shipping Act*. Sheria hii ilikuwa imesheheni uzoefu mbaya tulioupata miaka

kadhaa iliyopita kutokana na ajali ya *M.V. Bukoba*. Ukiisoma sheria hii inasema hatutarudi kule, sijui kama mnanielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya *Merchant Shipping Act, 2003*, ilivyowekwa inasema haturudii ng'o ya *M.V. Bukoba*, lakini mwaka 2006 Serikali ya Zanzibar ikasema hatuitaki *SUMATRA*. Sasa ndiyo nasema kwamba mamlaka yangu yanaishia Chumbe, na ndiyo mnafurahia sana hiyo *statement*. *SUMATRA* wakaondolewa, ikaundwa Sheria mpya ya *Maritime* ya Zanzibar na mwaka 2009 ndiyo ikaundwa Zanzibar *Maritime Authority* kama *SUMATRA* kusimamia masuala ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ninachokisema ni kwamba, napenda kumpongeza sana Waziri mwenzangu Masoud kwa kujuzulu. Lakini mimi ni mkweli nasema kuwa nadhani amechelewa kidogo, alitakiwa ajiuzulu wakati wa *M.V. Spice Islander. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu alisimamia mchakato huo wa sheria wakati inabadilishwa kutoka kwenye sheria iliyokuwa *very strict* kwenda kwenye sheria ambayo iko *loose*. Nataka nieleze maana mimi ninazo sheria hapa. Maana naogopa nikikaa kimya itaendelea kuwa hadithi magazetini na kutusema watu ovyo. Nataka hizi *facts* muwe nazo kama Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ilisukwa ili kuzuia tusirudi kule. Sheria inasema kwamba; moja, hatusajili

meli yoyote kwa usajili wa kwanza ambayo imezidi umri wa miaka kumi na tano, *that is very strict*. Hatusajili meli yoyote ambayo hakuna Mtanzania humo ndani mwenye hisa asilimia zaidi ya hamsini na moja na ndiyo maana toka uhuru mpaka leo *registry* ya *Mainland* ina meli mia moja tu. Nafikiri niishie hapo. Haya yote yaliondolewa kwenye sheria za ZMA. Hata meli iliyochoka inapewa usajili mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikutaka kwenda huko kwa sababu kuna kitu kinachunguzwa ningeweza kusema acha waendelee! Lakini ninachotaka Wabunge naomba tuheshimu maamuzi ya Serikali, naomba tuache hizi shutuma za juu juu. Mimi chini ya Sheria ya Zanzibar *Maritime Authority*, uwezo wangu mwisho ni Chumbe, sina sauti hata kupata *documents*. Hata taarifa kwamba Zanzibar *Maritime Authority* wamesajili meli 399 za nje nimezisikia juzi. Sina *document* hata moja kama Wizara; nitapewaje sina mamlaka? Kwa hiyo, Wabunge sijiuzulu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashindwa sijui nishike lipi maana mambo yapo mengi. Ningetamani tubadilishe Kanuni nipewe kama siku tano maana mambo ni mengi. Nimalizie kwa kusema kuwa bajeti yangu ya Wizara mwaka 2012/2013 ni bajeti ya kuifufua sekta ya uchukuzi, naomba niwahakikishie hilo. Ninawasihi Wabunge muiunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa Wabunge wana nia nzuri sana kusema bajeti ndogo, lakini mimi ambaye nipo huko jikoni, nasema inanitosha. Nitoe

mfano mdogo tu, hii sekta ilikuwa *ICU*. Ni kama mcheza mpira yupo *ICU*, anapoanza kupata nguvu kidogo huendi kutenga sasa bajeti ya kununua mipira, kocha unamtafuta. Unatafuta tu pesa ya kwanza ya kupata mtori apate nguvu polepole. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ninachohitaji mimi. Leo hii ukinipa mabilioni ninunue vichwa vya treni, nitashindwa kupitisha kwenye reli hii kwa sababu baadhi ya madaraja hayaruhusu kupitisha *axle weight* zaidi ya 13.7 *tonnes*, vitaishia tu pale bandarini. Naomba mnipitishie hii bajeti ndogo, mtaona mambo yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa wale wasiomfahamu, huyu ndiye Dkt. Harrison Mwakyembe. (*Makofi*)

Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Harisson Mwakyembe mwenye dhamana ya Uchukuzi na sasa umetoa hoja ili Bunge liingie kwenye hatua inayofuata, hoja hiyo imeungwa mkono na baada ya hoja hiyo kuungwa mkono sasa nitamwita Katibu atuongoze kwenye hatua inayofuata. Katibu!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Sasa Bunge linaingia kwenye Kamati ya Matumizi ili kuweza kupitisha mafungu yaliyoombwa kutumiwa na Wizara hii.

### **KAMATI YA MATUMIZI**

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **FUNGU 62 - Wizara ya Uchukuzi**

Kif. 1001 Admin. & HR. Management... ... ... Sh.  
2,009,544,400/=

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ukarasa 43 kuhusu ujenzi wa magati mwambao wa Ziwa Tanganyika kwamba utakamilika...

**MWENYEKITI:** Fungu gani Mheshimiwa Kessy?

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 43 kwenye hotuba ya Waziri.

**MWENYEKITI:** Fungu gani kwenye kitabu tunachoendelea nacho?

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Fungu gani?

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 1100. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kessy hebu jiandae kidogo halafu nitakuita baadaye kidogo.

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshajiandaa na kitabu cha Waziri hiki ninacho. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu endelea.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana. Fungu 1001, Mshahara wa Waziri.

Katika mchango wangu wa maandishi na vile vile mchango wangu wa kuongea, niliomba kupatiwa majibu kwa maswali yafuatayo ambayo nahitaji majibu hapa sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge ni swali moja tu, kwa mujibu wa Kanuni hapa unauliza kitu kimoja tu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maswali yanayohusu kitu kimoja, tusvurugane hapa, ni maswali yanayohusu kitu kimoja. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu, naomba unielewe hicho kitu kinachoulizwa kinatakiwa kuwa kitu kimoja sasa ukisema una maswali matatu yanayohusiana na kitu kimoja...

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti ni jambo moja.

**MWENYEKITI:** Kama ni jambo moja sawa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuambiwa kuhusiana na meli zilizopata ajali M.V. *Spice Islander* pamoja na M.V. *SKAGIT*, zilifanyiwa ukaguzi na *SUMATRA* kwa vile zilikuwa zinabeba abiria na mizigo kutoka bandari za Bara? Zilifanyiwa lini ukaguzi huo na matokeo ya ukaguzi huo kama upo, yalikuwa yanasema nini?

**WABUNGE FULANI:** Ahaaa!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dakika tano, hizi kelele za ahaa, ahaa! ni za watu wasiojua Kanuni.

**MWENYEKITI:** Wewe ongea na mimi.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na nilikiri katika mchango wangu wa maandishi na wa maneno kwamba masuala ya uchukuzi siyo masuala ya Muungano. Nakubaliana na Waziri kwamba siyo masuala ya Muungano mpaka wake ni Chumbe, lakini inapofika meli zinakuja kwenye bandari za Bara zinabeba abiria, zinabeba Watanzania kutoka Bara, Waziri hilo suala linakuwa chini ya mamlaka yake kwa kupitia *SUMATRA*. Kwa hiyo, Waziri hawesi akakwepa hili, kama *SUMATRA* haikufanya ukaguzi kwa hizi meli ambazo zinakuja kwenye bandari zetu anawajibika moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya maswali yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri utaratibu ni swali moja kwa kila Mbunge, hata Mbunge akibebesha maswali matatu utaratibu ni swali moja.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Tundu Lissu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi meli *M.V. SKAGIT* na *M.V. Spice Islander* hazikuweza kufanyiwa ukaguzi na *SUMATRA* kwa sababu wao siyo mamlaka yao ya usajili. Inapokuja meli kusajiliwa kwako unafanya *thorough* ukaguzi na ukaguzi huo ndiyo unakupa dozi hiyo ya meli kuweza kuikagua, upande wa kushoto unakuta kuna hiki na kingine. Inapokuja bandarini hapa wanakuja na *document* ambayo tayari imefanyiwa ukaguzi na *Zanzibar Maritime Authority*, wewe ni kufuatilia tu huna mamlaka zaidi kwa sababu huna *data* kuhusu hiyo meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimwambie tu Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba *SUMATRA* haijawahi kufanya hicho na kitu cha kuzingatiwa hapa ni kwamba, ilipoanzishwa Zanzibar *Maritime Authority* na usajili ukaanzishwa Zanzibar, meli nyingi zilizokuwa zimesajiliwa Bara ambazo zinamilikiwa na Wazanzibar zikahamia kwenye *registry* ya Zanzibar na kujisajili upya.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGWALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nina swali dogo tu la kuomba ufanuzi kwa Waziri, kwamba wawekezaji kwenye Sekta ya Madini wanapokuja kuwekeza hapa kwetu wanajenga viwanja vyao vyao ndege kwa ajili ya kusafirisha rasilimali wanayovuna katika ardhi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, pale Nzega kuna Kiwanja cha Ndege ambacho kimekuwepo kwa miaka mingi sana *a small air strip*, ni kwa nini wawekezaji wa Kampuni ya *Resolute Tanzania Limited* walipokuja kuwekeza pale Nzega walipewa ruhusa ya kujenga Kiwanja kingine cha Ndege kwenye eneo la mgodi wao badala ya kutumia kile cha umma ambacho tayari kilikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anipe ufanuzi kuhusu suala hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti hivyo viwanja vinavyojengwa kwenye migodi, kwenye hospitali za Makanisa, kwenye mbuga za wanyama, kwenye vitalu ni *private airstrips* hizo haziruhusiwi ndege kutoka nje ya nchi kutokea kwenye viwanja hivyo. Kwa hiyo, huo wasiwasi aliokuwa nao hauna msingi wowote.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilimwombwa Mheshimiwa Waziri aweze kutupatia majibu kuhusu wafanyakazi wa *TRL* wakati Kampuni ya *RITES* waliponunua hisa asilimia 51

kuna wafanyakazi takribani 1,900 hivi walilipwa mafao yao kuanzia milioni sita kwenda milioni 47 mpaka milioni 50. Lakini baadhi ya wale ambao walilipwa mafao hayo wamerudishwa kazini kwa mkataba. Lakini kuna wafanyakazi wengine takribani 2,700 mpaka sasa hawajalipwa mafao yao wakati ule wa Shirika lilipokuwa linabinafsishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwalipa mafao yao hawa wafanyakazi inakuwa ni sehemu ya kukata tamaa na kufanya vitendo viovu dhidi ya njia zetu za reli na mambo mengine ambayo siyo mema hata kuyatamka. Sasa naomba majibu kwa Mheshimiwa Waziri hawa wafanyakazi ambao bado hawakulipwa mafao yao, wana utaratibu gani za kuwafanya waweze kupata stahili zao ili waweze kuendesha shirika letu vizuri kwa maslahi ya Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbatia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuhama kwa waendeshaji wa shirika hili kuanzia *East African Railways* baadaye TRC na baadaye TRL wako wafanyakazi ambao walipunguzwa na wako wafanyakazi ambao *wali-retain* kazi zao, wale waliokuwa wamepunguzwa walilipwa mafao yao wakaondoka. Bahati mbaya wapo wale ambao kwa namna ambayo hata Wizara haikuelewa walirejeshwa tena kazini, Wizara tumekwishatoa agizo kwamba hawa wote sasa waondolewe kwa namna hiyo hiyo ambayo walikuwa wameingizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda kutumia nafasi hii kulielezea vizuri hili kwa wale ambao bado wako kazini, Sheria ya Mafao, Sheria ya Hifadhi ya Jamii iko wazi, mtu huwezi kulipwa *pension* ukiwa bado kazini. Kwa hiyo, hao waliopo kazini hawawezi kudai *pension* wakati bado wanaendelea na ajira zao. Ajira zao hazijawahi kusitishwa zinaendelea. Kwa hiyo, watakapokuwa wanafikia umri wao wa kustaafuli na wao watalipwa mafao kama Sheria inavyotaka.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu ndio hicho hicho. *Program 10 subvote 1001* kama nilivyosema, Mshahara wa Waziri. Katika Hotuba ya Waziri ukurasa 43 hiki kitabu tunaamini sana Hotuba ya Waziri kinaweza kuwa ni kweli asilimia 100 lakini kwangu mimi siamini. Sasa je, Waziri atanuhakikishia kwamba hizi tarakimu anasema Bandari za *Lake Tanganyika* zitakwisha kwa tarehe. Mimi naweka udhamini, Ubunge wangu wa Nkasi, ikipita tarehe hii aliyoandika kwenye kitabu na mimi Ubunge nauacha maana yake si kweli, wamemdanganya Waziri, hakuna kinachofanyika mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi ameshakimbia hakuna chochote kinachofanyika kuanzia Bandari za Kigoma mpaka Kipiri hakuna kilichofanyika. Waziri anatuhakikishia anataja tarehe na mwezi, si kweli, maana sasa tunakuwa tunadanganyana hapa. Hakuna Mkandarasi kule mwambao wa Ziwa Tanganyika. Sasa swali langu anihakikishie tarehe aliyosema, mimi na yeye kama

itakwisha tarehe hii na mimi naacha Ubunge, siji Bungeni tena, hii tarehe imeandikwa humu. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, unataka kusema nini hapa?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema taarifa hii si ya kweli.

**MWENYEKITI:** Unachosema, taarifa si ya kweli.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Anihakikishie kama ni sahihi. Kama ni sahihi na mimi nauacha Ubunge. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kulaumiwa baadaye. Mheshimiwa Keissy anajishtaki kwa wapiga kura wake yeye mwenyewe sasa hivi, kwa sababu ninachotaka kusema ni kwamba, hizi tarehe tulizoweka hapa ni mkataba kati yetu na mkandarasi. Asipotimiza hiyo tarehe tunadai fedha. Pengine hajawahi kusikia *term* ya *liquidated damages*, ndiyo tunachodai hicho. Sasa niseme nini, niseme kwa sababu wanaweza wakandarasi hawa wasifanye, kwa hiyo, niache kuandika tarehe!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naandika hii tarehe huku Wakandarasi wote nchini wakijua kwamba tumekuja watu ambao hatupati taarifa kwa simu. Hivi sasa mfano, kesho Mheshimiwa Naibu Waziri anaondoka hapa kwenda kwenye ukaguzi Songwe kuona kama Mkandarasi yuko pale. Atatoka pale kuelekea kwingine sijui kama mwenzetu una ubavu kumfuata Waziri kule

maana wewe unaongea ukiwa hapa huelewi mambo yanayotendeka kwenye Jimbo lako. Ahsante.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze Dkt. Mwakyembe kwa kazi yake nzuri. Nataka kusema kwa upande wa Kigoma mabehewa sasa yanakwenda kule ni ya daraja la tatu, nataka kujua utaharakisha vipi ili tuweze kupata daraja la pili na la kwanza hasa kusaidia wagonjwa wanaotoka Kigoma kuja Dar es Salaam kwa matibabu ili waje wamelala. Je, utafanya kwa uharaka kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kwa upole kabisa nitofautiane kidogo na mdogo wangu Obama kwamba Kigoma kwa sasa zinakwenda behewa za abiria za aina mbili, daraja la kwanza na daraja la tatu. Jana tumepitisha hapa behewa za daraja la kwanza zikienda Kigoma. Daraja la pili ndizo zilikuwa zimeharibika sana *beyond repair*. Kwa hiyo, tunayo mabehewa ya aina mbili yanayokwenda kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika huu mkakati tullionao wa mabehewa 22 mapya na kukarabati mengine mabehewa ya daraja la kwanza yataongezeka na tunao utaratibu wa kutaka *phase out* hilo daraja la tatu ili tubakie na mabehewa angalau yenye hadhi kubwa zaidi kwa treni zinazofuata.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mujibu wa nyaraka tulizonazo tarehe 27 Machi, mwaka huu kuna kikao kilikaa kati ya Wizara ya Fedha na wawakilishi wa Kampuni *Wares Trading* ya *Lebanon*. Kwa mujibu wa hicho kikao ni kwamba, walikubaliana kwa sababu *Wares Internationally* inadai Shirika la Ndege la Tanzania *ATCL* fedha nyingi za ukarabati wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa hiki kikao ni kwamba walikaa na *Wares Intentional* ilidai kwamba wapewe Bandari ya Mtwara kwa sababu *ATCL* wameshindwa kulipa hayo madeni ili wa-*compensate* wapewe bandari ili waache kutudai haya madeni. Hiki kikao kilikaa na kiko kwenye *advance stage* na Waziri hajatujibu. Sasa tunataka kujua kama je, Bandari ya Mtwara iko salama na walioshiriki kwenye kikao cha kutaka kuchukua mali yetu kuwapa watu ili ku-*compensate* deni liliilosababisha na uzembe wa watu kadhaa waliokuwa wanafanya kazi *ATCL* watachukuliwa hatua gani?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge Wenje kwamba sina taarifa ya hicho kikao na kama kilifanyika nakuhakikishia over my dead body hawapewi Bandari ya Mtwara. Sioni msingi huo kwa sababu sikuhusishwa na mimi ndio mwenye sekta hiyo. Sasa kama kuna mwingine anaendesha vikao huko vyta kutoa vitu ambavyo viko kwenye Wizara yangu, basi aendelee na hiyo mikutano. Nina uhakika pengine huna taarifa

sahihi, ndio shida ya kufuatilia mno jamii *Forum*, ndio shida hiyo. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye mchango wangu nimeulizia ni jinsi gani Wizara imejizatiti katika kutoa elimu ya kujiokoa baharini hasa uvaaji wa *life jackets*. Tatizo limejitokeza kwamba meli zetu zinapakia abiria wengi sana. Lakini sijui Wizara inahakikisha vipi kwamba zile meli zinakuwa na vifaa vingi vya kuokolea na elimu hiyo wanayoitoa inawafikia walengwa.

Sasa nataka kujua ni mkakati upi ambao umewekwa kuanzia sasa na ukiangalia kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameelezea hata miezi ambayo ajali huwa zinatokea kwenye bahari au kwenye maziwa? Napenda kufahamu ni mkakati gani ambao atahakikisha abiria watakuwa wana usalama hasa ukizingatia akinamama na watoto ambao ndio wengi wanaopoteza maisha?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vullu kama ifuatavyo:-

Nataka kukuhakikishia kwamba hali sasa imebadilika kabisa kwa sababu viongozi wetu waandamizi wa Taifa hili Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, wameshatupa maelekezo ya kuvunja ule ukuta wa kwamba hili sijui ni ZMA hili sijui ni *SUMATRA*. Nimeshatangaza kuanzia sasa na nilishatangaza juzi wakati nasoma Hotuba yangu kuanzia nimetoa agizo kwa *SUMATRA* kuhakikisha

kwamba hakuna chombo chochote kilichopakia abiria kuruhusiwa kuondoka bandari yoyote hapa nchini kama haina vifaa hivyo vinavyohitajika kuwemo kwenye chombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida tunayopata tu nimeanza kupigiwa simu kwamba, wananchi wanalamika ndio kawaida hiyo. Mimi mwenyewe nimeshudua, nimekuwepo katika kukagua usalama ndani ya mabasi, abiria anakuja juu, anatukana kabisa matusi ya nguoni kwamba, unatuchelewesha tu hapa kwani tukifa unakufa wewe. Lakini ninachosema tutaendelea na maudhi hayo na huu utakuwa ndio utamaduni kuanzia sasa na kuendelea.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya sababu zilizotolewa na Nohodha wa *M.V. Skargit* iliyozama ni kuwa hali ya hewa ilikuwa mbaya, upopo ulikuwa mwingi, meli ikapigwa mtama, ikaanguka na ikazama. Lakini tunayo mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ambayo inatoa taarifa ya masaa 24 au zaidi juu ya hali itakavyokuwa baharini. Swali langu nauliza je, mamlaka ya hali ya hewa ilisaidiaje na inasaidiaje kuepusha ajali za aina hili baharini? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwanza kwa kutoa taarifa kwamba utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa siyo asilimia 100, sisi sasa hivi utabiri wetu uko katika *accurate* ya asilimia 84. Hili naomba tuelewane kwanza. Lakini la pili mamlaka ya hali ya hewa wao

wakishafanya utabiri wao wanapeleka ripoti hiyo *SUMATRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nahodha wa vyombo vyote wanapokuwa wanataka kutoka bandarini wanapata taarifa kutoka *SUMATRA* ya hali ya hewa baharini. Kwa hiyo, ni wajibu wa Nahodha mwenyewe kutumia taarifa aliyonayo ya hali ya hewa kuamua aende au asiende. Kwa hiyo, hata kama yule bwana alipata taarifa ilikuwa pia anao wajibu wa kujua kwamba kwa taarifa hii anaweza kwenda au asiende. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba tusiingie sana kwenye undani wa hili kwa sababu jambo lenyewe limeundiwa Tume na wako watu Mahakamani wanafanyiwa uchunguzi.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri, katika mchango wangu wa maandishi, niligusia na kutaka maeleo zaidi kuhusiana na hatima ya mabehewa ambayo yamepelekwa Zambia mpaka sasa hatuna fedha yoyote ambayo tumeipata, aidha, kwa kukodisha ama yameuzwa. Kwa hiyo, nataka kujua mabehewa haya ambayo hayapungui 40, yameuzwa ama yamekodishwa kwa Zambia na kiasi gani kama Serikali tunapata?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna hiyo taarifa ambayo tumeihakiki ya mabehewa siyo 40 ni 38 ambayo yapo yanazagaazagaa huko. Hilo

suala ilikuja mbele ya Baraza la Mawaziri, tumelifanyia mkakati na naomba tu subira kwa sababu haya ni mambo ya kujadiliana na wenzenu polepole. Naomba tu tusubiriane, tuvumiliane hili suala tunalijua na tunalifanyia kazi.

**MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye hizi fedha ambazo zinaombwa ziko fedha za kufufua reli ya kati jambo ambalo jema na sisi wadau wa reli ya kati tumelipongeza sana. Nataka tu ufanuzi kwamba hii reli ina matawi yake kuna Kaliua, kuna Mpanda, Tabora mpaka Mwanza na kuna Singida Manyoni. Nimepekua nimeona matawi yale mawili mengine yametengewa fedha, lakini tawi la Singida- Manyoni sikuona naomba tu ufanuzi Waziri anisaidie anatoa kauli gani kuhusu hili tawi? (*Makof*)

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimjibu kaka yangu Mheshimiwa Chiligati kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa hatukutenga fedha kwa ajili ya njia ya Manyoni kwenda Singida. Yote hii ni kwa sababu tuliamini na mkakati wetu ni kwamba, kwa fedha ndogo tuliyonayo tukitekeleza miradi michache ikafanikiwa, Manyoni – Singida ni rahisi sana kutekeleza kwa sababu njia yao bado ni nzuri na leo hii tulikuwa tunaongea na Mtendaji Mkuu wa *RAHCO*, wanaanza kutembeza kiberenge chao kuangalia wapi pameharibika. Yote haya ni maandalizi. Hivyo baada ya kusogea mbele na miradi iliyopo sasa hivi, tutaingia kwa upande wa Manyoni – Singida.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni namba 104(2) tunaingia katika upitishaji wa mafungu kwa ujumla wake.

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ... Sh.394,535,000/=  
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ... ... Sh. 644,293,200/=  
Kif. 1004 – *Government Communication*  
                  *Unit* ... ... ... ... ... Sh. 133,545,000/=  
Kif. 1005 – *Procurement Management*  
                  *Unit* ..... .... .... .... .... Sh. 161,361,000/=  
Kif. 1006 – *Internal Audit Unit* ... .... Sh. 158,849,000/=  
Kif. 1007 – *Legal Service Unit* ... ....Sh. 137,862,000/=  
Kif. 1008 - *Inform.and Comm.*  
                  *Tech. Unit* ... .... .... .... Sh. 137,279,000/=  
Kif. 2005 – *Transport Infrastructure*  
                  *Division* ... .... .... .... .... Sh. 304,241,000/=  
Kif. 2006 – *Transport Services*  
                  *Division* .... .... .... .... Sh. 60,543,258,400/=  
Kif. 5002 – *Transport Safety and Envirnt*  
                  *Division* ... .... .... .... .... Sh. 327,583,000/=

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **FUNGU 62 – Wizara ya Uchukuzi**

Kif. 1003 – *Policy and Planning*... ...Sh. 7,112,130,000/=  
Kif. 2005 – *Transport Infrastructure*  
                  *Division*... .... .... .... Sh. 128,900,000,000/=  
Kif. 2006 – *Transport Services*  
                  *Division* .... .... .... .... Sh. 116,520,000,000/=

Kif. 5002 – *Transport Safety and Envirnt*  
*Division* . . . . . Sh. 226,000,000/=

*(Bunge lilrudia)*

## **TAARIFA**

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati na kuitia Makadirio na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Uchukuzi, Fungu namba 62 kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 mafungu kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa  
Mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuitisha bajeti hii, naomba sasa niwatakie kila kheri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na timu ya watalaam wote katika Wizara yenu. Kwa kweli Watanzania wanategemea kuona mabadiliko makubwa. Hasa katika haya matukio mazito ya ajali na mambo mengine ya namna hiyo. Basi tunamwomba

Mwenyezi Mungu awape nguvu na imani, uzalendo na Utanzania wa hali ya juu ili muweze kutusaidia kutupeleka mbele zaidi kwenye sekta hiyo mliyokabidhiwa na Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Waziri nawatachia kila la kheri.

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo hapa mezani, muda wa kuahirisha shughuli za Bunge umefika kwa hiyo, sasa naahirisha shughuli hizi za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 jioni Bunge liliahirishwa mpaka  
Siku ya Ijumaa, Tarehe 3 Agosti, 2012  
Saa Tatu Asubuhi)*